ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini - Tarehe 11 Juni, 2015

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ya mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Marina Joel Thomas (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka 2015/2016. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 21

Juhudi za Kupunguza Maambukizi Mapya

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la serikali ni kufikia 03 (sifuri tatu), kwa maana ya kwamba, unyanyapaa 0 (sifuri), maambukizi mapya 0 (sifuri), UKIMWI 0 (sifuri). Na kwa kuwa katika kijiji cha Mochwari kilichopo *Fidel Castro* katika Jimbo la Wawi, kila siku wananchi wa rika mbali mbali kwa kiasi kikubwa wanaendelea na matumizi ya mihadarati pamoja na pombe za kienyeji zinazoathiri sana afya pamoja na baadhi ya viungo vya binadamu na hatimaye vijana hao kujiingiza katika ngono uzembe, tendo linalopelekea maambukizi mapya.

Je, Ofisi kupitia Tume ya Ukimwi imechukua juhudi gani katika kupunguza maambukizi mapya pamoja na UKIMWI katika eneo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake Nam. 21 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba eneo la Mochwari ni moja kati ya maeneo hatarishi ndani ya jamii na kwamba vitendo viovu vinavyoendelea hapo vinaweza kusababisha pamoja na mambo mengine, kuendelea kwa maambukizi ya VVU na hatua muhimu ambazo serikali inazichukua ni kama hizi zifuatazo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kudhibiti vitendo hivyo viovu, serikali kupitia Jeshi la Polisi wanafanya doria za mara kwa mara na kuwakamata wahalifu hao na kuweza kuwachukulia hatua za kisheria. Doria hizi zinakusudiwa kuwa endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya UKIMWI, kupitia mpango shirikishi wa jamii kwa kupambana na UKIMWI ilianzisha Kamati Maalum na kuweza kuijengea uwezo ili iweze kufanya kazi ya kutoa elimu, ushauri nasaha na pia kupeleka huduma za upimaji wa VVU kwa jamii katika maeneo hayo ya Mochwari .

Mhe. Mwenyekiti, Tume ilihamasisha kuanzishwa kwa kikundi cha Polisi Jamii na baadaye kukijengea uwezo kikundi hicho kwa kukipatia mafunzo jinsi ya kufikisha elimu ya UKIMWI na athari ya Dawa za Kulevya kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na changamoto zilizopo hapo, Tume ya UKIMWI inakusudia kuishirikisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kusini Pemba ili iweze kusaidia kutatua tatizo hilo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mhe. Waziri, mdogo wangu pale Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji naomba niulize swali dogo sana la nyongeza.

Kwanza kabla ya kuuliza swali napenda nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, mdogo wangu Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kwa kuweza kufika Mochwari na kujionea mwenyewe hali ilivyo. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Mohammed Aboud.

Kwa kuwa Mhe. Waziri ametwambia hapa kwamba Jeshi la Polisi huwa linafika mara kwa mara na doria na kuwatia mbaroni wale vijana wanaotayarisha ile pombe haramu (gongo) pamoja na kuuza bangi.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazopelekea kwamba hawa waliokwishakamatwa na kupelekwa Polisi badala ya kufunguliwa mashtaka na hatimaye kuwajibishwa siku ya pili unawaona pale pale wanauza gongo na kuuza bangi.

(b) Kwa sababu hili suala la gongo na bangi sio tu linaweza likasababisha hatari za UKIMWI, lakini linaweza likasababisha vijana wetu wanapata tatizo sana pale, kwa sababu *alcoholic drinks.* Hivi vinywaji vikali wanapovitumia sana huwaathiri ule mfumo wa usafirishaji hisia katika miili yao, yaani ile *transmission of impulses across synapses*, inakuwa tatizo na hatimaye hata ukiwapiga sindano ya ganzi haiwashiki, jambo ambalo wanapata tabu sana madaktari wetu kuwatibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saleh Nassor Juma uliza swali, unatoa hotuba wewe sasa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Baada ya dibaji hiyo fupi Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana naomba Mhe. Waziri anijibu, ni lini serikali kwa kutumia Jeshi hili la Polisi litaweza kuwachukulia hatua wale ambao walikwenda wakawapiga Polisi Jamii pale akiwemo Bwana mmoja anaitwa Miserure.

Hawa Polisi Jamii walipokwenda kuwadhibiti pale walipigwa vibaya sana na walevi, lakini mpaka leo hii hakuna hatua iliyochukuliwa. Ni lini serikali itawachukulia hatua wale waliowapiga Polisi Jamii siku ile waliokwenda kutaka kuwakamata hawa wapika gongo na wauza bangi.

Je, kutochukua hatua si kuwarejesha nyuma hawa Polisi Jamii ambao mmewaanzisha nyinyi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Saleh Nassor Juma nimletee majibu haya kwa maandishi, kwa sababu haya anayonielezea mimi ndio nayasikia kwake kwa mara ya kwanza, na taarifa hizi sina, inabidi nizifuatilie kutoka Vyombo vya Ulinzi na Usalama ikiwemo Polisi ili niweze kumpatia majibu yake.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri.

Kwa kuwa hivi karibuni tu au jana tumerudi katika safari kutoka Rwanda tukiwa pamoja na yeye Mhe. Waziri na Mwenyekiti. Mhe. Waziri tulichokiona kule

wanawake wamejipanga kuendeleza masuala yao ya kushirikiana kuhusu suala la UKIMWI na masuala mengine ya madawa ya kulevya.

Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuwaelimisha wananchi kuhusu suala hili, na kwa kiasi kikubwa kule wenzetu wa Rwanda wamefanikiwa.

Je, Mhe. Waziri kwa kushirikiana na wanawake wa hapa Zanzibar pamoja na serikali, ana mikakati gani na yeye kuelimisha suala hili ili kupunguza madawa ya kulevya pamoja na UKIMWI. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumerudi kwenye ziara ya siku mbili jana jioni kutoka nchini Rwanda, ambapo tulikwenda kujifunza harakati za Umoja wa Wabunge Wanawake wa Bunge la Rwanda ambao wanashirikiana na jamii katika masuala haya ya kijamii, ili kupunguza uhalifu wa aina mbali mbali ndani ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, maana ya kujifunza ni kwamba unaporudi uweze kutumia ile elimu ili na wewe uweze kupata mafanikio ambapo wenzetu wa Rwanda wameweza kufanikiwa.

Ninachomuahidi Mheshimiwa ni kwamba, kupitia umoja wetu huu wa UWAWAZA, Wawakilishi Wanawake waliomo humu ndani, tutaishirikisha jamii kikamilifu ili kuweza kupambana na mambo haya mawili, kama vile ambavyo tumewaona wenzetu; njia na mikakati ambayo wanatumia katika kushirikiana na jamii katika kutoa elimu ili kupambana na uhalifu huo.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sehemu hii ya Mochwari imeshazungumzwa mara nyingi kuhusiana na uhalifu unaofanyika pale. Na kwa kuwa masuala ya kinyume cha maadili ya Kizanzibari yanayotendeka pale yamechukua muda mrefu, kwa kuwa Askari Polisi wanafanya doria mara kwa mara pale ili kuzuia harakati hizi.

Je, ni watu wangapi wamekamatwa, na ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa dhidi yao ili kulikomesha tatizo hili katika eneo hilo. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye anayeshughulikia masuala haya ya ulinzi, na zaidi anashughulika na mambo ya ulinzi na usalama na Polisi ana majibu kuhusu suala hili ambayo tayari aliyaeleza humu ndani ya Baraza, naomba tu amkumbushe Mhe. Mjumbe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chambani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ni hivi karibuni tu, tulijibu swali hili ndani ya Baraza lako Tukufu, na Kanuni zetu zinatueleza wazi kwa kuwa kuna muda maalum kunapotolewa taarifa ama swali kujibiwa, bado hatutakuwa na sababu ya kulijibu tena swali hilo zaidi ya yale maelezo tuliyoyatoa. Hata hivyo, hili jambo liko Mahakamani si vyema sana kuzungumzia mambo ambayo tayari yako Mahakamani.

Kwa hivyo, naomba nitoe taarifa hiyo tu Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Nam. 33

Rais wa Ujerumani Kuingia Zanzibar kwa Kutumia Usafiri wa Baharini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Rais wa Ujerumani amesafiri kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar kwa kutumia boti, na baadae kutembea kwa miguu na kupata nafasi ya kusalimiana na watu wa Zanzibar.

(a) Kwa kuwa kiongozi huyo alifuatana na vyombo vya habari vikubwa duniani, tutarajie nini katika suala la kuimarisha utalii na kuitangaza Zanzibar kuwa ni visiwa vya amani.

(b) Ni viongozi wangapi wa Kimataifa wamewahi kuingia na kutoka Zanzibar kwa kutumia utaratibu aliotumia Rais wa Ujerumani au yeye ndio kiongozi wa kwanza.

(c) Kwa kuwa utaratibu huo wa kusafiri kwa boti umepunguza gharama kubwa, serikali ina mpango gani wa kutumia gharama nafuu kwa viongozi wake wa Kitaifa badala ya kukodi ndege.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Rais wa Ujerumani amesafiri kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar kwa kutumia boti na baadaye kutembea kwa miguu na kupata nafasi ya kusalimiana na wananchi wa Zanzibar.

Kutokana na ziara hiyo ya Rais wa Ujerumani, sasa naomba kumjibu Mheshimiwa kwamba:

(a) Kutokana na Rais huyo kufuatana na vyombo vya habari vikubwa duniani tutarajie nchini kwetu kutangazwa zaidi utalii. Sababu ya kusema hivyo ni kuwa Rais huyo wa Ujerumani ameendelea kutangaza utalii kwa asilimia kubwa sana, na pia kuendeleza amani na utulivu wa kidini. Hayo ni matokeo ya ziara ya kiongozi huyo.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo mbali mbali vya habari vimekuwa vikitangaza hivyo, kutokana na hali hiyo tutarajie kuongezeka viwango vikubwa vya watalii kutoka Ujerumani kwa kupitia njia zote mbali mbali za baharini na kwenye viwanja vya ndege.

(b) Katika kipindi cha zaidi ya miaka Arubaini (40) Rais wa Ujerumani ni kiongozi wa kwanza kutumia usafiri huo wa kutumia boti au meli na baadae kutembea kwa miguu kukutana na wananchi wa Zanzibar.

(c) Viongozi wetu wa Kitaifa wamekuwa wakitumia usafiri wa boti wanapopenda, lakini siwezi kushauri viongozi hao kutumia usafiri huo kwa sababu gharama zake ni nafuu kuliko kukodi ndege. Siwezi kushauri hivyo, kwani kanuni na miongozo ya safari za watumishi wote wa umma wakiwemo Viongozi wa Kitaifa zinatolewa na Tume ya Utumishi Serikalini kwa kuzingatia vigezo maalum vya utumishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake na nimpongeze, alipokuwa akijibu swali la msingi viongozi wetu wamekuwa wakitumia boti wanapopenda, lakini sasa hatuwezi kuwashauri wakatumia usafiri wa boti kwa kuwa ni usafiri nafuu.

Nimuombe Mhe. Naibu Waziri tunge-*save* kiasi gani fedha hizo zikawasaidia wanafunzi wetu kuhusu madeski na madawa ambayo yamekuwa ni tatizo sugu kwa wananchi wetu.

Je, kutoka hapa mpaka Dar es Salaam kutumia ndege ni gharama shilingi ngapi.

La pili, alipokuwa akijibu swali alisema ni miaka 40, hapo nyuma kuna Rais yeyote aliyetumia boti, maana alipojibu swali la msingi kasema miaka 40 haijawahi kutokea.

Je, huko nyuma kuna Rais aliwahi kutokea katika suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa boti kwa kawaida ni uamuzi wa kiongozi mwenyewe anavyoamua. Rais wa Ujerumani aliamua kufanya hivyo na baada ya kushauriana na serikali, serikali ikakubaliana na uamuzi huo.
Nataka nimpongeze sana Rais wa Ujerumani kwa uamuzi huo, kwa sababu ulisaidia sana katika kukuza utalii wa Zanzibar katika nchi mbali mbali duniani ikiwemo Ujerumani.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu safari za viongozi wetu wa Kitaifa hizi zinaratibiwa kwa utaratibu maalum kwa ajili ya usalama wao, na kwa ajili ya maamuzi mahsusi ya utendaji wao wa kazi.

Kwa hiyo, kutumia ndege ni jambo ambalo linakubalika kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kisheria na kwa mujibu wa kiutaratibu wa kiulinzi na usalama.

Hivyo walinzi wetu wametushauri vizuri kwenye jambo hili na tunakubaliana nao na hata Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwenyezi Mungu akimjaalia kumpandisha cheo basi ajue atatumia usafiri huo hata akitaka wa boti basi atatumia usafiri huo. Kwa hivyo, ni utaratibu wa kawaida.

Kuhusu masuala ya gharama ni mambo ya kawaida na zimo katika utaratibu wa Mfuko Mkuu wa serikali, kwa hivyo, ni haki yao kuitumia hiyo. Kama alivyowekwa na haki anapolipwa posho hapa Barazani. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na nikupongeze kwa kurudi safari yake ya Rwanda, kwa kweli wanawake wanaweza Mwenyezi Mungu awabariki.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kiongozi anatakiwa awe mfano mzuri kwa wananchi wake na viongozi mbali mbali wa Zanzibar wamekuwa wakisafiri Unguja na Pemba kwa kutumia boti nyakati tofauti, na serikali hii imekiri hilo limefanyika kwa Dkt. Salmin Amour, hata Rais Mstaafu Rais Aboud Jumbe Mwinyi, na kwa

kuwa viongozi ni kigezo kizuri kwa wananchi, na kwa vile Rais wa Ujerumani ambaye SMZ iliwahahakishia usalama wake, ni kwa nini sasa Rais Shein kabla ya kumaliza awamu hii asiamue angalau siku moja akasafiri kwa boti kwenda Pemba kuona angalau ule Mkondo wa Nungwi unavyowatesa watu.

(b) Nchi yetu ina tatizo kubwa la fedha, na fedha ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi zote duniani. Kwa nini hatupunguzi gharama za matumizi ya safari za ndege kwa viongozi *VP I* na *VP II* akiwemo yeye na mimi na baada yake viongozi hawa wakasafiri kwa boti na hata jahazi kwa ajili ya kuaga vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Rais Ali Mohamed Shein kusafiri kwa boti. Mhe. Rais anaweza kusafiri kwa boti wakati wowote atakapoamua . Lakini moja katika haki zake ambazo tumekubaliana ni kusafiri kwa chombo cha ndege kwa ajili ya usalama wake kwa ajili ya uharaka wake, kwa ajili ya kutimiza matakwa ya mahitaji ya shughuli anayokwenda kuifanya.

Kwa hiyo, Mheshimiwa usafiri wa boti kati ya Pemba - Unguja, Unguja- Dar- es Salaam. Lakini Rais wetu huyu anasafiri kwenda sehemu mbali mbali za nchi yetu.

Kwa hivyo, huna namna yoyote ile utasema atatumia boti anapotaka kwenda Mwanza anapotaka kwenda pahala pengine na kadhalika anapokwenda nje ya nchi. Kwa hiyo, ni utaratibu wa kawaida, sikudhani kabisa kabisa kama mpaka leo tutafikiria kuulizia kuwalazimisha viongozi wetu kusafiri na boti wakati tunajua kabisa namna gani wanavyohitajika kufika kwa wakati katika maeneo muhimu ya kutekeleza majukumu yao ya kitaifa. Ni utaratibu uliowekwa kisheria kutumia usafiri wowote ule.

Kwa hiyo, wanapoamua kusafiri kwa boti ni uamuzi wa viongozi, na hilo halikataliwi na ni kweli huko nyuma baadhi ya viongozi wetu akiwemo Dkt. Salmin Amour na wengine walitumia usafiri wa boti pale ambapo wameamua kutumia hivyo, lakini mara nyingi wametumia ndege, na ndege kwa sababu ya uhakika wa usalama wao, na kwa sababu ya uhakika wa kufika kwa wakati katika maeneo wanayohitajia. Kwa hiyo, sidhani wala si vizuri kuwalazimisha viongozi wetu kwamba lazima watumie usafiri wa boti.

Hata hivyo, kuhusu kupunguza matumizi. Mheshimiwa ni kweli utafikiria unapunguza matumizi lakini ile *disturbance* inayotokea kwa wasafiri wanaotumia hiyo boti nikupe mfano tu, siku aliyokuja Rais wa Ujerumani ilibidi abiria tuwaweke mahali mbali wakae kwa muda wamngojee Rais wa Ujerumani ashuke, unawaweka mle ndani wana mizigo wao na mambo chungu nzima.

Kwa hiyo, ukitizama kwa ufupi unasumbua abiria wanaotumia ile meli ya abiria. Gharama zake ni kubwa na inawezekana kabisa ukakera wananchi wetu kwa sababu ya mambo ambayo tunaweza kuyafanyia utaratibu mzuri, yakaondoa bughudha kwao, na shughuli zikafanyika vizuri na usafiri wa viongozi wetu ukaenda vizuri.
Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Kwanza mimi nampongeza sana Rais wa Ujerumani kwa kuonesha uzalendo na imani kubwa kwa Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla kwa ajili ya kusafiri kwa boti kushirikiana na wananchi akaja Zanzibar.
Lakini napenda nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa tumeshuhudia alipokuja Rais wa Marekani zilitangulia ndege na ulinzi mkubwa nchi nzima; mbwa, ndege na askari wa kila aina.

Je, Mhe. Mwenyekiti kwa sababu Rais wa Ujerumani alikuja kwa boti, ni ulinzi gani uliimarishwa na kwa siku ngapi ziliimarishwa ulinzi, na je, baada ya kurudi kulionekana kuna tofauti gani wa ulinzi mpaka ikabidi Rais wa Marekani kuna na mbwa na ndege. Je, imani hiyo ilionekanaje.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali hili naomba nitoe maelezo yafuatayo:

Kwanza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein ni mfano wa kuigwa na wananchi wote na viongozi wote katika kuwapenda wananchi wake na katika matumizi yake pia ya nafasi yake ya Urais. Baada ya maelezo hayo naomba niseme yafuatayo:

Mhe. Subeit Khamis Faki aelewe kwamba kiongozi yeyote anapoondoka katika nchi yake kwenda nchi nyengine ama anaondoka katika eneo moja kwenda eneo jengine la nchi yake lazima utangulie ulinzi kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa kiongozi wao kabla hajafika kule endako na kama kuna jambo lolote ambalo litasababisha dalili tu za kuvunjika usalama wake, kiongozi huyo hulazimika kuambiwa asiende safari hiyo, na ndio maana pale unaposikia kwamba kiongozi fulani amesitisha ziara ya kwenda pahala fulani, kutokana na sababu hizo za kiusalama zaidi. (*Makofi*)

Lakini kuhusu suala lake aangalie *reference* ya ziara ya Rais Obama ambayo ameifanya kule nchini Kenya, akiangalia *reference* hiyo basi atajua, na yeye Rais wa Ujerumani alipokuja hapa mambo gani yalifanyika mpaka yakamhakikishia yeye kuja katika nchi yetu ya Zanzibar. Walihakikisha kwamba usalama wake katika muda wote atakapokuwepo Zanzibar na Tanzania kwa jumla utakuwepo,

ndio maana akatembelea Zanzibar na manufaa yake ya ziara hiyo tunayaona baada ya kufuatia kwa ziara ya Dkt. Ali Mohamed Shein, ambayo alikuweko nchini Ujerumani na amerejea nchini jana inatokana na faida ya Rais wa Ujerumani baada ya kuja Zanzibar na kuona utulivu na amani na ustaarabu wa watu wa Zanzibar, ndio maana Rais amepata mualiko na kwenda nchini Ujerumani na mafanikio yake tutayaona baadae.

Ahsante sana. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2015/16

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Majadiliano yanaendelea nina wachangiaji kumi mpaka sasa hivi, na jana wakati Mhe. Mwenyekiti anamaliza alitaja majina ya Wajumbe ambao wataanza.

Mhe. Hija Hassan Hija ningeomba kidogo umpe nafasi Mhe. Farida Amour amepata dharura na nafasi ya pili utachangia wewe. Ahsante, nashukuru kwa ridhaa yako.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia na kuniamsha salama na kufika hapa kwenye Baraza lako Tukufu na kunipa nafasi hii ya mtu wa mwazo leo kuchangia katika hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuwa na mchango wangu mdogo sana katika wizara hii.

Nataka nianze na ukurasa wa 8 lakini kabla ya hapo naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote jinsi walivyofanya kazi ya ziada katika kuiandaa hotuba hii, na yeye pia akaamua kuisoma hotuba hii kwa umakini sana na sote tumeifahamu.

Pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na ukurasa wa 8 katika ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Farida Amour unaombwa uongeze sauti kuna watu wengine hawasikii vizuri.
Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimekuelewa. Nasema nitaanza ukurasa wa 8 katika mchango wangu katika sekta hii ya uvuvi.

Mafanikio katika sekta hii ya uvuvi. Miongoni mwa mafanikio hapa waliyoyataja moja ni:

"Kutiwa saini kwa makubaliano baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Shirika la Korea juu ya kuanzishwa mradi wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki huko Beit-el Ras".

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri, lakini kwa sababu hili suala la kuzalisha vifaranga lipo kwa muda mrefu, na mwanzo kulikuwa kunataka kujengwa eneo jengine sasa hapa ndio lengo limepatikana na saini tayari. Kwa hivyo, naomba watufafanulie tu ni muda gani tunategemea itakuwa tayari hatua hii na kuanzisha huo mradi wa ujenzi wa hicho kituo na kuanzisha vifaranga.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wengi wamehamasika katika kufuga samaki hawa. Sasa inakuwa ni tatizo kupatikana kwa vifaranga. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atufafanulie zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huo huo nataka nitoe pongezi za dhati kabisa kwa kukamilika kwa ujenzi wa soko la mboga mboga na samaki Tumbe. Hili lilikuwa ni tatizo kubwa la muda mrefu, kilikuwa ni kilio cha Wazanzibari na Wapemba hasa kutoka Kaskazini Pemba, kwa sababu lile soko ni kubwa, ni pwani, lakini lilichukua muda mrefu lakini sasa nachukua fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa kukamilika kwa soko hili.

Pia namuomba Mhe. Waziri katika hili jambo lolote lile bila ya kulifuatilia ukaliona na mwenendo wake na maendeleo yake itakujakuwa tena uharibifu. Kwa hiyo, tunaomba sana wizara yako kupitia sekta hii ifuatilie, itafute muda maalum wa kwenda kufanya ukaguzi na kuwapa mawazo na kubadilishana mawazo, na wale watu wanaohudumia lile soko ili lidumu kwa muda mrefu sio kila siku tunategengeneza jambo hilo kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye ukurasa wa 9 naingia kwenye changamoto. Changamoto katika sekta ya uvuvi zilielezwa hapa ni nyingi, mojawapo ikiwa ni uhaba ya nyenzo za kufanyia kazi za doria unaopelekea kuzidi kwa uvuvi haramu.

Mhe. Mwenyekiti, hili pia ni tatizo, kwa sababu wavuvi wetu katika bahari zetu tunaingiliwa na watu katika kuvua waliokuwa si halali kama walivyozungumza hapa katika changamoto yao. Sasa nyenzo za kufanyia kazi ni muhimu sana. Sasa kama watu wetu hawajapewa nyenzo za kufanyia kazi kweli kweli watashindwa kulinda doria itakuwa watu wanahangaika na baadae watakuja kupata athari kubwa. Kwa hiyo, naomba changamoto hii serikali ipo iipe uzito na ilichukulie hatua kuwatafutia nyenzo watu wetu katika kupelekea hali hii.

Pia kuna upotevu wa mazao ya baharini kwa kuharibika baada ya kuvuliwa kutokana na usarifu mdogo. Hizi changamoto ni kubwa, na katika hili Mheshimiwa kwa sababu kuna mambo mengi yanayotakiwa hapa yafanikishwe na nchi yetu imezungukwa na bahari na wavuvi ni asilimia kubwa katika nchi yetu. Sasa baada ya kinachovuliwa kama kitakaa na kuharibika hakijatayarishiwa mbinu maalum itakuwa ni tatizo na hatuendi mbele, na lengo ni kuondoka katika umasikini na kubadilisha kipato cha kila mtu.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali kupitia wizara hii kujitahidi sana katika suala la kuwatafutia watu wetu hawa vifaa maalum vya kusarifu hichi kinachovuliwa.

Mhe. Mwnyekiti, nikija kwenye suala la mwani, hapa katika changamoto pia wamesema ni bei ndogo ya mwani. Kweli mwani hauna bei lakini kwanza kabla ya hapo naomba niipongeze kwa dhati kabisa serikali kupitia Wizara ya Uwezeshaji kwa kuwapatia wakulima wa mwani vitendea kazi kwa njia ya mkopo, lakini vitatusaidia sana katika harakati za kuvusha ule mwani kutoka baharini na kupeleka maeneo ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, masuala haya lazima wizara mbili hizi zifanye kazi kwa mashirikiano ya karibu sana na inaonesha wanafanya kazi kwa mashirikiano. Kwa sababu Wizara ya Uwezeshaji kazi yake ni kusaidia, na hapa wamesaidia jambo kubwa sana, kwa sababu wanawake ndio walimaji wakubwa wa mwani, na hapa walikuwa wanapata matatizo makubwa ya kubeba mwani kwa kichwa kuvuka na vidau vidogo vidogo. Lakini sasa hivi wamepewa vifaa maalum vya kuvushia huo mwani.

Lakini sasa kwa sababu mwani una matumizi mengi, na nimeona humu hata kitabu tulichopewa asubuhi leo kutoka Ikulu; "Serikali kwa Maendeleo ya Wanachi" kinasema SMZ inavyoliimarisha zao la mwani kwa kufanyia vifaa mbali mbali. Lakini bado Mhe. Mwenyekiti, panahitaji nguvu za ziada za kutoa mafunzo kwa watu, kwa sababu mwani unaovuliwa ni mwingi, bei ni ndogo lakini yakitolewa mafunzo maalum katika kila eneo lilokuwa na wakulima wa mwani wakapewa angalau na wao wamkapata kujua mwani huu unatengenezewa nini, na baada ya kwishatengenezwa pia wakawatafutia soko, kwa sababu soko ndio tatizo hasa kwa kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji na Wizara ya Biashara. Naiomba sana serikali kupitia wizara hii kuwatafutia wakulima wetu wa mwani, ili na wao wapate angalau kujiendesha kujikimu kimaisha kwa sababu wengi wakulima wa mwani ni wanawake, na wanawake ndio wanaopata tabu sana majumbani.

Kwa hiyo, naomba wanawake hawa tuwaonee huruma kwa kuwatafutia masoko ili kupata bei za mwani kwa sababu unalimwa, ni mwingi, lakini kwa bahati bei ya mwani haijaonekana kukua.

Mhe. Mwenyekiti, katika muelekeo wa baadae wa sekta ya uvuvi, kuna muelekeo namba sita unasema kuwa kuwawezesha wavuvi kuvua katika kina kirefu cha maji.

Hili ni jambo zuri sana, lakini Mhe. Mwenyekiti, mkumbuke bahari ni bahari, na kama tunavyoiona meli zetu zinakumbwa na mitihani na misukosuko tunapoteza roho za watu wengi, na hawa ni vijana wetu tunataka kuwawezesha wavuvi katika kina kirefu cha maji.

Sasa naomba katika hili kabla hatujafanya hilo tujipange kwa dhati kabisa kuwatafutia vifaa vya kisasa na mafunzo ili vijana hawa badala ya kuwatafutia maendeleo tukaja tukawatafutia mauti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea nataka nije katika ukurasa wa 22, "Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo". Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba ninukuu kidogo:-

"Mhe. Spika, maendeleo ya sekta ya mifugo yanategemea sana afya ya mifugo yetu. Aidha, mifugo ndiyo chanzo kikubwa cha maambukizo ya maradhi kwa binadamu. Sasa Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo ina jukumu la kudhibiti maradhi kwa mifugo yetu kwa kutoa huduma za kinga na tiba za maradhi ya mifugo.

Idara pia ina jukumu la kuhakikisha mifugo yetu haisambazi maradhi kwa binadamu na kulinda nchi yetu isipate maumbikizi ya maradhi ya mifugo kutoka nje ya nchi kwa kufanya ukaguzi na udhibiti wa wanyama wanaoingizwa nchini".

Mhe. Mwenyekiti, hili suala ni zuri na lipo kwa muda mrefu, kuna watu maalum wanakaa katika kukaa kudhibiti wanyama wanaoingia na kutoka, ili kupunguza kasi ya maradhi yanayoingia nchini kwetu kutokana na bidhaa mbali mbali zikiwemo hawa wanyama.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada zote zilizofanywa au zinazotegemewa kufanywa na Wizara hii, ni karibuni tu juzi juzi tulisikia taarifa kwenye vyombo vya habari, kwamba kuna mbuzi wengi tu wamekamatwa wameingia hapa kwa meli ya Bakhressa na kwenye magari, na mbuzi wale kwa bahati njema nataka niipongeze Idara ile iliyohusika na mambo yale waliangamizwa.

Sasa hapa tunalinda wanyama wanaoingia pengine wakiwa wazima, lakini katika nyakati nyengine wanaletwa wanyama tayari wameshachinjwa, sasa wale hatujui wanakotoka wako vipi.

Sasa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, suala hili la kufuatilia hili lisifuatiliwe kwa wale wanyama wanaoletwa hapa wakiwa wazima, kwa sababu kuna wengine kama wale walioletwa matani kwa matani (*tonnes),* kwa bahati mbaya wameonekana na athari wakaamua kuwaangamiza. Kwa hivyo hili ni suala zuri lakini linataka ufuatiliaji katika sehemu zote.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kidogo ninakuja kwenye ukurasa wa 24 *paragraph* ya mwisho hapa, kuna jumla ya *samples* 320 za maziwa ya ng'ombe, 150 za damu na 320 za kinyesi zilizochunguzwa, asilimia 46 ya *samples* hizo za maziwa ziligunduliwa kuwa na vimelea vya maradhi ya kiwele.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme asilimia kubwa ya Wazanzibari wanatumia maziwa katika kufanyia mambo mbali mbali. Lakini hapa kuna asilimia 46 imegunduliwa na vimelea na kila kichochoro tunayopita Unguja hii na Pemba, unakuta pahala pana vimeza wanauza maziwa; wengine wanatembeza kwa baiskeli, wengine wanatembeza kwa mapikipiki.

Sasa naiomba sana Serikali kupitia Wizara hii, kwa sababu maziwa yanatumika sana, kwa hivyo naomba sana waangalie kwa umakini hatma ya maisha yetu na maradhi kwa sababu ya haya maziwa. Kwa sababu hapa imeonekana ni asilimia ndogo, lakini sijui wengine wanatumia hekma gani za kufanya utafiti katika kujua kama kila yale maziwa tunayouziwa yanakuwa yapo salama.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee katika ukurasa wa 31, "Utekelezaji wa Malengo kwa mwaka 2014/2015". Hapa naomba ninukuu kidogo:-

"Wawakilishi wa wakulima wa mwani kutoka vijiji 53 walipatiwa mafunzo juu ya njia bora ya kilimo cha mwani na matumizi yake. Kati ya vijiji hivyo, wawakilishi watatu walitoka Kisiwami Pemba".

Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna mambo mawili. Kuna watu wanachukuliwa sehemu kwenda kutoa mafunzo mbali mbali katika maeneo tofauti. Kwa sababu ni sahihi, si kweli kama watu wote katika eneo moja watachukuliwa kwa kwenda kupewa mafunzo, lakini lengo la kupewa mafunzo ni baadae wale waliotoka kwenda kupewa mafunzo na mafunzo yale wayachukue na wayatumie kwa wenzao.

Sasa lazima mufanye uchunguzi baada ya kupewa mafunzo hawa watu. Je, mafunzo haya wameyaeneza kwa wengine au wamebakia nao wenyewe tu. Kwa sababu tabia hizo tunazo, wengi wetu mtu akishapewa mafunzo akirudi anakaa kitako elimu ile haiwezi kuitoa wakafaidika na wengine. Kwa hivyo naiomba sana Wizara ifanye ufuatiliaji baada ya kutoa mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nisogee kidogo karibu na kumalizia katika ukurasa wa 63, kwenye kiambatanisho Nam. 12.

Kwenye kiambatanisho Nam. 12 kuna malengo ya utekelezaji kwa mwaka 2014/2015. hapa kuna utekelezaji wa jumla. Jumla ya skuli 43 wanafunzi 605, walimu 42 na maafisa elimu 6 walipatiwa mafunzo juu ya athari za kichaa cha mbwa kwa binadamu. Mafunzo hayo yalifanywa katika Wilaya zote sita za Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nina swali. Haya mafunzo katika hawa walimu na wanafunzi yote yametolewa katika Wilaya sita za Unguja. Ninataka kujua kuhusu Kisiwa cha Pemba, ni wangapi waliopewa mafunzo haya, kwa sababu mafunzo ni muhimu na haya maradhi ya vichaa vya mbwa na wanyama wengine yanaenea Zanzibar nzima. Sasa na watu wa Pemba nao wanahitaji kupewa mafunzo ili wapate kujua jinsi ya kujikinga na matatizo haya.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kwa kusema katika kiambatanisho Nam. 14, "Malengo ya Utekelezaji kwa 2014/2015".

Hapa kuna eneo la Mkokotoni halikukidhi vigezo badala yake lilichaguliwa eneo la *SUZA* liliopo Beit el Ras katika kutengeneza hivyo vifaranga vya samaki. Sasa je, baada ya kwisha kuchaguliwa hilo, tutegemee baada ya muda gani litakuwa tayari hili ambao tutapata hivyo vifaranga, kwa sababu bado ninaendelea kusema vifaranga vya samaki ni muhimu na ni vichache mno.

Kuna watu ambao Mhe. Mwenyekiti, walianza mwanzo katika ufugaji wa hawa samaki, na watu hao sijui mumewachukulia uzito gani, angalau kuwapa motisha.

Ndani ya Wilaya yangu ya Wete kwa jumla Mhe. Mwenyekiti, kuna mabwawa mengi tu ya samaki ambao kuwa wengine wanazalisha vifaranga mpaka wanafikia watu kutoka maeneo mengine wanakuja wakinunua vifaranga vile.

Je, Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba Mhe. Waziri aniambie anawapa maana yake kama zawadi gani wale watu ambao wamechimba mabwawa yao, mabwawa yale ni kazi, yanatumia nguvu kubwa na idadi ya mchango au pesa wanazopatiwa ni kidogo mno.

Sijui Mhe. Waziri atanieleza ni kiwango gani anachowapa watu hawa, kwa sababu mabwawa ni mengi, nguvu wanayotumia ni kubwa mpaka inafika wakati watu wanashindwa kuyahudumia yale mabwawa.

Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri avifanyie tena tathmini vikundi vyote ama mabwawa yote ya samaki. Kwa sababu mabwawa haya ya samaki pia yanazuia kuua matumbawe yetu yaliomo ndani ya bahari. Hivyo namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie tena hili la wafugaji wetu hawa ili awasaidie nguvu ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa tunamkaribisha Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi hii, na naomba nitoe mchango wangu mfupi kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri kama ambavyo ameisoma jana.

Kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyosoma hotuba yake, na nipongeze Wizara kwa jumla kwa jinsi ambavyo wameandika hotuba hii; hotuba fupi lakini kwa kweli ni nzuri na imejieleza vizuri. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye uwezo wa Ofisi ya Mhe. Waziri, uwezo wa wafanyakazi *(main power)* ya Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi hii au Wizara hii kwenye jadweli Nam. 8 limeeleza jinsi ya idadi ya wafanyakazi na viwango vyao vya elimu. Ukifanya mahesabu hapa Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wenye elimu ya diploma na kwenda juu ni asilimia 31.7 na wale wenye chini ya diploma ni asilimia 68.3. Sasa utaona jinsi Wizara ilivyo kwamba kwanza ni Wizara ambayo ina wafanyakazi wachache, lakini viwango vya elimu vya diploma na kwenda juu ni chini ya asilimia 32.

Mhe. Mwenyekiti, niishauri Serikali, na niwaombe Wajumbe wenzangu kwamba fedha ya mafunzo ya wafanyakazi lazima iongezwe na isimamiwe.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Wizara ambayo inategemewa kuajiri Wazanzibari wengi, ni Wizara ambayo inategemewa kuongeza pato la Taifa. Sasa kuwaacha wafanyakazi na viwango vidogo vya elimu, wala hatuwezi

kufikia maslahi ya bahari kuu, wala hatuwezi kufikia maslahi ya mwani, hatuwezi kufikia maslahi ya mifugo na mambo mengine. (*Makofi*).

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kiwango cha wafanyakazi wetu wa Wizara hii, kwanza ni wafanyakazi wachache sana. Idadi ya wafanyakazi hawa ni Idara moja tu iliyokuwa chini ya Wizara. Ukiangalia Idara ya Ofisi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina wafanyakazi zaidi ya 500, lakini Wizara nzima ya Mifugo na Uvuvi ina zaidi wafanyakazi mia saba. Kwa hivyo, ni kuonesha kwamba hawa wafanyakazi wachache, hivyo ni lazima wasomeshwe kwa uchache wao. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninaishauri Wizara kwamba fungu la kusomesha wafanyakazi hasa kwenye masuala ya mazao ya uvuvi, mwani na mifugo, lazima vipewe kipaumbele, na Mhe. Waziri nikuombe sana kwamba watu hawa tuwasomeshe ili viwango vya elimu vya wafanyakazi wetu basi viridhishe kwa ajili ya kuleta faida kwa Wazanzibari. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo ninayotaka niiseme ni suala zima la tafsiri. Mhe. Mwenyekiti, hichi kitabu maelezo yote haya yaliyoandikwa ni tafsiri ya *data* za hesabu. Unaweza ukaandika hata vitabu kumi na mbili lakini tafsiri yake pengine ni hesabu moja ya tafsiri.

Sasa mimi ninaangalia maelezo yenu na tafsiri ya hesabu zilizoandikwa ni mbingu na ardhi. Maana yake zilizoandikwa ni tofauti sana na maelezo, yaliyoandikwa humu matamu, maelezo matamu sana. Kwa kweli mwandishi amepasi sana, mtungaji ana maelezo mazuri sana, lakini uhalisia wa hesabu haziendi hivyo. Nataka nithibitishe hayo mambo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uvuvi kama nilivyosema mwanzo ni Idara pekee ambayo tunategemea ingetoa mchango mkubwa kwa ajira na mchango mkubwa kwa pato la Taifa, lakini ukiangalia kitabu kikubwa hichi ambacho ndicho mwenye hesabu na ndiyo tafsiri ya haya maelezo muliyoyaandika.

Tuanze na *page* 591 Mhe. Mwenyekiti, "Programu ya Maendeleo ya Mifugo", kuna shughuli au *activity* ya kuimarisha jumuia za wafugaji. Wizara imetenga milioni tano. Nchi inataka iimarishwe kwa wafugaji lakini fedha iliyotengwa ni milioni tano. Eti hiyo ndiyo iwasomeshe wafugaji wa Unguja na Pemba mwakani tupate matunda ya ufugaji.

Kwa hivyo, siyo tafsiri pana kihesabu, ambayo kwa mimi naona kwamba ni tafsiri ya kufikia maendeleo. Hivyo ukisoma humu Waheshimiwa Wajumbe utafikiria kesho kila mtu atapata ng'ombe mia hapa, lakini tafsiri yake ni mahesabu yaliyotengwa. Je, mahesabu haya yatafikia malengo? Kwa hivyo wafugaji wetu

wametengewa milioni tano ziwasomeshe kwa ajili ya kufikia ufanisi wa maendeleo ya kilimo!s (*Makofi*).

Nyengine shughuli Nam. SO2, "Kudhibiti maradhi yanayoenezwa na kupe". Ng'ombe wetu wote, mifugo yetu yote imeathiriwa na kupe lakini Wizara imetenga milioni moja ndiyo iondoshe maradhi ya kupe. *Are we serious?* Kwamba eti ng'ombe wetu wa Zanzibar nzima waondoshwe kupe na tupate mifugo mizuri kwa milioni moja iliyotengwa. *(Makofi).*

Lakini shughuli nyengine ni kudhibiti magonjwa ya kuku na jamii ya ndege, kwamba kuku hawa wanaofugwa na ndege hawa wanaofugwa wadhibitiwe maradhi kwa milioni moja. Lakini kichaa cha mbwa, hili nimesikia wakitangaza wamedhibiti, mbwa wametafuna watu hapa Wilaya ya Kati mbwa saba, wao wametengewa milioni mia moja na arobaini na saba.

Ndiyo! mbwa ambao wanatafuna watu ni hatari sana, lakini ili kuwadhibiti mbwa hawa zimetengwa milioni mia moja arobaini na saba laki mbili thamanini na nne(147,284,000), lakini kuku wetu ambao ndio wafugaji wadogo wadogo wanategemea, imetengwa milioni moja kwa ajili kuondosha maradhi. Ni tafsiri mumeandika kwa mahesabu! (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi hanipi picha kwamba kwa kweli tutafika pahala. Sasa kama fedha ya wananchi itengwe milioni mia moja arobaini na saba kuondosha vichaa vya mbwa, lakini wafugaji wetu wa Unguja na Pemba wadogo wadogo kwa milioni moja ya kuondosha maradhi, ninawashauri Wawakilishi wenzangu hili fungu tusilikubali, na libadilishwe. Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya mimi jioni nitakuwa sipo lakini ninakuombeni fedha hii musiikubali. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kudhibiti maradhi ya minyoo ya hawa wanyama ni milioni moja imetengwa. Wanyama hao ni ng'ombe wetu, mbuzi hawa, kuku shilingi milioni moja inatosha kuondosha maradhi ya minyoo, lakini kichaa cha mbwa ni mia moja na arobaini na saba milioni.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine ambalo nataka nilitafsiri ni kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira zimetengwa pesa nyingi milioni tatu. Huku wafugaji wetu, watu wa Kojani na Micheweni mumewatia pingu kwa sababu ya nyavu feki. Lakini ili muimarishe uvuvi wa mazingira Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej mumemtilia milioni tatu nzima kwa ajili ya kuimarisha uvuvi wa kimazingira.

Waheshimiwa Wajumbe kweli tupo makini. Sasa ikiwa wewe umetenga milioni tatu Idara ya Uvuvi ili uimarishe uvuvi wa kimazingira, utamzuiaje mtu wa Kojani

Muwambe asivue kwa nyavu ya macho madogo. Maana yake wewe mwenyewe hujali.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, lakini niwakumbushe Mhe. Waziri kwamba bajeti hii Serikali mimi nikiwa Mwenyekiti, mulitwambia kwamba mutanunua boti kuanzia boti mbili kuelekea bahari kuu. Huku nimetafuta sana sijaona humu mote. Sasa ama bajeti ya Serikali tulidanganywa ama sijaona nioneshwe. Sijaona fedha ya kununua boti na Mhe. Omar munanunua maboti au vihori? Kwa hivyo, sijaona hayo maboti yale muliyotwambia maboti mawili ya kuelekea bahari kuu.

Kwa hivyo, mutwambie kwenye kitabu hichi cha Waziri na hili buku kubwa kama yale matumizi ya fedha ya kununulia boti mutuoneshe ipo wapi, bahati mbaya sijaiona.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kitabu cha Mhe. Waziri ametwambia kwamba mara hii wanategemea kukusanya mapato ya milioni mia tisa na hamsini na sita bahari kuu.

Ukiangalia haya mapato ni mengi sana, milioni mia tisa na hamsini na sita, lakini unatumia bilioni kumi na mbili na milioni mia nane. Waheshimiwa hiyo hesabu munaiona kwamba wewe utatumia bilioni kumi na mbili, milioni mia nane lakini utazalisha milioni mia tisa, ni asilimia ngapi, ni asilimia chini ya moja!

Maana yake wewe unaomba wananchi wakupe bilioni kumi na mbili, milioni mia nane ili ufanye kazi bahari kuu, lakini mwisho wa mwaka uwe unakusanya milioni mia tisa na hamsini na sita, ni asilimia chini ya moja. Mhe. Mwenyekiti, haikubaliki, anayekula sana lazima azalishe sana.

Umepewa bilioni kumi na mbili, milioni mia nane, maana yake angalau tupate bilioni tatu za faida. Lakini bilioni kumi na mbili tukupe kwa bahari kuu, lakini wewe mwisho wa mwaka utupatie milioni mia tisa.

Mhe. Mwenyekiti, ninawashauri wenzangu hili jambo waliangalie, kwa kweli haiendani sambamba na tafsiri ya mahesabu yaliyoandikwa. Na nini maana yake? Maana yake moja tu, kwamba hatujawekeza kwenye kupata faida, tumewekeza kwenye ama kufanya doria bahari kuu au kujinufaisha baadhi ya watendaji wa Ofisi za Bahari Kuu. Haiwezekani katika mahesabu kwamba utumie bilioni 13 wastani, lakini uzalishe chini ya bilioni moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi nashauri kwamba wenzangu jioni watakaokuwepo wakubaliane na Mhe. Waziri na hasa Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, basi tufuateni kule Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kule kidogo ilikatakata pesa ikapeleka maeneo muhimu.

Hapa nawashauri kidogo mkatekate mpeleke kwenye maeneo muhimu, ili wananchi wetu wapate ile *impact* inayotarajiwa wazi wazi.

Mhe. Mwenyekiti, msipokata fedha hizi mkapunguza kidogo, kwa kweli mtakuwa mnachangia nyinyi wafugaji wetu wasifuge kuku ili waongezeke, na badala yake maziwa ategemewe mfugaji mzee Bakharessa.

Mimi ushauri wangu nashauri kwamba hizi fedha zote apelekewe Bakhressa afanye hizi kazi. Nashauri hivyo mimi, kwamba hizi fedha zote zilizotengwa na idara hii ya mifugo hasa masuala ya maziwa na nyama, basi apelekewe mzee Bakhressa aongezewe nguvu, kwa sababu sisi tumeshindwa kuzalisha ndani ya Idara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya mambo yale ninayoona mimi kwamba hamna jipya, si dharau ya watendaji wa wizara na dharau kwamba uelekezaji wa fedha siko ulikopelekwa.

Huwezi ukawatangazia watu kwamba utafuga sana lakini kupe, maradhi ni milioni moja ndio wanafuga sana. Lakini wakifuga sana maana yake wakigonjwa sana maana yake milioni moja ndio ihudumie hiyo gharama, lakini mbu ambaye pengine maradhi yake huja kwa msimu milioni 150,047 haiwezekani Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti nashauri kwamba hii bajeti ipitishwe lakini kwa maelekezo ya kubadilisha vifungu, ili wafugaji wetu wadogo wadogo hasa wa kuku na ng'ombe wa maziwa waweze kupata tija inayotegemewa.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona humu Mhe. Waziri amesema kwamba ataongeza ufugaji wa samaki, na yapo mabwawa humu ambayo yametajwa mengi tu, lakini naomba nijue mabwawa hayo yako sehemu gani. Kwa sababu kule Kiwani kuna mabwawa yalichimbwa, lakini tangu siku yaliyochimbwa tangu Waziri Mhe. Said Ali Mbarouk, mpaka leo sijamuona tena mwengine. Kwa hivyo, mtwambie mabwawa haya yako wapi. Ni vizuri mtutajie mabwawa haya yako Mpendae, Magogoni, Kiwani ili tuyajue na tuyaone, sio mtuandikie tu mabwawa!

Mhe. Mwenyekiti, hii bajeti mpya ni bajeti ya programu kwamba Wawakilishi mwakani wafuatie kitu kwa kitu. Sasa ukitwambia leo mabwawa yako wapi bila ya kusema, kaka yangu Mhe. Mlinde Mabrouk Juma mwakani atakuwa hajui aende wapi, lakini mtwambie bwawa hili liko sehemu fulani ili mwakani wakaliangalie Kamati, lakini mkiandika hivi mabwawa 15 yamechimbwa yako wapi?

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kuwa niwashauri wenzangu kwamba jioni bajeti hii kidogo ifanyiwe marekebisho na hasa kamati, sio mfute fedha lakini muelekeze kule maeneo ambayo wananchi watapata maslahi.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Naomba niseme kwamba siungi mkono hii hotuba kwanza mpaka marekebisho ya vifungu vizingatiwe, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mwanzo kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wataalla* aliyeniwezesha kusimama hapa na kuweza kupumua kwa pumzi nilizoazimwa, hapa sijui ni muda gani zitahitajika.

Hii ni neema kubwa, ni wangapi sasa hivi wako *ICU*, wangapi wamezama, wangapi wamezikwa na wengine wanazaliwa. Hii ni neema kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu, hakuna utajiri kuliko afya, asikwambie mtu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa jitihada anazochukua katika wizara pamoja na wananchi wake. Hii wizara ni mpya kuwekwa peke yake, uzoefu huko nyuma unatuonesha kuwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kitu kama hicho, lakini imetengwa mbali kabisa, uvuvi na mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha kwa kweli kuna maelezo katika kitabu kikubwa kama ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Mwenyekiti wangu hapa alipozungumza kwamba bado kuna muelekeo mkubwa wa kusogezwa mbele. Nitakuwa sijafanya haki kwenye Kamati hii inayoongozwa na Mwenyekiti makini, Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, akisaidiwa na Makamu wake Mhe. Abdalla Mohammed Ali na Waheshimiwa Wajumbe, akiwemo Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Assaa Othman Hamad, Mhe. Kazija Khamis, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Mohammedraza Hassanali na rafiki yangu Mhe. Mussa Ali Hassan na makatibu wao wawili makini kabisa akiwemo ndugu Himid Choko na ndugu Salum Khamis Rashid, kwa kuisaidia kamati kwa uwezo mkubwa. Niwashukuru sana kwa kazi mliyoifanya Waheshimiwa.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nije na kilio changu cha muda mrefu tangu naingia humu ndani ya Baraza hili kuahidiwa ahadi za muda mrefu ahadi mbili.

Moja ni ya boti ya wananchi wa Jimbo la Muyuni, tuliahidiwa muda mrefu na sasa mimi ninakaribia kumaliza kibarua cha wananchi wa Jimbo la Muyuni, nitahitaji maelezo ya boti ile kama imeota mbawa au bado iko njiani inatengenezwa au itafika.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kulikuwa kuna hali ya banda la wavuvi la wananchi wa Muyuni. Nilileta maswali na nikaambiwa yanatafutiwa jawabu, lakini hakuna jawabu lililopatikana mpaka leo. Katika maeneo hayo mawili nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kilio cha wananchi wanyonge hasa sehemu za pwani, ikiwemo Jambiani, Muungoni, Kitogani, Muyuni, Paje, Bwejuu, Michamvi na kwengineko katika maeneo yote ya bahari.

Mhe. Rais aliagiza wizara nne zikae hapa, ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na hii ya Mifugo na Uvuvi, kuhusu kilio cha muda mrefu cha mwani.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wanateseka sana na wanahangaika katika hali ambayo hairidhishi hata kidogo. Maana yake hata huo mwani wenyewe kuna wakati unaharibika, haujulikani, mtu nguvu zake zinapotea kupita kiasi na bei ya soko lenyewe kilo shilingi 500 au 400 kazi ya kutwa nzima ambapo hairidhishi, na humu katika buku kuna pesa zilizotengwa huwezi kuamini, maana yake kuhusu mwani.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa uzalishaji, kuimarisha chakula. Kuna sehemu hapa imetengwa, sijui kama milioni 5 *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, muda wako unapotea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hauna neno Mheshimiwa, lakini hapa nitahitaji maelezo.

Kuna *point* hapa ule u- *serious* haupo, sijui milioni 5 au milioni 4 katika kitabu hiki. Kuimarisha kilimo cha mwani milioni 10, nimeiona Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Kuimarisha kilimo cha shughuli za mwani milioni 10,999,000 Unguja na Pemba. U- *serious* haupo, wananchi watazidi kuteseka, watazidi kupata shida, shughuli kama hii inatengewa milioni 10. Hapa wizara ifanye jitihada kubwa kweli kweli.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la uvuvi na mifugo. Bado ipo haja kubwa sana kwa serikali kupitia bajeti yake kuziimarisha sekta za uvuvi, kuangalia njia bora za kisasa na kuongeza kipato kwa mwananchi wa kawaida, ili kuongeza pato kwa wananchi na kwa nchi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali bado haijataka kuwasaidia wavuvi, hawajawapa nyenzo. Serikali ilipotaka kuwekeza katika eneo la karafuu tumeona wamepewa karabai na majamvi wanakopeshwa. Leo kwa nini wavuvi wasisaidiwe. Kamati ilisema

walipokaa viongozi wa kamati wakasema watafutiwe boti wasaidiwe japo sehemu mbili mbili. Ikawa leo karafuu ndio zimepewa kipaumbele, bado uvuvi serikali haijaupa kipaumbele. Wamekopeshwa watu majamvi, karabai, lakini zana za uvuvi ziko wapi?

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije suala la ufugaji nchini halijakamilika. Hii ni kwa sababu licha ya kuwa na uzalishaji wa maziwa kuongezeka kwa asilimia 8 ni asilimia ndogo. Nyama ya ng'ombe imeongezeka kwa asilimia 3.5 bado ni ndogo. Uzalishaji wa nyama ya mbuzi umeongezeka kwa asilimia 40.9.

Hili ni jambo la kupongezwa, ni hatua kubwa, panapo ukweli uzungumzwe ukweli, hii imeongezeka. Lakini mahitaji ya maziwa bado yanahitajika na nyama ya ng'ombe bado yanahitajika, u- *serious* bado haupo. Hebu serikali au wizara ichukue juhudi za makusudi kwa wananchi ili ijulikane wizara hii kweli imeteuliwa juzi, na kufanya mambo ya ajabu mapya makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kuhusu taaluma ya wafugaji. Hili ni jambo la msingi sana, ili kuzalisha maziwa yenye viwango na yaliyo bora yatakayoweza kuingia katika soko.

Pia ipo haja kwa wizara hii kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji, ambapo jambo hili la elimu halipo kwa wafugaji, wizara haijachukua hatua hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha, elimu kwa wafugaji bado haijatolewa au kwa baadhi ya sehemu tu imetolewa, lakini jimboni kwangu haijatolewa. Kwa hapa nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo jambo jengine la msingi ili tuzidi kuimarisha sekta hii ni suala la matibabu ya wanyama. Licha ya kuwa katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa fedha kwa ajili ya matibabu ya wanyama na kufanya uchunguzi juu ya mbali mbali ya wanyama, lakini bado ipo haja ya kuliboresha zaidi eneo hili kwa kunusuru wanyama na maradhi, jambo ambalo hupelekea vifo vya wanyama na kuathiri matumizi ya binadamu, na hatimaye kurudisha nyuma shughuli za wafugaji.

Hivi juzi tu niliuliza swali hili mimi katika chombo hiki. Angalau kungekuwa kuna utaratibu japo kwa wiki, wakawafuata wafugaji kama vituo hamna vya hospitali ya wanyama, angalau wakapitiwa wafugaji kwa kila wiki wakakaguliwa mifugo yao. Leo katika bajeti hii fupi katengewa shilingi milioni 1 kwa Unguja na Pemba, mfugaji ataneemeka wapi? Hakuna! Shilingi milioni moja Unguja na Pemba kuhusu kupe.

Mhe. Mwenyekiti, utafutwe usafiri angalau akafuatwa mfugaji. Leo mfugaji wa Muungoni, atoke Muungoni aje kumfuata daktari Fuoni, atoke pale aende Makunduchi na siku nyengine asimkute.

Bado Wizara ichukue jitihada maalum za makusudi kuhusu madaktari kuwapitia wafugaji. Wafugaji wanajituma.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nije kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia Zanzibar ni visiwa ambavyo vimezungukwa na bahari. Kwa hivyo, ni wazi kuwa sekta ya uvuvi ni moja ya sekta muhimu sana katika kuinua uchumi wa Zanzibar, kwa sababu rasilimali ya nchi yetu ya visiwa ni bahari.

Zipo nchi kadhaa ambazo zimeendelea kutegemea bahari kwa kupitia sekta hii. Hii ni neema kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, leo kweli kibua akatoke China aje kuuzwa Unguja, hebu tuangalie kama Mwanza wana Ziwa na wana Viwanda karibu vitatu vya samaki, leo neema hii tuliyonayo tunaipiga teke. Wizara ijipange itafute njia mbadala angalau mbadala wa kujenga viwanda vya samaki kuweza kusafirisha samaki.

Mhe. Mwenyekiti, kama Mwanza wana viwanda karibu vitatu sijui kama havijaongezeka, tena ni Ziwa tu. Leo sisi neema hii tunayoizungumza ya bahari tuliyozungukwa nayo hatuwezi kuitumia ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Mwenyekiti. Hapa wizara ikae, ifikirie na iangalie zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kumalizia, mwaka jana lilikuja suala la soko la Malindi kujengwa, ilikuwa Mji Mkongwe waliweka kizingiti walikuwa hawataki kujengwa, na tukaambiwa lile soko limeshakubaliwa kujengwa, hapa nitahitaji maelezo.

Soko lile limefikiaje la Malindi, ukitizama mazingira yale ya wauza samaki pale hayaridhishi, pamoja na kuwa samaki ni mtamu lakini hali ya Malindi ya kuuza samaki hairidhishi Mheshimiwa. Soko lile limefikiaje au mradi ule umefikiaje. Kwa hapa nitahitaji maelezo ya kina kabisa Mhe. Waziri, soko lile limefikiaje, au bado Mji Mkongwe wameendelea kupiga vita vitu vile mpaka leo?

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la majosho ya ng'ombe. Wizara ikae ifikirie kuhusu majosho na machinjio ya ng'ombe, mazingira yale ya machinjio ya ng'ombe kweli yanaridhisha kwa wananchi?

Mhe. Mwenyekiti, kuna maelezo mengine alizungumza Mhe. Hija Hassan humu kuhusu kuimarisha usarifu wa uongezaji wa thamani ya zao la mwani, suala hili nitakuwa mkaidi sana kuhusu kitengo hiki mpaka nipate elimu ya kutosha.

Kudhibiti maradhi yanayoletwa na kupe shilingi milioni moja. Haya mambo ya kudhibiti magonjwa ya kuku na jamii ya degedege shilingi milioni moja, kudhibiti maradhi ya minyoo shilingi milioni moja. Kuimarisha doria shirikishi katika maeneo ya bahari kuu shilingi milioni 42. Hivi ni vitu vya kusikitisha Mhe. Mwenyekiti.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nisipoteze muda mwingi, baada ya kupata maelezo ya Mhe. Waziri tutakayoafikiana basi nitaweza kupitisha kifungu hiki.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetujaalia uhai, lakini pia akatupa na uzima na akatuwezesha kuwepo kwetu humu, ili kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe kwa kunipatia na mimi fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika hotuba ya bajeti hii iliopo mezani wakati huu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kusema kwamba jana na juzi tulizungumzia jabeti ya Kilimo ambayo wanakwenda sambamba na bajeti hii ya Mifugo na Uvuvi. Kule tumepata chakula na huku tunapata kitoweo, tunajenga afya zetu na tunaimarisha ustawi wa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar imezungukwa na bahari, na uchumi wetu, tukiacha wizara tuliyoiacha jana ya Kilimo na Maliasili, ambapo wananchi wengi wanaajiriwa au wanajiajiri kwa kupitia sekta hiyo, lakini na Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, basi nayo pia hutoa ajira kwa wananchi wetu na kuweza kufanya shughuli zao za kimaendeleo, kujikimu kimaisha na shughuli nyengine pengine za kupata maendele yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli imezoeleka kwamba nikisimama, wengi huwa wanasema labda nina sababu za kusemea ukali. Haikuwa hivyo kama wanavyodhani. Lakini mara nyingi huwa nakumbuka ile dhamana ya uongozi, ambayo wanawake wenzangu wamenituma katika chombo chao hiki, na pale ninapoisoma bajeti au ninapopata nafasi na yanapozungumzwa mambo yanayowagusa wananchi, nalazimika mara nyengine kusema kwa uchungu mkubwa, ili kuonesha kilio cha wananchi juu ya tatizo hilo ambalo linawagusa.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na uchangiaji wangu katika bajeti iliyoko mezani kwa ukurasa wa 30 hadi 32 ambao unagusa Idara ya Mazao ya Baharini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hija Hassan wakati alipokuwa anachangia aligusagusa hayo mahesabu na kutazama michanganuo, na mimi nikawa nimetulia na hatimaye nilikaribia kusema kwamba nisichangie hapa leo, aliyoyasema yalikuwa yananitosha.

Mhe. Mwenyekiti, naongezea maneno yake kwa kusema yafuatayo. Ukiangalia ukurasa huo unakuta kwamba kuna uingiaji wa fedha hizo zilizoombwa katika hayo mazao ya baharini, kwa kipindi hicho ambacho kimemalizika.

SMZ yenyewe ilijipangia milioni 176,400,000 na wenzetu wa shirika wa maendeleo wakatoa shilingi milioni 384,680,000, lakini cha kusikitisha ambacho kinanipa uzito, ni kwamba SMZ kwenye milioni 176, 400,000 imetoa milioni 5, ambayo ni sawa na asilimia 3.

Nasita nasema sina cha kusema, kwa sababu ninaposema hayo huwa tunaona kama tumekuja kufanya masihara humu ndani. Milioni 176, unatoa milioni tano ambayo ni sawa na asilimia tatu tu (3%), unakusudia kusema je hivi kifanyike nini? Na mshirika wa maendeleo naye anatugaia milioni 36 kati ya zile 384 asilimia tisa, tisa na tatu asilimia 12%, bajeti hiyo tunahitaji kuboresha, kuzalisha mazao ya baharini kulinda, kufanya tafiti na mambo kadhaa kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa nisingependa niendelee huko, lakini nadhani kwa matamko haya ya asilimia tatu ya bajeti ya Serikali niiambie Serikali, jamani tulijibweteza mno katika kufuata fedha za wahisani, sasa hizi fedha jamani zinatukataa, sisi wenyewe tumejipangaje, nilitarajia Serikali iweko mbele kule, iwe inasikia tunayoyasema, maana tunaishauri Serikali yetu ili iweze kutekeleza, lakini huachiwa Waziri husika asikilize, peke yake Mwanasheria Mkuu unanisikia lichukue hilo.

Kama kweli tuna nia, na kama kweli tunahitaji hayo, asilimia tatu ndio bajeti iliyotolewa fedha tusitarajie kuleta mabadiliko ya uchumi wa Taifa na wananchi kuweza kutoka katika umasikini, tusitarajie hili, maana hata hiyo mipango haiendi.

Mimi niliwahi kusimama katika Baraza hili bajeti iliyokwisha nikamuambia Waziri wa Fedha hebu angalieni makusanyo yetu na fedha zetu uhalisia, ili tunapoandaa ile miradi yetu iweze kutekelezeka kwa ufanisi hata kama ni mmoja lakini uwe umetekelezeka kwa asilimia mia moja.

Nadhani mwaka huu tukaja na hiyo *PBB*, tuidhinishe fedha halafu haya matokeo tutakuja kuyaona mwakani, *inshaallah* Mungu akitujaalia, sijui hivyo, lakini kwa

utaratibu huu nasema kwamba tunafaa tujiulize, hivi kweli? Naiacha hapo Mhe. Mwenyekiti.

Sasa naomba niende katika ukulima wa mwani, Mhe. Mwenyekiti, wanawake wengi wa Zanzibar wameingia katika ukulima huu wa mwani, na shughuli hii hawafanyi wanaume, kwa kweli wanaofanya ni wanawake. Mimi nafikiri Serikali ndio maana wameshindwa hata kushughulikia hiyo bei yenyewe ya mwani, aah si wanawake!

Nadhani huku mkijua kwamba mwani una faida kubwa, na ni biashara nzuri, hili mnalifahamu. Wanawake wanatoka tangu asubuhi wanakwenda kushinda kwenye maji ya chumvi na mwani huo kuanikwa kwake ni kwa mtihani mkubwa, na shughuli yake ni ngumu lakini kwa kweli bei ya mwani haistahili, haiendani na ile tabu na dhiki wanayoipata wale wananchi.

Pia kwa mujibu wa shughuli za mwani nyinyi mmetwambia watu wa mifugo hapa mnasema kwamba mmefanya taratibu, na mmefanya *research* kuona kwamba mnachanganya katika vyakula vya kuku kwa hivyo mmeona faida yake.

Mimi nataka niwaambie kuna kikundi cha ushirika kinaitwa *ulezi una kazi;* wanatengeneza sabuni na mambo mengine unatumika mwani hata kwa kupika keki, kama hamjui hayo ninakwambieni.

Kwa hivyo una matumizi mengi na inawezekana sana kwamba Serikali bado hamjatoa kipaumbele kwa hili niwaombe hivi jamani kweli tutaongeza kipato kwa watu na kupunguza umasikini kwa utaratibu huu tunaokwena nao, nasema tena naomba sana kwa niaba ya wanawake, kwa sababu mwani halimi mwanamme serikali ilione hili.

Lakini jambo jengine ambalo nakusudia kulisema katika ukurasa huu huu ambao unaendelea hadi 32 ni uanikaji wa dagaa. Nataka niseme kwamba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ameleta utaratibu mbadala wa kuwaajiri au wa kujiajiri wananchi wetu kupitia uanikaji wa dagaa, kwa kuwa ni kisiwa tumezungukwa na bahari basi Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ameleta neema ya dagaa lile wananchi wetu wengi wamejiajiri kupitia sekta hii au taasisi hii ya uanikaji wa dagaa.

Nataka niiulize Serikali kwanza inayaelewa maeneo yote ambayo shughuli hizo yanafanyika? Mnipe jibu, na kama mnayajua mtwambie basi ni watu wangapi iliyowaajiri taasisi hii kama kweli Serikali mko makini katika kuangalia ajira za wananchi na kuwaongezea kipato na kuwapunguzia umasikini mtwambie, mmewaajiri wangapi na katika hizo sehemu zao wanazofanyia shughuli zao hizo

hizo shughuli zao watu wanapokutanika wakiwa pamoja kuna mambo ya msingi lazima yapatikane, yakiwemo maji safi na salama, pamoja na afya zao na vyoo mlikwenda mkaona vitu hivyo vinapatikana katika maeneo wanayofanyia shughuli zao.

Jengine ni kwamba shughuli hizi za uanikaji wa dagaa ambazo nazo pia wanawake wengi masikini wamejiajiri huko, Serikali kwa masikitiko makubwa kabisa nimeona kwamba sehemu zile za fukwe ambazo wananchi wanazitumia kwa kufanya shughuli hizo kwenye madiko yao tumekwenda sambamba na utalii, basi hata mita 30 mnashindwa kuwaachia.

Nayasema hayo Nyanjale tumekwenda kwenye uwekezaji wa Kiwanja cha Gofu lakini wananchi mita 30 tumeshindwa kuwaachia kufanya shughuli zao ambazo zaidi ya watu 500 walijiajiri pale. Hivi Serikali katika ajira hii ambayo wengi wao ni wanawake wajane, wanasomesha watoto wao, mmefikiria fikiria nini kuhusu eneo hilo la uanikaji wa dagaa la Nyanjale ambapo watu zaidi ya 500.

Hatukatai uwekezaji, tunajua Serikali yetu kwa wakati huu lazima iende sambamba na mambo hayo ili kukuza uchumi wa Taifa na pato la Taifa letu. Lakini Je, hawa wananchi raia wenye haki katika Taifa lao, mita 30 pia mnashindwa kuwaachia? Naomba mkija hapa mnieleze mna utaratibu gani juu ya Nyanjale na mita 30 Mhe. Waziri lazima unieleze hilo, kwani nawaona jinsi wanavyopata dhiki kwa wakati huu.

Mheshimiwa uniambie tena biashara hii ya uanikaji wa dagaa Serikali hamna lazima ya kutafuta soko, soko liko wenyewe kuna ndugu zetu wa Congo, biashara hii Serikali hamhitajiki wenyewe wanakuja wanainunua hivi mna nini mpaka hamuwaboreshi hawa watu? Nasema hili kwa sababu Serikali inataka kujenga hapa Maruhubi, hatukatai bandari huru sawa, lakini mnambie watu wa Maruhubi wapi mnawapeleka waanika madagaa wale, hili nalo pia nipate majibu yake, na niwaambie hivi mmewasajili hawa waanikaji wote wa madagaa walio katika sehemu zao. Hiyo naiacha hapo.

Sasa nije kwenye ukurasa wa 26 katika Idara ya Maendeleo ya Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti juzi nimesema kwamba azma ya Dkt. Shein ambayo alitoa katika hutuba yake mwanzoni mwa Baraza hili aligusa mambo haya akichanganua baina ya Wizara hiyo ya Kilimo na akaleta hii ya Uvuvi na Mifugo ili kusudi kuona kwamba anainua pato la wananchi wa Zanzibar, na akaweka hasa azma hiyo ya kusema tunahitaji uvuvi wa bahari kuu kuimarishwa.

Imekuwa ni nyimbo na imekuwa ni lele mama, maana mwenzangu Mhe. Hija Hassan Hija ameipambanua vyema, mimi niseme jamani penye nia huwa pana njia.

Mbona sisi bado tumefunga tu, maana nimeona hapakuwekwa kwamba labda kutanunuliwa boti ya uvuvi, meli ya uvuvi wa bahari kuu, nimeona tu kwamba kuna watu watasomeshwa, kwa hivyo kumeandaliwa utaratibu wa kusomeshwa wavuvi masuala ya uvuvi wa bahari kuu, niambiwe ni idadi gani ya wavuvi hawa ambao wanahitaji kusomeshwa uvuvi wa bahari kuu? Nipewe idadi yake. Na watapatikana kwa utaratibu upi, nalo hilo niweze kupewa.

Mhe. Mwenyekiti, halafu jengine ni lile la ujenzi wa soko la Malindi katika mradi huu na uimarishaji wa uvuvi wa bahari kuu hapa kuna bilioni nane, naomba nichanganuliwe hizi zinakwenda wapi kw,a sababu zimechanganywa kwa miradi miwili, naomba mchanganuo wake niweze kupatiwa ili tuweze kuona hiyo hali inakwendaje.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye sekta ya mifugo. Wamesema wenyewe kwenye kitabu chao hichi katika ukurasa wa tano kuna changamoto za mifugo; uhaba wa wataalamu na nyenzo, hivi kama kweli tuna nia niungane na Mhe. Hija hii *point* ilikuwa nimeiweka, kwamba hivi kwa nini tusiongeze wafanyakazi wenye kiwango na sifa, lakini pia tuwasomeshe wale tulionao tutafikia je, malengo? Maradhi yanatawala katika mifugo; kuna vikundi mbali mbali vya ushirika vilivyopatiwa ufugaji wa ng'ombe wa kisasa, vimepatiwa ufugaji wa kuku wa kisasa mbuzi waliobakia wa kukunia nazi lakini wale walioletwa hasa wamekufa wote ndio ukweli, hivi jamani tunapokusudia kufanya tunafanya *research* ya hao wanyama tunaokwenda kuwachukua, tunafanya na tunajua kwamba kule tunakowachukua na joto na hali ya hewa yetu ya visiwani wanakubali, *research* hiyo imefanywa tukaona. Kwa sababu mingi ya mifugo ambayo imechukuliwa kuletwa kwetu sisi kuja kujiendeleza vikundi hivyo jamani wamekufa, hasa imebakia maneno ya kwenye vitabu lakini uhalisia haupo huo ndio ukweli.

Niombe basi kwamba fanyeni *reserch* kwanza kama hao ng'ombe mnaochukua Bara huko kwa wenzetu Tanganyika au kwengineko hali yetu sisi mazingira yetu ni visiwa na tunaishi katika mzunguko wa bahari je, wanahimili. Kama hawahimili mbinu mbadala ipo, ng'ombe wana maradhi, kuku wagonjwa lakini samaki jamani hatujawahi kusikia samaki na maradhi, hatujawahi kusikia hicho kitu basi tuimarike huko sisi tumezungukwa na bahari tuimarisheni huko zaidi.

Leo sisi tukitaja bahari kuu tumeshasema, na soko nimeona humu kwamba litajengwa lakini nauliza kama kweli tumekwenda huko na tumefanikiwa baada ya hilo soko kama soko pindi wavuvi wamefanikiwa na wamewapata, tuna utaratibu gani na namna ya kujenga viwanda vya kusindika misosi na sisi tukasafirisha, kwa nini mpaka leo jamani tuna mapeduu na samaki nao sasa hivi wameshaletwa peduu, ni aibu Wazanzibari kuletewa tumezungukwa kisiwa chetu na bahari

tukinunua samaki kutoka katika taifa jengine wamehifadhiwa ndani ya majokofu, hili linawezekana na nasema linawezekana kabisa.

Jamani hii nia tunayo ya kuyatenda hayo au tunasema tu kwa maneno, kwa sababu ukituangalia tumezungukwa na bahari, lakini sisi tunakula samaki leo samaki hasa peduu wa kuku, tuna nini tusioimarisha uzalishaji wa ndani ili wananchi wetu wakaweza kujikweza kipato.

Leo masoko yote peduu ndio utaratibu mzima, na ndio chakula nacho hatuna hakika hasa kwenye viwango, jamani hawa kweli wako salama kiasi hicho au wako salama kula tu mwanadamu hilo pia halionekani.

Niiombe Serikali, kwa haya madogo mimi nadhani yanawezekana. Jamani kuna mambo yanawezekana lakini mimi nasema na usimamizi nao tuna matatizo, tuna matatizo ya usimamizi, tuna matatizo ya kuchanganya madawa; ukiamua mpango wako huu ambao wataalamu au wale watu wa mipango sisi tuna tabia ya kuingia kati, Zanzibar ndio tabia zetu hapa lifanyike hili na hapa hili, wakati tayari wataalamu wameshaweka *indicators* zao za kuonesha tunaweza kufikia kwa kufanya moja mbili tatu, hii tabia tunayo.

Mhe. Mweyekiti, nikitoka hapo nataka nije nielezwe kidogo kwenye ukurasa huu wa 38 huu unasema kwamba kuna mradi hapa wanasema wataimarisha ajira kwa vijana; ambapo programu hii ipo kule kwa wanawake na watoto ambao wanasema ufugaji wa mbuzi, tena mbuzi wenyewe wale wa kienyeji ajira 120.

Mheshimiwa hii ndio ile niliyoisema hadithi za alinacha, ikiwa mbuzi anae mwenyewe mbuzi wa kienyeji Serikali mnawatoa wapi, nasema hivi ukisikia wafugaji waliojiweza na kujiendeleza nataka nikwambieni ni watu wa juu wenye uwezo ndio wenye kumiliki kufuga lakini wanyonge kwa kweli hawafugi, hawana taaluma.

Ndugu yangu Mhe. Mshimba jana alisifia sana kwamba yeye ni mfugaji kweli, maana akimtaka mtaalamu saa ile ile anakwenda kumchukua anampigia simu anakuja na anamshughulikia lakini wale wa chini wamefikiwa kwa kiasi gani? Niwape ushauri wa bure huo hauhitaji fedha lakini niuseme Serikalini.

Katika eneo langu la Nyanjale kuna mto umepenya kuna sehemu nzuri sana kabisa ambao kama wataalamu mtakwenda kuiona na kuifanyia utaratibu pale upo uwezekano mkubwa wa kufugwa samaki wengi kabisa na hali ikawa nzuri na tukaongeza kipato kwa wale wananchi wetu waliopo pale.

Serikali hamjafanya *research* ni maeneo gani hasa yanaweza yakafugwa hao samaki wenyewe, nyinyi mnasema tu tufuge, mabwawa yachimbwe, mmewahi kufanya *research* ni sehemu zipi na zipi hasa zinawezekana kwa urahisi zaidi na kuweza kuzalisha au kujenga hayo mabwawa.

Jengine nimeona kwamba programu yenu katika kitabu hichi inasema kwamba mnahitaji kuendeleza hiyo mifugo yenu sijui wangapi hao, mmewataja humu lakini kinachokuwa kinanipa mashaka kwamba yale madawa au chanjo zenyewe wanazohitaji wafugaji wenyewe basi inafika pahala anaambiwa hiyo dawa haipatikani, tunayo hayo!

Wale wataalamu wenu hawapatikani, inaweza wanyama wako wakaanza kupata maradhi basi unaweza kufika muda mrefu sana kabisa kwamba hujampata hata huyo mtaalamu, na ukimkuta anakwambia dawa sina ngoja nikazitafute, muda wa kupata tunapoteza inakuja homa, pengine kuku wanakufa wote, pengine ng'ombe wananyong'onyea miguu hali masikini wanyonge wanaendelea kurudi katika hali ile.

Mhe. Waziri nikuombe uniambie mbuzi hawa utawanunua? Mnataka kuwanunua hawa wa kienyeji mnapoimarisha, au mnataka kuwapa mitaji wanunue wenyewe, maana yake sioni kwamba hii mmetoa ajira kama ilivyosema hizi pesa mnazipeleka kwenye utaratibu huu kwa kununua hao wanyama kuwapelekea, ama mtawapa fedha ama mtawawezesha kwa kuwapa taaluma, sijui lakini mmesema hapa mna programu hii ya ajira kwa vijana.

Kwa hivyo inasimamiwa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa jamii, Vijana wanawake na Watoto, naomba basi unipatie kuhusu mradi kwamba mtatoa fedha, mtatoa taaluma mtafanya kitu gani hasa kwenye milioni mia moja hii ambayo mumeiweka hapa na mmekusudia kutoka kwa vikundi vingapi? Hao watu 120 mtawapata kwa kupitia utaratibu upi?

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo niulize huu ufugaji wa samaki wa maji baridi, hapa kwetu

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika nne za kumalizia.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Zinatosha kabisa Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Lakini niulize hivi jamani tunataka sisi samaki wa maji baridi hapa kwetu? Maana yake naona tumezungukwa na bahari, na humo baharini hatuwezi kuwavua hao tuliona.

Sasa tunasema tujenge bwawa tuvue samaki wa maji baridi huku juu, hivyo mimi kidogo napata wasi wasi. Maana yake naona tumezungukwa na bahari lakini tunasema samaki wa maji baridi.

Halafu la mwisho kabisa mtwambie katika utaratibu huu wa upatikanaji wa soko kwa ajili ya wale wafugaji wetu. Hebu twambieni kwenye sehemu za utalii hawa wananchi wetu wanapata soko vipi, kupitia samaki pamoja na hiyo mifugo yao mtwambie.

Mtwambie na kwamba mahitaji ya sasa hivi yanakidhi haja, na nyinyi pia mnakusudia katika mpango wenu mliosema mlianza ule mradi wenu wa 2011/12 hadi 17/18, hivi mnafikiria tunaweza tukafikia hayo malengo kwa mlipo sasa hivi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba nikae kitako nisubiri hayo na hatimaye kuweza kujua utaratibu unavyoendelea, ahsante nakushukuru.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii nikaweza kutoa mchango wangu mdogo katika hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo tunaijadili kwa maslahi ya Wazanzibari kwa ujumla na Taifa pia.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia nikaweza kuamka salama, lakini pamoja na wenzangu na tukaweza kufika katika jengo hili kutimiza majukumu yetu tuliyopewa na wenzetu ambao hawana uwezo wao wa kufika hapa, na hatuwezi tukafika hapa sote, bila ya shaka kutakuwa kuna watu wanaowakilisha na ndio sisi na tupo katika kuwawakilisha, kuona kuwa zile shughuli zao wanazofanya basi zinafanikiwa kwa kiasi fulani katika kujiondolea umasikini mdogo mdogo wa kipato.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru sana Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa ujumla katika kufanya shughuli zao.
Tunajua kwamba serikali yetu watendaji wao wanafanya kazi kwa uzalendo mkubwa, ambao wao wana imani ya kuwa wananchi wetu wafanikiwe kwa kiasi fulani.

Pia nataka nichukue fursa Mhe. Mwenyekiti, katika picha hii iliyopo hapa mbele ambayo inamuonesha Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein, akipata maelezo katika ufunguzi wa Soko la Samaki la Tumbe. Nichukue fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka bajeti ya mwaka jana tulikuwa tuna mawazo ya kumaliza lile Soko kwa ufanisi mkubwa ili lile lengo lilokusudiwa basi lifikiwe.

Kwa hiyo baada ya kumaliza bajeti nadhani yale ambayo tulieleza hapa walilokuwa wametutuma wenzetu, basi nashukuru na namshukuru Waziri wa Fedha aliweza kufika katika eneo lile na zile changamoto ambazo zilikuwepo ndogo ndogo zikaweza kufanikiwa, na hatimaye soko hili limefunguliwa liko katika hali nzuri. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuweze kudumisha kile tulichokuwa tumekusudia.

Lakini kwa kupitia soko lile nataka niiombe serikali kwanza wafanye matembezi katika soko lile, waone ile hali halisi ilivyo pale. Kile kilichokusudiwa ndicho kinachofanywa. Lakini kama kuna matatizo madogo madogo basi wasichoke, wawe mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa lile soko linatumika vile ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hilo ni suala ambalo nimesema niliseme, kwa sababu mimi ni mkaazi wa Tumbe na tulikuwa tukisimamia kwa ukaribu sana na wenzetu ili kuona pale tumefanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye hii sekta ya mifugo, lakini kwanza nataka nianze kwenye hii hotuba ambayo Mhe. Rais katika uzinduzi wake wa Baraza alipokuja kutuzindulia hili Baraza kwa mara ya kwanza nikiwa na mimi ni Mjumbe niliyekuwemo, alieleza madhumuni yake katika kuhakikisha kuwa sekta mbali mbali zinakuwa zinapewa kipaumbele katika kufanikisha majukumu yake wanayopewa na wananchi.

Tulianza tukaambiwa kuwa kutakuwa na Mapinduzi ya Kilimo. Tumeona hali halisi lakini kumbe pia na kwenye ufugaji pia Mhe. Rais alitwambia kuwa kutakuwa na Mapinduzi ya Ufugaji.

Sasa kwa sababu tupo kwenye kikao chetu cha mwisho, ambacho tumeshafanya kazi miaka mitano, na hii ilikuwa ndiyo muelekeo wa taasisi mbali mbali katika kitabu hichi, tulitegemea kuwa tutafanikiwa kwa asilimia angalau japo sio kwa asilimia 100 lakini japo asilimia 70, tulitegemea tufanikiwe katika masuala haya.

Kwenye kitabu hichi Mhe. Rais alisema kuwa naomba ninukuu;

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba itaimarisha ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi na kuku, ili kuongeza tija na kipato cha wafugaji"

Hichi ni kipande kidogo tu ambacho Mhe. Rais, kwenye kitabu chake kipo. Sasa tulitegemea pia katika kuendeleza azma hiyo, basi miongoni mwa hivi vitabu vya bajeti pia navyo tuone yale mafanikio ambayo yalifikiwa. Lakini hatimaye kwenda

na kurudi zilizomo ndani ya vitabu hivi vya bajeti nyingi ni changamoto ambazo Wizara inashindwa kukabiliana nazo katika masuala haya.

Mimi nafikiri Mhe. Rais, alikuwa na nia nzuri tu katika kusema haya. Ninavyotegemea kuwa Wizara hii pamoja na Wizara ya Kilimo ilikuwa ipo mbali mbali lakini zikachanganuliwa Wizara hizi kwa ajili ya kuleta ufanisi. Lakini ufanisi kwa kusema kweli tunakwenda ile ile katika hali ya mazoea tu. Tunachokipata tugawane kidogo kidogo lakini ile azma hasa hatujaifikia.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tuna rasilimali zetu tulizonazo ni ardhi yetu tuliyonayo japokuwa ni chache, lakini inahitajika itumike vizuri kwa shughuli pengine za kilimo na makaazi. Lakini pia tumezungukwa na bahari yetu ambayo nayo ni moja ya nyenzo za kukuza uchumi.

Tunayo bahari kuu ambayo siku zote inazungumzwa na kutegemea kuletewa meli za uvuvi hapa. Lakini mpaka leo hata ile boti hatujasikia kuja, achilia mbali meli, na wala sio kwa sababu uwezo huo hatuna, bali hatujawa tayari tu na hili. Tunakuwa ni wasemaji wazuri lakini utekelezaji unatupiga chenga.

Mhe. Mwenyekiti, nilimsikia Mwenyekiti wa Kamati hapa anazungumza kwa mbali kidogo anasema kuwa suala la meli hizi pesa tayari zimekwishakwenda kuwekwa kwenye Wizara ya Uwezeshaji. Kwa hiyo kama ipo hiyo basi tuombe Mungu ili tuweze kutumia rasilimali yetu hii tuliyonayo ya bahari.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwenye hii sekta ya mifugo. Mafanikio katika sekta ya mifugo nashukuru sana Zanzibar kuwa uzalishaji wa nyama inaoneshea Zanzibar tunao walaji wa nyama sana. Ukiangalia kwenye mafanikio yao hapa ni kuongezeka kwa uzalishaji wa nyama. 2014 nyama ya ng'ombe imeongezeka kwa asilimia 3.4%, lakini nyama za mbuzi zimeongezeka asilimia 4.9%. Kwa hivyo kwa uzalishaji wa nyama basi nitoe pongezi kwa hili. Sasa nadhani badala ya nyama na maziwa pia tunapata kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye hii changamoto ya Sekta ya Mifugo moja aliyosema ni fursa ndogo ya wafugaji katika kuwapatia mitaji. Sasa hili kwa sababu tuna Wizara ambayo inawawezesha wananchi wake, kuna hii Wizara ya Uwezeshaji, Kiuchumi ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri aje anieleze je, wameshawahi kukaa pamoja na hii Wizara kuhakikisha kuwa wafugaji wanapatiwa hii mitaji na wao ya kukopa ili wakaweza kuendeleza hii mifugo yao. Kama ni moja ya changamoto ambayo inaikabili Idara hii ya Sekta ya Mifugo.

Fursa naona zipo, siku zote mawaziri wanatwambia hapa wakopeshwaji tunaona ni wengi. Mikopo ya AK na JK ipo, sasa kwa nini wasiweze kupatiwa na wao wafugaji hii mitaji katika kuendeleza shughuli zao hizi za ufugaji ili kupata tija zaidi. Lakini kuna muelekeo huu wa baadaye, moja katika muelekeo huu kasema kuwa kuna kuboresha uzalishaji wa mifugo ya kienyeji kwa kubadilisha vinasaba.

Sisi Wazanzibari tulikuwa tuna mifugo ya asili ambayo tulikuwa tunafuga kama ng'ombe, kuku lakini tukaingiliwa na utaalamu sasa wa kutafuta mambo mengine ya kuwa tuwe na kuku wa kisasa, tuwe na mambo ya kisasa.

Sasa hapa katika hii kuboresha uzalishaji wa mifugo ya kienyeji, sasa tunataka turudi kule tulikokuwa ambapo tulikuwepo huko lakini tukatoka tukaingia kutafuta makuku wengine wa kufuga, sasa tunataka turudi tena huku kwenye kuku wa kienyeji au kwenye mifugo ya kienyeji?

Sasa kama hivyo ndivyo ni sababu zipi za msingi zilizopelekea huku tulikokuwa tusiweze kukuendeleza, tukatafuta mambo mengine na sasa hivi tuko ndani ya kutaka tutoke huko pengine katika kutafuta kupandisha hivyo vinasaba.

Sijui utatuelezaje Mhe. Waziri, tueleze hasa tatizo ni nini ambapo kuwa tusiimarishe ile mifugo ya kisasa tuliyokuwa nayo ambayo kuwa kuna ng'ombe wa maziwa, kuna mbuzi wa maziwa, kuna kuku wa siku mbili tatu, sasa tunataka tuache huku, tuelekee huku ni kwa sababu gani?

Lakini suala la mafanikio katika sekta ya uvuvi kaeleza Mhe. Waziri kuwa kuna jumla ya vikundi 144 vya wafugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini, zimeanzishwa Unguja na Pemba. Na mimi naomba hili kwanza niungane na Mhe. Hija Hassan Hija, tunataka tuvijue hivyo vikundi vilivyoanzishwa katika haya maeneo ili na sisi tuweze kufuatilia kwa karibu kuona uzalishaji wao unakuwaje.

Mhe. Mwenyekiti, najua hili kuwa lipo linafanywa na serikali tunashukuru kuwa vikundi vipo; cha ufugaji wa samaki au ufugaji huu wa mazao ya baharini vikundi vipo vikiwemo mwani, ufugaji wa samaki. Serikali kupitia wananchi wao na kutoa michango mbali mbali ya vikundi hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi vikundi saa nyengine vinataka vipitiwe na kuangaliwa hasa katika mpango mzima ambapo kuwa pengine tunatoka kwenye msimu mmoja kuingia kwenye msimu mwengine. Kuna msimu huu masika ambao kuwa umeathiri wafugaji hawa wa mazao ya baharini wakiwemo wale wafugaji wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti, pale Sizini pana kikundi wanafuga samaki hawa, lakini sio wa maji pepo, wanafuga samaki kwenye maeneo ya bahari lakini kwenye mabwawa. Sasa hawa katika kipindi hichi cha masika waliathirika kwa kiasi fulani na matatizo haya ya mvua hizi za Masika, wakafikia pahali samaki wao waliokuwemo kwenye mabwawa wakalewa na hatimaye mabwawa yale yakaingiwa na maji mengine. Sasa imekuwa ni hasara. Lakini hawajavunjika moyo, bado wanaendelea na shughuli zao, kwa sababu wenyewe wanaona wana tija ndio maana wakaendelea. Kwa sababu kikundi hichi sio cha leo, nakumbuka tangu Waziri Said Ali Mbarouk alivyopewa Wizara hii. Tulikwenda katika kikundi kile na tukaona, japokuwa ilikuwa mwendo wao ni huu wa kusuasua, lakini nadhani kama mpaka leo wanacho kikundi kile basi wana nia nzuri ili kuendeleza kile kikundi chao.

Nakuomba Mhe. Waziri katika hili basi Idara yako iweze kufuatilia kwa karibu ili muwasaidie mawazo na maarifa wasije wakavunjika moyo ndizo ajira zinazotafutwa hizo. Sasa kama wanapata hasara fulani basi angalau mkienda kuwapa ule mchango wa mawazo wataridhika nao, ili wasije wakavunjika moyo katika shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, hii changamoto ya sekta ya uvuvi ambayo kuwa ni uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi za doria umepelekea kuzidi uvuvi haramu.

Hili nalo hatujawa tayari kwa sababu tuna vikosi vyetu, tuna KMKM hawa kwa nini hawawezeshwi na ndio wanaofanya kazi hizi za kulinda doria. Kwa nini iweze kuwezekana katika kulinda magendo ya mafuta lakini isiweze kulindika kwenye uvuvi huu wa haramu.

Hili bado Wizara mjipange kwa sababu serikali ni hii hii moja. Kwa hiyo mtu wa huku atoke ashirikiane na wizara hii kushirikiana kwa ajili ya kuhakikisha hili halifanyiki, magendo ya karafuu yamedhibitiwa, magendo ya mafuta yamedhibitiwa, iwezekanaje kutodhibitiwa kwa uvuvi haramu? Bado ni kujipanga, bado hamjajipanga na hamjashirikiana kwa kusema kweli serikali kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine hapa kuna utekelezaji wa malengo vile vile utafiti wa ufugaji wa mbuzi katika kijiji cha Kiuyu Mbuyuni unaendelea, tafiti hizi zitawasaidia wafugaji kujua jinsi ya kulisha na kunenepesha mifugo yao kwa gharama nafuu.

Mhe. Mwenyekiti, nishukuru sana hili suala, kwa sababu wale wala hawataki kufanyiwa utafiti watu wa Kiuyu na Maziwang'ombe na Micheweni. Hawataki kufanyiwa utafiti wa ugawaji wa mambo kama haya ya mbuzi. Kwa sababu wao ndio kazi zao tangu asili zao kule ni ufugaji wa mbuzi na ng'ombe, lakini hawa ng'ombe ni kidogo kuliko ufugaji wa mbuzi. Sasa hawa ni kuwapa taaluma tu

ndogo sana au kama kuna hao mbuzi mnaosema wa maziwa sijui wanaotoa lita ngapi. Basi na wao ni kuanzisha vikundi tu kule, ili mkaweza kuwaona namna gani wanaweza kushughulikia, kwa sababu hawa naona ni wataalamu wa ufugaji wa mbuzi. Lakini bado serikali kupitia haya mambo yanayoibuka ibuka wanawasahau na wako nyuma. Kwa hiyo nashukuru kuona hili na nadhani kuwa mtakapofanya hivi basi na wao wataendelea na kazi yao wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nije kwenye Idara ya Mazao ya baharini kuhusu suala zima la mwani. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza serikali kuona kuwa wakulima wa mwani lengo lao ni kutaka na wao wapate bei nzuri lakini wapate tija kwa kiasi fulani.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwani ni suala gumu ambalo wanawake wengi wanajiajiri katika sekta hii ya upandaji wa mwani, wengi sana, lakini niliposoma hili gazeti asubuhi niliona kama kuna vifaa ambavyo vilitolewa hivyo vihori kwa ajili ya kupewa wakulima wa mwani na kufanya shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka Mhe. Waziri akija anambie katika kugawa hivi walizingatia nini? Kwa sababu katika Wilaya inayopanda mwani au inayozalisha mwani kwa wingi basi Wilaya ya Micheweni au Mkoa wa Kaskazini kupitia Wilaya ya Micheweni, ndio wanaozalisha mwani kwa wingi sana. Lakini katika kugawa vifaa hivi hapa bado sijaona, lakini japo huko nyuma pengine walikuwa na wao washapata basi kama ni hivyo itakuwa sina la kusema.

Kuna suala zima la kuusarifu huu mwani kuuanika na kuuza vile vile ulivyo na kuusarifu katika kufanya biashara mbali mbali. Hili suala Mhe. Mwenyekiti, ni zuri sana, kwa sababu mwani hauna bei lakini sasa kumbe unaweza kusarifiwa katika mambo mengine.

Sasa hili ninaiomba Serikali kuwa hili basi waweze kuanzisha vikundi mbali mbali na kuwapa hizi taaluma ili waweze kuondokana na ile kuuza mwani kwa shilingi mia tano, lakini kumbe watakapousarifu vyengine watakuwa wana kipato zaidi ambacho kitawasaidia. Kama hivyo ndivyo Mheshimiwa hapa tumeona katika hili gazeti kuna vileja vya mwani, humu ndani ya vipakti sijui kuna vidubwasha gani lakini keki pia ziko za mwani.

Kwa hivyo tuwape mafunzo, na ninashukuru kuna mradi mmoja ulikuja hapa wao wakulima wa mwani maeneo ya Kinoe pale walipewa mashine lakini naona bado ujuzi hawajawa nao, walipewa mashine ya kusagia mwani na ule unga wa mwani kilo moja, karibu shilingi ishirini elfu, sasa hiyo ni ajira iliyoje hiyo, ikiwa tutawawezesha basi watu watapungua ule utegemezi wa kutegemea waume na kutegemea Serikali kwa ujumla.

Suala jengine hili lilikuwa lishazungumzwa, kwa kweli Serikali bado haijawa makini na azma yake nzuri iliyonayo lakini wajitahidi katika sekta hii ya uvuvi ambayo wawaingizie pesa basi ambazo zinalingana na kazi zao. Kwa sababu unapoziwezesha wizara hizi; Wizara ya Kilimo, lakini Wizara hii ya Uvuvi ni Wizara ambazo zinawaajiri wazanzibari wengi walio na kipato cha chini, watu wajiajiri kupitia humu, aliyekuwa si mkulima ni mvuvi, aliyekuwa si mvuvi ni mfugaji lakini ndizo sekta za kuzipa kipaumbele, lakini ukisema tunazipa kipaumbele au ukiona kama hivi yanayozungumzwa pengine mtu kaomba pesa chungu nzima anakwenda kupata asilimia 26 ni tatizo kweli kweli. Kwa sababu hao tunaowabebesha mzigo tunawabebesha majukumu, tunawapa lawama kumbe na wao maskini hawana uwezo, kila kitu kinataka kufuatiliwa.

Sasa ina maana kama hawana pesa watabaki kukaa mawizarani kwao, basi kazi inaendelea lakini wale walengwa watakuwa hawafikiwi, hatufikii lile lengo.

Kwa hivyo naiomba Serikali kwa ujumla ione sekta ambazo zinazalisha ajira kwa wananchi wake wazipe kipaumbele, wao hawana uwezo wa kujenga kiwanda Serikali hiyo, wao hawana wawekezaji ni matatizo, hivi sasa tunatafuta wawekezaji wa kuwekeza kwenye hiyo Bandari Kuu. Lakini ukitizama kumbe Zanzibar ina wavuvi wazuri wako huko mitaani, ukienda Kojani, ukienda huko Tumbe ambao wana uwezo wa kufika kwenda kuvua kule lakini wanataka kwenda kwa nini, watakwenda na vidau.

Sasa tunategemea ile bahari yetu kwa kutegemea kodi za wazungu wanaopita huko wanakuja kuchukua mali wakaenda zao sisi tunatafuta muwekezaji hivi sasa. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa suala la kutafuta muwekezaji Zanzibar litaendelea wawekezaji wengi watapokuja hapa ni ujenzi wa mahoteli basi.

Hivi sasa Zanzibar kuna mahoteli karibuni nyota zinafika ngapi sijui za mahoteli, lakini sasa mambo mengine yapo maeneo huru hapo siku zote tunayapigia kelele. Kuna Fumba, kuna Micheweni tokea mwaka yaliyowekwa kuwa maeneo huru ni muwekezaji gani anayekuja hayupo, kwa sababu hatujipangi, anataka kwenda tu muwekezaji hakuna miundombinu yoyote.

Sasa na hii bahari kuu tunayo wavuvi wetu Zanzibar wa asili; wa jadi, wanaweza kuvua wapeni vyombo waende kwenye bahari kuu wakavue mafao yaingie huku, lakini hatutotegemea kuwa wapite wazungu wakaenda wakavua hatimaye tupate hizi fedha kwa kweli zinapatikana?

Kuna tofauti kati ya kodi mnazozikusanya wavuvi wa nje na wavuvi wa ndani, inaonesha kwamba wavuvi wanaovua nje ni kiwango kikubwa cha pesa kinachopatikana. Lakini ninaiomba Serikali iwawezeshe wavuvi wetu wana

taaluma nzuri, wana uwezo mzuri wa kuvua, wamezaliwa ndani ya bahari. Lengo na madhumuni ya kupatiwa nyenzo na vifaa basi wanaweza kwenda kufanya kazi katika bandari hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi sina matatizo na wizara hii naunga mkono kwa asilimia mia, lakini naomba yale tunayoyazungumza basi yazingatiwe kiasi fulani. *(Makofi).*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii nikachangia bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na pumzi na nikaweza kufika katika Baraza lako hili Tukufu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri kwa uwasilishaji wake pamoja na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti niende moja kwa moja kwenye sekta hii ya Mifugo na Uvuvi. Kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri kwanza nimpongeze, kunaonesha kwamba kumeongezeka idadi ya wafugaji wa ng'ombe, mbuzi na kuku wa kisasa kutoka 46,000 mwaka 2013 hadi 47,058 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 2.3%.

Nishukuru kwa hilo lakini kama walivyokwisha kusema wenzangu kwamba mafanikio haya, lakini vile vile kuna changamoto na changamoto vile vile nazo zitizamwe na changamoto ni kubwa sana. Kwenye changamoto nimeona kwamba kuna upungufu wa wataalamu na nyenzo za kufanyia kazi kwa baadhi ya vitengo kama utafiti, ugani, pamoja na utabibu wa mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli juu ya ongezeko hili kukawa na changamoto kama hizi kwa kweli inatia hofu katika nafsi, kwa sababu hizi changamoto juu ya kuwa kuna ongezeko lakini uhaba wa malisho upo katika changamoto hizo, pia fursa ndogo za ufugaji, wafugaji kupata mitaji, kwa kweli Serikali ichukue juhudi za makusudi kuwawezesha hawa wafugaji. Kwa sababu tunajua kwamba hii ni sekta ambayo inachangia pato la Taifa, na vile vile tukitizama wananchi wetu wengi hawana ajira, ajira ndio hizi. Kwa hivyo ni lazima kuwe na mikakati ya makusudi ili kuwawezesha hawa wafugaji.

Vile vile katika hizo changamoto kuna uwekezaji mdogo katika viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa bidhaa za mifugo. Ni kweli kama Serikali inataka mafanikio ya mambo haya kwenye sekta hizi, basi ni lazima zitafutwe mbinu mbadala ili iweze kusarifu haya mazao. Na kwa sababu kuna *PPP* basi Serikali ingechukua

juhudi za makusudi, ili kuwawezesha na *Private Sector* nazo kujiunga katika mambo haya ili kuwasaidia hawa wafugaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa namba 6 kwenye muelekeo wa baadae katika Sekta ya Mifugo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sioni kwa nini mpaka sasa Serikali yetu hii tukufu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, lakini bado kuna matatizo ya hapa na pale, lakini hii siilaumu Serikali ni kwamba bado tunategemea tukusanye na baadae tutumie.

Kwa hivyo mfumo huu wa kukusanya fedha za mapato kutoka maeneo mbali mbali na tunakuwa hatuna uhakika. Kwa sababu mara nyingi tumeona kwenye bajeti kwamba kile kinachokisiwa kukusanywa kinakuwa ni kidogo hakipatikani kama ilivyo, hatukusanyi kama ilivyo, na ningeishauri Serikali kwamba kwanza ule ukusanyaji wa mapato wayadhibiti vizuri ili yasiwe yanavuja.

Kwa hivyo ni lazima hili litatokea wala si jambo la kulaumu sana, kwa sababu wenzangu hapa wamesema kwamba tule tunachokipata tugawane kidogo kidogo, kwa hivyo ukitizama na hali hiyo ni lazima tuone kwamba Serikali ina nia nzuri ya kufanya mambo mengi lakini kinachopatikana kinakuwa kidogo. Lakini kuna maeneo mengi ambayo tunasema ya ukusanyaji wa mapato au vianzio vyetu vya mapato vinapotea potea.

Nimeona katika hata zile hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara nyingi kuna maeneo kama kwenye *land lease*, kwenye *land lease* kuna aidha watu wamechukua maeneo lakini hawalipi zile *lease* zenyewe na ni mabilioni ya pesa.

Kwa hivyo kupitia sekta hiyo tu ya ardhi kuna mapesa mengi ambayo yanapotea. Kwa hivyo ni lazima sasa hivi Serikali itilie mkazo katika maeneo yale.
Tumeona vile vile kwenye hiyo hiyo sekta ya ardhi wawekezaji wamejenga zile *jet*, lakini zile *jet* hazikujengwa pia kisheria, na vile vile imekuwa haifuatilii Serikali mapato ya maeneo kama yale.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Serikali lazima iwe na mkakati wa makusudi kuona wapi pesa zile zinavuja ndizo zitakazotusaidia katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi ni muhimu na inachangia katika pato la Taifa na kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Tume ya Mipango sekta hii ndogo inachangia kwa kweli kiasi kikubwa.

Mwaka 2014 mifugo imechangia kama asilimia 7.5%, uvuvi umechangia 8.9% pia uvuvi kwa mwaka 2014 inaonesha kwamba umeongezeka kwa tani 32,924 ukilinganisha na mwaka 2013 ambayo ilikuwa ni tani 30717 na kuchangia pato la Taifa kwa mwaka 2014 shilingi bilioni 127.2 ukilinganisha na mwaka 2013 ambayo ni bilioni 111.9.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hizi ni takwimu ambazo tumepata kutoka Tume ya Mipango na niipongeze kwa kutupa takwimu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona hapa pia katika hiyo sekta ya uvuvi kwamba kuna mafanikio yaliyopatikana, kukamilika kwa ujenzi wa soko la samaki na mboga mboga kule Tumbe Pemba.

Kwanza nishukuru kwa kumalizika kwa soko lile kwa sababu kuna kipindi tulikwenda na kamati yangu ya *PAC* tukaliona lile eneo lililojengwa, na kwa kweli ilikuwa hakukuwa na *value for money*, kwa sababu ni muda mrefu lilikuwa limekaa tu bila ya kutumiwa. Na kama kitu hukukitumia umeshakitayarisha lakini ukawa hukukitumia kwa kweli inakuwa ni tatizo, kwa sababu kutakuwa hakuna hasa ile faida ambayo imepatikana. Kwa hivyo hata baadaye linaweza likachakaa na kuharibika bila ya kufanyiwa kazi, kwa hivyo *value for money* inakuwa haipo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Idara hii ya Uendeshaji na Utumishi. Mimi kwanza niipongeze kwa uwajibikaji wao wa kuandaa na kutekeleza mipango ya mafunzo kwa watumishi, kuratibu kazi za uhasibu, manunuzi, ukaguzi wa ndani na hesabu za wizara kusimamia masuala ya mtambuka kama jinsia, ukimwi, mazingira ulemavu, utawala bora na kadhalika.

Kwa kweli hii niipongeze kwa sababu ya kuwajibika huko, kwa sababu bila ya kuwapa mafunzo watumishi hawawezi kufanya chochote. Vile vile kuratibu kazi ya uhasibu ni jambo la msingi, kwa sababu bila ya wahasibu basi hatuwezi kufanya, yote haya tunayofanya yatakuwa ni bure kwa sababu bila ya uhasibu hawawezi kuweka vitabu vyao kama kawaida vya kupanga mahesabu na wakajua nini kimetumika na kipi kilichobakia na kufanya *reconciliation* wakajua ni nini tumekitumia. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli naona mimi mafanikio ni hayo lakini pia ile pesa tukaisimamia vizuri ni jambo la kulizingatia.

Mhe. Mwenyekiti, malengo ya mwaka 2014/2015 nimeona katika hiyo Idara ya Mipango kuendelea kufanya ukaguzi wa hesabu za mapato na matumizi ya fedha na zana za Serikali hilo ni jambo la msingi, ni lazima kuwe na jambo hilo la ukaguzi, bila ya ukaguzi mtu anaweza kufanya mambo yake anavyotaka.

Kwa hivyo hilo ni jambo la msingi. Lakini vile vile nimeona kwamba kuendelea kusimamia haki na wajibu wa watumishi hili ni jambo vile vile stahiki lazima tuwasimamie na haki zao, pia wapewe watumishi kwa sababu hawana wanakotegemea isipokuwa wanaifanyia Serikali kazi, basi kwa hivyo na hasa niseme kwenye stahiki zao wapewe kama kuna *overtime* zao wapewe, na vile vile kama kuna fedha za likizo pia wapewe na hii ni Idara muhimu katika wizara.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda Idara ya Uzalishaji Mifugo malengo kwa mwaka 2014/2015 ni mazuri lakini kuna lengo hili la msingi kuongeza uzalishaji, mifugo na mazao yake kwa kutumia mikakati ifuatayo:

i.Kuimarisha huduma ya ugani hili ni jambo la msingi.

ii.Kuvijengea uwezo vituo vya utafiti wa mifugo.

iii.Kuongeza thamani za ubora wa mazao, bidhaa za mifugo

Haya yote ni mambo ambayo ni muhimu sana, lakini jambo ambalo tunasema kwamba tuwaongezee uzalishaji wa mifugo, lakini tumeona kwamba changamoto zilizopo ni kwamba kwanza hatuna wataalamu wa kutosha wa hiyo mifugo yenyewe, lakini tukisema tunataka tuzalishe kwanza tutafute lile kero au tatizo ambalo linatukabili, hatuwezi tukasema kwamba tunazalisha lakini sasa kuna matatizo pengine ya wataalamu wa mifugo.

Kwa hivyo lazima kwanza tuone kipi cha mwanzo na halafu kipi kitafuata, kwa hivyo Mhe. Waziri hilo ni jambo la msingi kabisa liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Idara hii ya Maendeleo ya Uvuvi. Mhe. Waziri amesema Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ina jukumu la kuwahudumia wavuvi pamoja na wadau mbali mbali wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi. Kwa hivyo hili Mhe. niiombe Serikali kama inataka maendeleo ya uvuvi kwanza kuwe na vitendea kazi. Kwanza tumesema tunakwenda kwenye uvuvi wa bahari kuu, na kama bahari kuu basi mpaka sasa hivi hatuna vyombo hata hivyo vya kuendea kwenye bahari kuu.

Kwa hivyo ni lazima serikali ijiandae kwa hilo, kwamba lazima hata ile Sheria ya *PPP* pia itumike ili kuweza kupata uvuvi ambao utafika huko hiyo miundombinu ya kwendea huko.
Mhe. Mwenyekiti, kwenye hayo hayo maendeleo ya uvuvi ukurasa wa 28 anasema utafiti juu ya kiwango cha samaki katika maeneo ya maji ya ndani haukufanyika. Pia ufatiliaji wa tathmini za matumbawe yaliyowekwa Chwaka na Maruhubi haukufanyika. Sasa sijui haukufanyika sababu ni zipi ambapo hazikufanyika kwa utafiti huo.

Nikiendelea inasema kwamba Mhe. Waziri ametwambia kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ilitekeleza mradi mmoja wa kuimarisha uvuvi wa kina kirefu cha maji ambao uliombewa jumla ya shilingi 261,600,000 kutoka SMZ. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 mradi huu uliingiziwa jumla ya shilingi 78,000,000 ambazo ni sawa na asilimia 30 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli fedha hizi ni kidogo bado na niseme kwamba bajeti inakuwa ni ndogo kusema kweli na inakuwa yale malengo hasa yanakuwa hayafikiwi na hii inakuwa ni athari ya kibajeti.

Mhe. Mwenyekiti, naona unakamata kamata hapa lakini bado itakuwa labda muda bado ninao kwa sababu nina mambo mengi kidogo humu ya kuchangia. Mara nyingi tunakuwa tunategemea wahisani…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa endelea wala wasikukere hao una dakika 10 nyengine.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, tumeona kwamba Mhe. Waziri amesema kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Mazao ya Baharini ilitekeleza mradi mmoja wa kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini ambao uliombewa shilingi milioni 176,400,000 kutoka SMZ na shilingi milioni 384,680,000 kutoka washirika wa maendeleo, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 mradi huu uliingiziwa shilingi 5,000,000 sawa na asilimia 3 kutoka SMZ na shilingi 36,000,000 sawa na asilimia 9 kutoka *FAO*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tumeona namna gani fedha za wahisani zinapatikana kidogo na mara nyingi inakuwa wao ndio tunawakisia kwamba watatoa pesa nyingi. Ni yale yale ya kawaida ambayo nasema mtumai cha ndugu hufa masikini siku zote, kwa hivyo tusitegemee sana wahisani kutokana na hali tunavyoona sasa namna wanavyotusaidia. Kwa hivyo, ni lazima tujiimarishe sisi wenyewe zaidi kuliko kwa kuwategemea wahisani.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwenye muhtasari wa mapato na matumizi kwa mwaka 2015 kwa kweli pia nagundua kwamba 2014/2015 wizara ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 613,000,000 kati ya mapato hayo shilingi 400,000,000 kutokana na leseni ya uvuvi wa bahari kuu na shilingi 213,000,000 kutoka kwa mapato ya ndani ya wizara. Ada ya leseni za uvuvi wa ndani, utabibu wa wanyama, ada ya mazao baharini hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 ilipita lengo na kukusanya jumla ya shilingi milioni mia tano sabiini na moja, arubani na moja elfu mia nane sawa na asilimia 143.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niulize kwa nini kwa sababu makisio ndio makisio na makisio yote huwa yanapitishwa kwenye Baraza hili la Wawakilishi, na kinachokusanywa hapa, tunachokipitisha hapa basi kisipitane sana aidha kikizidi tunataka tujue kwa nini kimezidi na kikipungua vile vile tuseme kwa nini kimepungua.

Kwa hivyo, ni lazima tujue kwa nini fedha hizi pengine kulikuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya hizi. Lakini sasa tukakisia kidogo kwa hivyo hapa inatia mashaka kidogo kwa nini tukakisia kidogo na tukapata kingi. Hapa ni fedha ya umma ambayo inananihii, kwa hivyo lazima tuzingatie kile tunachokikisia na kile ambacho tume…

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kuna moja hii utabibu wa wanyama, kwa kweli mimi niipongeze sana kwa taasisi hii ya mifugo kwa kuwashughulikiwa wanyama mbali mbali. Siku moja mtoto wangu wa kiume nilicheka kwanza nikashangaa nimetoka kidogo, mtoto wenyewe alikuwa unajua watoto wetu alikuwa kidogo hakuwa katika hali ya kawaida, alikuwa ameshajiingiza ingiza kwenye mambo ya madawa madawa, lakini kwa bahati nikamuwahi.

Sasa nimerudi nyumbani ananiambia mama yule paka wangu nimempeleka hospitali kapata kitanda, (amelazwa). Kwa hivyo, nilishangaa kwanza nikacheka, lakini baadae kufatilia kweli alilazwa yule paka na akawa mwenyewe anamfatilia fatilia. Kwa hivyo, nilipongeze suala hili na niwapongeze kwa namna wanavyojali wanyama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kunastahili pongezi ya haya changamoto zipo maeneo mbali mbali nashukuru kwamba safari hii tumekwenda katika huu mfumo wa kibajeti ambao ni *reform* ambayo ni kupitia programu na niseme tu kwa hali ile ile lazima kuwepo na uwajibikaji na uwazi zaidi na fedha hizi ziwe na usimamizi, ili tuweze kufanikiwa kwa kile kidogo ambacho tumekipata, kwani tugawane hicho kidogo kidogo. Lakini tusilaumiane kwa serikali kuisema sana kwa sababu mfumo wetu tunaujua kwamba ni mfumo ambao ukusanye na utumie na kile kidogo tunachokipata lazima tugawane hicho hicho, lakini yale malengo kiasi fulani yatakuwa hayatofikia kama tunavyokusudia. Kwa hivyo, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani naunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa *hundred percent*. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, ahsante na mimi kupata nafasi ya kusema machache sana katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hivyo, basi nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha mchana huu kusimama mbele ya Baraza lako hili na nikupongeze wewe kunipa hii nafasi. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyowasilisha bajeti yake hii kwa vizuri sana, kwa *speed*

kama fundi wa charahani anavyoshona, kwa kweli alitumia muda mfupi lakini tulimuelewa.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii kama inavyoitwa mifugo na uvuvi ni wizara ya vitoweleo, kwa hivyo ni wizara ya vitu vya *protein* tupu nyama ni *protein*, samaki ni *protein*, chaza ni *protein*, maziwa yamezidi, kwa hivyo, hii ni *potential ministry*. Ni wizara ambayo inatupa vitu ambavyo ni muhimu sana katika uhai wa mwanadamu. Kwa hivyo, ni wizara moja muhimu sana ingawaje inaonekana kama ni wizara toto hivi, ni wizara yenye isiyokuwa na umuhimu mkubwa, lakini kwa sababu vitu vilivyomo ndani yake ni wizara muhimu sana kwa sababu mapembe yanahitaji kitoweleo, mashelisheli yanahitaji kitoweleo, muhogo unahitaji kitoweleo na vitoweleo vinapatikana katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nianze kidogo kwenye sekta hii ya mifugo na niangalie kwenye hiki kitabu cha Mhe. Waziri ukurasa wa 4 kwenye sekta ya mifugo, sehemu waliyoifanya wenyewe kuwa ya mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, kama kitabu kilivyojieleza kuwa hii wizara imefanikiwa kuongeza idadi ya ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kuku wa kisasa na mengineyo. Kwa hivyo, kutokana na ongezeko hilo pia wamepata kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita hizi 27 milioni mpaka kufika 29.9.

Ongezeko hili la maziwa linaleta faraja kwa sababu Wazanzibari tunapenda sana maziwa, watoto wanapenda maziwa, wanawake wanakunywa maziwa, wanauma wanakunywa maziwa zaidi kuliko wote. Kwa hivyo, ongezeko la maziwa limeleta faraja kwa watumizi wa maziwa zaidi wanaume. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika kuna ongezeko kubwa la nyama, nyama ya ng'ombe imeongezeka, nyama ya mbuzi imeongezeka lakini kwenye ufugaji kumetajwa ongezeko la ufugaji wa kuku, lakini nyama ya kuku haikutajwa kwamba imeongezeka wala kupungua. Kwa hivyo, ningeomba kujua je hii nyama ya kuku haikuongeka, na kama imeongezeka katika mwaka uliopita na mwaka huu ni kiasi gani cha ongezeko? Na kama haikuongezeka kwa nini isiongezeke wakati ambapo ufugaji umeongezeka?

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ningependa kujua nyama hizi mbili ya ng'ombe na ya mbuzi ambayo imeongezeka zote ni nyama za ndani au nyengine zinatoka nje? Nyama za ndani nakusudia ng'ombe wa Zanzibar na wa nje wale ambao tunaagizia kwa ndugu zetu wa damu, ng'ombe hawa wote ni wa hapa ndani au wengine tunaagizia?

Sasa kama nyama imeongezeka kutokana na ng'ombe ambao tumeagizia kwa hivyo hapa hii Idara ya Mifugo itakuwa haijafanya kazi ya ziada, kwa sababu itakuwa tumewaagizia ng'ombe kwa ajili ya kupata nyama kutoka upande mwengine wa Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, ningependa Mhe. Mwenyekiti, nijue nyama hizi zilizoongezeka zote ni za ndani au nyengine ni za nje.

Mhe. Mwenyekiti, hapa pamoja na ongezeko hilo la maziwa, nyama ya ng'ombe na ya mbuzi lakini pato la Taifa limepungua kutokana na uzalishaji wa mazao haya ya nyama na maziwa. Sababu inayotajwa hapa imesema hii inatokana na kukua kwa sekta nyengine za kiuchumi. Kukua sekta nyengine za kiuchumi, si sababu ya kuwa sekta hii ya ufugaji tija yake kwa Taifa ipungue, tujalie nyama ilipoongezeka ilipungua bei.

Nyama ilipoongezeka ilikuwa haina wateja, siamini kuwa Zanzibar nyama ya ng'ombe na ya mbuzi kwamba inakosa wateja. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri anipe sababu hasa kwa nini uzalishaji ukaongezeka lakini pato la Taifa likapungua kwenye sekta hii ya mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, ufugaji hapa Zanzibar una changamoto zake kwa lugha yenu watu wa sasa, una matatizo yake. Mara nyingi tunapozungumzia hawa ng'ombe wa kisasa ni ng'ombe ambao tunaagizia kutoka upande mwengine wa Serikali hii ya Muungano na kuwaleta Zanzibar. Baadhi ya ng'ombe wanatoka katika sehemu za baridi mno, wanapoletwa katika visiwa hivi wanakuja katika sehemu ambayo ni ya joto kuliko kule walikotoka. Sababu hii pamoja na kukosa malisho bora, kwa sababu wafugaji wetu bado hawajakuwa na taaluma yakuwapatia chakula bora hawa ng'ombe wetu wa kisasa.
Sababu moja ya mabadiliko ya hali ya hewa, sababu ya pili ni ya kukosa malisho bora ng'ombe, hawa kwa kiasi fulani hawaishi muda mrefu wanakufa kutokana na sababu mbili hizo na ya tatu ni ile ya magonjwa.

Mhe. Mwenyekiti, shehia yangu uko mwaka mmoja ilipata ng'ombe 25 kutokana na Mradi wa *PADEP*, mimi nilipata ng'ombe mmoja. Katika 25 aliyebakia ni huyo wangu mimi tu na kwa sababu simchungi mimi na yeye angelikuwa ameshakufa hivyo hivyo, kwa sababu nimempa mtu anamshughulikia vizuri, katika 25 yuko huyo mmoja. Lakini kila anayezaliwa anakufa hii ni kukosa huduma za kimatibabu kwa hawa ng'ombe.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji mmoja hapa amesema kwamba Mhe. Mshimba yeye amesema kwamba ni mfugaji lakini mchangiaji amesema ndio kwa sababu Mhe. Mshimba kama akimpigia simu watu wa matibabu ya ng'ombe watamfika kulingana na hali yake.

Hii ni kweli kwa sababu huu Mradi wa *PADED* ulipoletwa pale mwanzo ambapo ulikuwa unahuduma zake madaktari wa mifugo ilikuwa mara kwa mara wanapita kwa wafugaji kujua matatizo yao. Lakini *balance* ya ule mradi ilipomalizika ikawa sasa mfugaji anajitegemea daktari hata umpigie simu anajua hapo hakuna kitu atakwambia kesho, kesho ng'ombe wanatoka kamasi hatimae anapotea. Kwa hivyo, huduma za matibabu bado ni duni na zinahitaji wizara waelimishe watibabu wao kuweza kuvipitia vikundi vya wafugaji, ili kuwapatia hawa wanyama huduma, vyenginevyo itakuwa tunafuga bila ya tija yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, pia kitabu hiki kimezitaja changamoto za huu ufugaji, wamesema upungufu wa wataalamu na nyezo za kufanyia kazi kwa baadhi ya vitengo kama utafiti, ugani na utabibu wa mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii au sehemu hii ya Sekta ya Mifugo inahitaji kusiwe na upungufu wa wataalamu hawa. Kwa sababu wanyama wana maradhi mengi inabidi wafanyiwe utafiti na uchunguzi wa hali ya juu. Kwa sababu kuna baadhi ya magonjwa yanayowasibu wanyama mwanadamu anapokula nyama ya mnyama aliyeathirika na baadhi ya magonjwa na yule mlaji naye anaathirika na baadhi ya wakati ng'ombe wanachinjwa madaktari wanapomtizama wanathibitisha kuwa hii nyama kuliwa haifai inaangamizwa. Sasa lazima kuwe na madaktari, kuwe na watafiti watakaohakikisha kuwa kila nyama inayoliwa ni salama kwa mlaji, kila maziwa yanayonywewa ni salama kwa mnywaji, kila kuku anayeliwa ni salama kwa mlaji.

Mhe. Mwenyekiti, mara moja nilihadithiwa na mzee mmoja humu Barazani wale kuku tunaoagizia huoni kwamba wadogo, lakini vinatiwa sindano wanapigwa dawa wanavimba wanakuwa wakubwa. Kama ile ni kweli hawa kuku tunaokula kwa kweli ni hatari kwa sababu ni kuku ambao wamekuwa *injected,* kupata huo unene walioupata.

Hii inaweza kuwa ni kweli kwa sababu hata wanadamu wanajidunga sindano ili yawe mabonge. Kwa hivyo, inawezekana na hawa kuku wanafanywa kweli hivyo, kama ni kweli ni hatari iliyoje sisi kula nyama ya kuku iliyoingizwa madawa ambayo hatuyajui athari zake za baadae.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo huu utafiti katika sehemu hii ya mifugo ni jambo kubwa na ni jambo la lazima, wizara ilitilie maanani kutafuta kuwasomesha watu kwa ajili ya kufanya utafiti katika sekta hii ya mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni changamoto moja niliyoiona, nyengine waliyoitaja ni uhaba wa malisho kutokana na ukame na wafugaji kutohifadhi malisho wakati wa mvua. Ni kweli hili ni tatizo kuwa bado wafugaji walio wengi hawajaelimishwa

namna ya kuweka chakula cha akiba cha mifugo yao. Kwa hivyo, wakati wa faraja ukimalizika ukija wakati wa ukame huwa ng'ombe, mbuzi, hawana chakula cha kutosha. Kwa hivyo, ni juu ya wizara kuhakikisha kuwa wanawapatia mafunzo ya kutosha wafugani namna ya kuhifadhi chakula cha akiba cha kutumia mifugo yao pale ukame unapojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine niliyoiona hapa ni fursa ndogo kwa wafugaji kupata mitaji. Ni kweli wafugaji walio wengi hawana mitaji na hii wizara inayoitwa ya uwezeshaji mitaji wanayotoa kwa kweli haikidhi haja. Huwezi ukamsaidia mfugaji kumpa mtaji ama kwa kukopeshwa kwa aina yoyote shilingi laki moja au mbili. Huu haujawa mtaji ni mitaji ya kuwadanganya tu, hakuna mtaji wa shilingi laki mbili kuwa unampa mtu tena kwa kujikweza tumemuwezesha, aka! unamuwezesha mtu kwa shilingi laki mbili akanunue kitu gani. Kwa hivyo, ili pesa zipatikane lazima hii mitaji ipatikane ya kuwawezesha kuendeleza huu ufugaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine wanasema utendaji mdogo katika viwanda vidogo vidogo vinavyosarifu bidhaa za mifugo. Bidhaa za mifugo ni pamoja na maziwa ina maana hatuna viwanda vya kutosha vya kuweza kuyasarifu maziwa yetu, hatuna viwanda vya kuweza kuisarifu nyama pengine kuitia katika makopo na kuifanya iwe bora kuiuza nje. Kwa hivyo, changamoto ni nyingi sana zinazoikabili sekta hii ya mifugo. ili kuondokana na changamoto hizo wafanye nini? Wameeleza wenyewe katika mwelekeo wa baadae.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hawa watu ni wataalamu kwa kima fulani, kwa sababu zile changamoto ndio hatimae walizozigeuza kuwa ni mwelekeo wao wa baadae, zile changamoto zao wamezi-*convert* sasa kuwa ndio mwelekeo wao wa baadae.
Kwa mfano hapa kuna mwelekeo mmoja kuendelea kutoa taaluma ya uhifadhi wa malisho kwa wafugaji. Kule wameshaonesha kuwa uhaba wa malisho, hapa wamebadilisha lugha kidogo tu kwenye mwelekeo wao wameweka katika lugha nyengine.

Kadhalika, mwelekeo wao mwengine kuwaunganisha wafugaji na taasisi za kifedha na Wizara ya Uwezeshaji ndio mwanzo nimeitaja hapa fursa ndogo za mitaji. Sasa huku ilikuwa ni changamoto, sasa wameigeuza kuwa ndio mwelekeo wao. Kwa hivyo, mwelekeo wao umo ndani ya changamoto zao, mwelekeo wa wizara hii zile changamoto zao ndio mwelekeo wao sijui wataelekea vipi ndani ya changamoto jambo ambalo wameshalifanya kuwa changamoto, baada ya kutafuta ufumbuzi wake wamefanya kuwa ndio mwelekeo wao na zote ya kwanza mwelekeo wao ndio ule ule wa kwanza kwenye changamoto.

Mhe Mwenyekiti, hapa kwa mimi nimeona hii wizara haina mwelekeo wa baadae, kwa sababu wamechukua zile changamoto kufanya kuwa ndio mwelekeo wao. Lakini kwa sababu ni wataalamu wazuri wanaweza wakanisaidia kutokana na dhana hiyo niliyoiona mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakia dakika tano kumalizia.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, kama ni dakika tano itabidi nikimbie kidogo niende katika ukulima wa mwani. Katika kitabu hiki kimeutaja mwani kama ni zao la pili linalosafirishwa kwa wingi nchi za nje. Lakini zao hili ni zao ambalo lina tabu kubwa sana katika uzalishaji wake na wazalishaji wakubwa wa mwani ni kinamama. Uzalishaji wa zao hili kunaathiri na unaharibu mazingira. Kwa sababu wanakata miti baharini kule wanayochomeka kwa ajili ya kutega hivyo wanavyofanya wenyewe, wanaweka kamba zao lakini kila siku, kila msimu wavunaji wa mwani miti mingi inakatwa kupata zile pigi au sijui wanavyoita wenyewe, lakini najua kuwa wanakata mbichi.

Je, hakuna mbinu mbadala ya kutumia ile miti inayokatwa wakapata jambo jengine la kufungia kamba zao, ili kunusuru hii miti kuipoteza kila siku?

Halafu pamoja na kazi kubwa ya huu mwani, bado mzalishaji faida yake anayopata ni ndogo mno. Kwa hivyo, serikali au wiara hii iwatazame hawa wazalishaji wa mwani katika jicho la huruma, kama mwani umefanywa kuwa ni zao la pili la kusafirishwa pengine soko letu huko nje ni zuri kidogo. Pamoja na kuwa si serikali moja kwa moja inayosafirisha, lakini hizo kampuni na taasisi zinazosafirisha serikali inajua ni kiasi gani wanauza huko katika soko wanalouzia.

Kwa hivyo, serikali iwatake, iwaombe na iwashawishi hawa makampuni yanayonunua mwani kuongezea hawa uzalishaji bei, ili na wao angalau waweze kufaidika na kazi ngumu, nzito wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, hapa mwani kuna kijana mmoja juzi alinilalamikia kuwa yeye kajisajili kuwa ni mfanyabiashara wa kuuza mwani, lakini hatimaye wafanyabiashara wakubwa waliingilia kati na biashara yake yeye ikawekewa vikwazo na hatimae akafunguliwa mashtaka kama alivyonieleza, lakini kwa sababu kafunguliwa mashtaka sitaki niseme lolote.

Mimi nilikuwa nataka kusema kuwa wafanyabiashara wakubwa wasiwe wachoyo wanapotokea wengine kwenda kuwekeza katika biashara wanayofanya wao. Kwa sababu kila mmoja mwenye uwezo ana haki na fursa sawa na yeye kwa kufanya biashara ambayo anataka kuifanya, wasiwe wachoyo wala wasione kuwa wao watashindwa biashara ni ushindani, kila tukipata watu wengi zaidi, makampuni

mengi ambayo yanasafirisha ndio vile vile tutakapomuongezea soko huyu mzalishaji mdogo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kutoa machache niliyotoa. Shukrani.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa.

Vile vile nichukue nafasi ya kukushukuru wewe pia kunipa nafasi hii angalau na mimi kwa uchache kutoa michango yangu kuhusiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Aidha, nimshukuru Mhe. Waziri wa wizara hii, Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara yake katika kufanikisha lengo zima la kuwapatia maendeleo wananchi wetu katika sekta hii ya uvuvi pamoja na mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika Sekta ya Mifugo ukurasa wa 4, Mafanikio katika sekta ya mifugo, niende katika kifungu cha (iii). "Kuongezeka kwa uzalishaji wa nyama ya ng'ombe kutoka tani 4,966 mwaka 2013 hadi kufikia tani 5,135 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 3.4".

Mhe. Mwenyekiti, wengi miongoni mwa Wajumbe wamelizungumzia sana suala hili la ongezeko la nyama katika visiwa vyetu hivi vya Zanzibar. Bila shaka dhana yangu nilikuwa mimi nadhania kwamba ongezeko hili la kupatikana kwa nyama basi ni ongezeko la kuwa na mifugo mingi ndani ya visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba. Kama hivyo ndivyo namuomba Mhe. Waziri anifahamishe ongezeko hili ni kwa ajili ya wanyama hawa ng'ombe kuwepo hapa visiwani au ni ongezeko la nyama tu kutoka katika sehemu nyengine ya visiwa hivi.

Kwa sababu nikiangalia sioni kwamba kuna maeneo ya kufuga ng'ombe wengi wa kuweza kupata nyama hii kwa kipindi hiki. Kwa hivyo, naomba Mheshimiwa atupe ufafanuzi, ili tuweze kuelewa kwamba ni nguvu gani ya kiuchumi kupitia mifugo ya ng'ombe kwa kuongezeka nyama kiasi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika changamoto kwenye Sekta ya Mifugo. Mheshimiwa miongoni mwa changamoto ambazo wamezitaja hapa ni upungufu wa wataalamu na nyezo za kufanyia kazi kwa baadhi ya vitengo kama utafiti, ugani na utabibu wa mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kukosekana kwa wataalamu tosha katika wizara hii ni tatizo, hii ni wizara muhimu imeanzishwa bila shaka kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi Wazanzibari ambao miongoni mwao wengi wao ni wafugaji.
Kwa hivyo, niiombe wizara na serikali kwa ujumla upungufu huu wa wataalamu usiendelee, kwa sababu kuendelea kwa upungufu wa wataalamu katika wizara basi ndio kuwafanya wafugaji wa visiwa hivi kuwa duni katika ufugaji wao. Hivyo, naiomba sana wizara kwanza ishirikiane na Wizara ya Ajira iwaajiri wataalamu wa mifugo lakini pia wizara iwasomeshe wafanyakazi wao wenye sifa za kufikia utaalamu huu, kukosekana kwa wataalamu kwa kweli ni tatizo.

Kwa hivyo, niiombe wizara iwe makini sana katika kutafuta wataalamu, ili wafugaji wetu pamoja na wananchi kwa ujumla wafaidike katika suala zima hili la kuwa na mifugo bora kwa kupata ushauri ambao unakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika kifungu hicho hicho cha changamoto kifungu cha (ii), "Uhaba wa malisho kutokana na ukame wa wafugaji wengi kutohifadhi malisho wakati wa mvua".

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili kwa kweli ni tatizo kubwa na linahitaji wizara iweke miundombinu madhubuti katika yale maeneo ambayo wafugaji wetu, wanajitahidi kupanda miti kwa ajili ya malisho ya wanyama. Naamini kwamba miongoni mwa changamoto ambazo zinakabili malisho yetu kuwa kidogo inawezekana kwamba maeneo ya kupanda malisho hayajatayarishwa rasmi. Kwa hivyo, niiombe wizara ilishughulikie sana suala hili na pia maeneo yale yatakayotengwa kwa ajili ya malisho basi wizara iwezeshwe miundombinu ya kupatakana kwa maji. Kuchimbwe visima vya kutosha ili kuwe na umwagiliaji kwa ajili ya malisho ya wanyama.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende katika sekta ya uvuvi. Kipengele ambacho nitakizungumzia hapa katika sekta ya uvuvi ni mafanikio katika sekta ya uvuvi. Mafanikio niende katika kifungu cha pili kidogo. Wananchi wengi wameshajihika kwa kuendelea ufugaji wa mazao ya baharini kwenye maeneo yao. Jumla ya vikundi mia moja arubaini na nne vya ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini vimeanzishwa Unguja na Pemba, Unguja vikundi 51 na Pemba 93.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi niwapongeze sana wananchi walioanzisha vikundi hivi kwa ajili ya ufugaji wa mazao ya baharini ikiwa ni pamoja na ufugaji wa samaki. Hii ndivyo wananchi wetu walivyoitikia wito wa serikali kwamba wananchi wajiajiri wenyewe. Lakini inasikitisha sana kwamba vikundi hivi serikali imevitelekeza. Wananchi wetu wengi wameamua ufugaji wa samaki katika maeneo

mbali mbali, lakini serikali inachokifanya kwa vikundi hivi ni kwenda kuwasaidia pauro tano au *pump* moja ya maji ya shilingi laki moja na hamisini.

Mhe. Mwenyekiti, lengo halifikiwi kuna vikundi vingi kwa mfano kuna vikundi katika jimbo langu la Chambani zaidi ya vikundi saba vinavyofuga samaki. Lakini tokea waanze uzalishaji huu wa ufugaji wa samaki kinachofanyika ni kupewa pauro tano, mashine ya maji ya shilingi laki moja na nusu, wanauza ngombe wao kwa ajili ya kujiimairisha, lakini matokeo yake wanashindwa kwa sababu mtaji wanaouanza ni mdogo na serikali inashindwa kwa asilimia kubwa kuwasaidia.

Mimi naamini kwamba ikiwa wizara itakuwa makini katika kusimamia suala zima la samaki, samaki wangetosheleza katika maeneo yetu ya Zanzibar kusingekuwa na haja ya kuagizishia samaki kutoka China au nchi nyengine. Ni aibu na mimi niungane na wasemaji waliotangulia kwamba Zanzibar ni visiwa ambavyo vimezungukwa na bahari na tuna mabwawa mengi ya kufugia samaki.

La kusikitisha, leo unakutia mapeduu ya samaki wanatoka China. Kwa nini samaki hawa hawatoki Uroa na Chambani au Pujini na kwengine neko. Kwa sababu wananchi wameshindwa kuwezeshwa, tunakwenda tu kuwaambia kuwa haya anzeni mitaji serikali itasaidia lakini msaada ya serikali kwa kweli ni wa maneno matupu si wa vitendo. Sasa nimuombe Mhe. Waziri atwambie hasa ni mikakati gani wa kuviwezesha vikundi hivi ili vikaweza kujitegemea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika mchango wangu niangalie jinsi ya serikali isipovipa vipaumbele vikundi hivi vya ufugaji wa samaki. Niende katika ukurasa wa 52 nilinganishe hapa, kuna kiambatisho namba 3 *column* ya kwanza hapo kuna idara, halafu kuna mradi makadirio fedha zilizopatikana na asilimia ya upatikanaji. Niende katika huduma za utaratibu wa mifugo.

Hapa huduma iliyofanyika udhibiti wa kichaa cha mbwa, ulikadiriwa kupewa fedha shilingi milioni ishirini na tano.
Kuanzia Julai 2014 hadi Machi 2015 kichaa cha mbwa wameingiziwa milioni ishirini sawa na asilimia 80. Lakini nikienda katika mstari wa chini yake Idara ya Mazao ya Baharini. Mradi uliokusudiwa hapa ni kuimarisha ufugaji wa samaki. Makadirio 2014/15 ni milioni mia moja na sabini na sita na laki nne, fedha zilizoingizwa Julai 2014 hadi Machi 2015, ni shilingi milioni tano sawa na asilimia tatu. Sasa jamani tunakwenda wapi na tutafika wapi?

Kuhusu kichaa cha mbwa, nakuomba Mheshimiwa utwambie kichaa cha mbwa wameingiziwa milioni ishirini. Hivyo, Zanzibar ni Mkoa gani, Wilaya gani, Shehia gani ambayo inakuwa na kichaa cha mbwa kiasi ya kuingiziwa milioni ishirini kwa kipindi hiki lakini tukaacha kuwaingizia wavuvi wa samaki, wafugaji wa samaki

katika maeneo ambayo sisi ndio tunamoishi na kuwaona watu wanavyohangaika. Wanawake wameingia susa za mikono kwa ajili ya kupiga matuta ya kuzuia maji, leo tunawaingizia asilimia tatu.

Kichaa cha mbwa tunaingiza fedha kwa asilimia thamanini, naomba ufafanuzi wa kina. Hivyo, mbwa hawa wako katika Wilaya gani, katika Mkoa gani ili tujue kwamba mbwa waliopigwa sindano kwa ajili ya kuzuia kichaa cha mbwa Wilaya ya Mkoani. Shehia ya Chambani Jimbo la Chambani walikuwa mbwa mia au tano au kumi. Shehia ya Mangapwani, walikuwa mbwa kadhaa na wametogwa sindano zenye thamani kadhaa.

Naomba Mhe. Waziri utupe ufafanuzi huo kwa sababu siamini, mimi kwamba asilimia tatu za wafugaji wa samaki kwa kweli zinaweza zikawakombowa katika maisha ya ufugaji wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika mafanikio, kifungu cha tatu hapo kidogo. Kutiwa saini makubaliano baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Shirika la Korea *KOICA* juu ya kuanzisha mradi wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki huko Beit- el Ras.

Je, Mheshimiwa tayari imeshatiwa saini lakini kituo hicho kitajengwa kuanzia lini, kwa sababu kutia saini kitu mbali na ujenzi kitu mbali na hivi vifaranga kwa kweli limekuwa ni kero sana, wafugaji wengi wa samaki wanakuwa na usumbufu mkubwa sana wa upatikanaji wa vifaranga hivi samaki.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba utuwekee wazi kwamba baada ya kuweka saini hii ni lini ujenzi huu utajengwa ili kuweka vifaranga vizuri na kuwapungizia matatizo hawa wafugaji wetu wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mafanikio ya wizara hapa kuna kifungu cha nne hiki kukamilika kwa mabwawa matano ya mfano ya ufugaji wa samaki. Mabwawa haya yako wapi naomba utufahamishe, ili tujue kwamba mabwawa yametengenezwa na yako wapi na wapi na wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mafanikio katika kifungu cha sita kuanzishwa kwa mashirikiano baina yetu na Wizara ya Kilimo na Uvuvi wa Serikali ya Oman. Mafanikio gani yaliyopatikana katika mashirikiano haya. Naomba tu yale mafanikio ambayo yamepatikana katika mashirikiano ya wizara pamoja na serikali ya Oman.

Nikiendela na mchango wangu niende katika zao la ukulima wa mwani. Asubuhi tulipewa kijarida hiki kutoka Ikulu na nashukuru kwamba hapa mbele kwanza

kuna picha anaonekana hapa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tunamuona Mhe. Waziri wa Uwezeshaji pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wengine.

Kuna maelezo kwamba SMZ inavyoliimarisha zao la mwani, wakulima wanatumia kutengeneza bidhaa mbali mbali. Nikifungua ndani ya kitabu hichi hapa nataka nisome ukurasa wa tatu unasema kwamba kilimo cha mwani Zanzibar ni moja kati ya shughuli muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar, ikizingatiwa kuwa hivi sasa kilimo hicho kinaajiri zaidi ya watu ishirini elfu, wengi wao wakiwa wanawake wa vijijini na ni zao la pili katika mazao yanayosafirishwa kwa wingi nchi za nje hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, haya maelezo ni mengi lakini nilitaka nisome haya kwa uchache tu kutilia nguvu kwamba kumbe zao la mwani serikali inatambua kwamba ni zao miongoni mwa mazao ambayo yanapatia pato la taifa Zanzibar.

Pamoja na kwamba karibuni walipewa vihori wakulima wa mwani ni hatua nzuri sana na ni jambo ambalo kwa kweli limewasaidia sana hasa hawa kina mama. Lakini bado zao la mwani linakabiliwa na bei ndogo.

Mheshimiwa katika kitabu cha waziri amesema miongoni mwa changamoto ni bei ndogo ya mwani. Lakini nashukuru kwamba zao la mwani limeingizwa katika gazeti la Ikulu kwamba ni miongoni mwa zao la pili, miongoni mwa mazao ambayo yanasafirishwa nchi za nje.

Sasa niombe serikali kwa ujumla wake zao la mwani kwa hali yoyote lifanyiwe utaratibu wa kuengezwa bei hawa wanaokuja kununua zao hili wasiwalalie wasiwadhalilishe ki bei wakulima wa mwani. Tumekaa miaka mingi tunapiga kelele kuhusu karafuu. Karafuu hazina bei, lakini *alhamdulillah,* si muda mrefu sana katika hiki ambacho wakulima wa zao za karafuu *alhamdulillah* kilimo kile kimepungua kwa asilimia kubwa.

Sasa tunaiomba serikali kwa ujumla wake ukipunguze kilimo cha wakulima wa mwani Zanzibar, ili na wao wajisikie kwamba zao muhimu ni zao ambalo linapatisha faida na mapato ya serikali lakini pia ni zao ambalo wakulima wa mwani na wao wanapata faida.

Mhe. Mwenyekiti, zao la mwani lina kazi kubwa. Ukulima wa mwani unachokesha mno; kina mama wakirudi katika upandaji wa mwani taabani hata kulea watoto wao wakati mwengine tabu kutokana na kuchoka. Sasa kuchoka kwao kuambatane na bei ya mwani.

Mhe. Mwenyekiti, nishukuru sana kwamba na mimi nimepata muda angalau wa dakika mbili tatu wa kuweza kuchangia hotuba hii na mimi, niseme kwamba hotuba hii naiunga mkono kwa malengo yale yale ya kuwasaidia wananchi wetu wakiwa wafugaji wa samaki pamoja na wale kina mama na kina baba, ambao wanapanda mwani kwa ajili ya maslahi ya nchi na maslahi yao yakifamilia zao. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutufikisha hapa leo katika Baraza letu tukufu na kujadili hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuziweka wizara 16 katika nchi yetu na zikatengwa kila mwananchi akapata wizara.

Mhe. Mwenyekiti, mvuvi na mfugaji amebahatika kupata wizara, mfanyabishara kapata wizara, mwalimu na yeye kapata wizara na halkadhalika. Kwa hivyo, ni neema kubwa sana kwa kila mwananchi kupata wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar Mwenyezi Mungu ametujaalia kutupa uchumi mkubwa wa bahari na bahari imetuzunguka pande nne zote Kaskazi bahari, Urejua bahari, Uchejua bahari, Kusini bahari na ndio maana tukapata wizara ya wavuvi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachangia ukurasa wa 26 kifungu namna 3.5 kinachuzungumza:

"Idara ya Maendeleo ya Uvuvi"

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar na Pemba wananchi wengi au idadi kubwa zaidi kuliko zote ni wavuvi. Lakini kwa hawa tuliokuwa nao Mhe. Waziri bado wanavua uvuvi wa kimasikini, kitabu kinasema kwamba, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi inajukumu la kuwahudumia wavuvi pamoja na wadau mbali mbali wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya uvuvi serikali bado haijawaangalia hasa wavuvi na ndio wanaotia tija kubwa katika nchi yetu. Wajumbe wengi wamechangia kwamba nyama zimezidi, lakini kuzidi kwake zile nyama zinatoka nchi za nje, mapeduu yanatoka nchi za nje, nyama za mbuzi nje, za ngombe nje hata samaki nje.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba serikali kuwapati wavuvi wetu wa Zanzibar elimu ya uvuvi na vifaa vya uhakika, samaki tunao wengi sana. Lakini samaki tuliokuwa nao wako bahari kuu na wavuvi wetu hawana uwezo wa kwenda bahari kuu.

Kwa hivyo, serikali iwapatie zana wavuvi wetu ili waende bahari kuu kuvua samaki na watafutiwe soko ili wapate tija. Wavuvi wetu wa Zanzibar hata Bima hawana, wanaishi hivi hivi tu akizeeka, akiumia hana kinachomuendesha.

Kwa hivyo ukosefu wa dhana, ukosefu wa kutunza wavuvi ni moja wapo linatupa maendeleo kurudi chini.

Mhe.Mwenyekiti, Wizara yetu hii iangalie sana, iwatunze wavuvi. Wavuvi wanatia tija sana katika nchi, watafutiwe dhana za kisasa. Mhe. Mwenyekiti, kama Jimbo langu la Matemwe idadi kubwa ni wavuvi, lakini bado wanavua uvuvi wa kimaskini, hawana tija, hawana soko, hawana uwezo. Hivyo ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Uvuvi iwaangalie sana na iwahudumie sana wavuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nikenda katika ukurasa wa 22 Kifungu nambari 3.4 "Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo".

Mhe. Mwenyekiti, mifugo tunayo lakini vile vile mifugo yetu hatuna elimu nayo, mifugo yetu haina utibabu, mifugo yetu hatujaweza hasa kuitibu mifugo. Kwa hivyo ninaiomba Wizara ihakikishe kwamba wananchi wanapokuwa na mifugo yao, watuletee wataalamu na madaktari ndani ya vijiji vyeti ili hii mifugo ipate chanjo za uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, sisi sasa hivi kuku wetu tunakula sana wafugaji ni mahepe, waingie mahepe tutafune, hatujui amekutana na maradhi ya kuambukiza, hatujui namna gani tunatafuna tu. Kwa vile hatuna utaalamu, hivyo ninaiomba Wizara ituletee wataalamu watuhakikishie kwamba wanatibu wanyama, wanatibu ng'ombe, wanatibu mbuzi, wanatibu kuku, hawa wanakufa ovyo hawana utibabu mzuri. Kwa hivyo ninaiomba Wizara ishughulikie kipengele hichi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninakwenda katika sehemu hii ya ufugaji wa mazao baharini hasa katika ukulima wa mwani. Kama walivyosema wenzangu hapa kwamba mwani ni zao la pili kusafirishwa kwenda nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ya Mwani inafanywa sana na akinamama. Hivyo kama akinamama ni sehemu moja wanayotia fedha katika nchi yetu, nao ni sehemu moja ya kuangalia upo wa uhakika katika nchi. Kweli akinamama wanakwenda kufunga mwani kutwa na wanachoka lakini kipato kidogo.

Hivyo ninaiomba Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi wawaangalie akinamama wanalima mwani. Sasa hivi upande wa mashariki hasa kama kule kwetu Matemwe, akinamama wengi sana kidogo wamechoka kwa sababu wengine wamechoka, ule mwani hawapati tija, wamechoka hawana chochote, bei ndogo.

Halafu kutafutiwa mbegu iliyokuwa nzuri na bora ambapo sasa hivi zipo mbegu zikifungwa kule kwetu zinaoza za mwani. Kwa hivyo vile vile Serikali kupitia Wizara yake hii ihangaike kutafuta mbegu bora, ili wale akinamama nao wapate maendeleo mazuri.(Makofi)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikimalizia sina mchango mkubwa ninapongeza Wizara, ninampongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa hotuba yake hii hasa kuwaona akinamama hapa wanafunga mwani. Lakini nikimalizia kwamba mimi huko nyuma nilipiga kelele sana juu ya kujengewa viwanda, juu ya kununua meli za uvuvi, wenzetu sasa hivi wanaendelea, ule uvuvi wa zamani tweka-tweka sasa hivi unatoweka.

Sasa hivi watu wanakwenda kiutalaamu kisasa, tuna samaki wengi lakini hawavuliki kwa sababu hatuna zana. Kwa hivyo ninaiomba Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wavuvi wanunuliwe zana za kisasa, wavuvi wajengewe viwanda vya kusindikia samaki. Ndipo mvuvi atamvua samaki anajua anapeleka wapi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, dunia yetu inakwenda na viwanda. Nchi yetu tumeimaliza kujenga nyumba kiholela bila ya viwanda, tumejenga mahoteli nchi nzima lakini tumeshindwa kujenga viwanda na vile viwanda ndivyo vinavyochukua watu wengi, ndivyo vinavyochukua wafanyakazi. Tuchukue mfano Kiwanda cha Mahonda ambacho kinachukua zaidi ya elfu moja, elfu tatu, elfu nne, elfu tano.

Sasa tungekuwa na viwanda kama kile vitano, sita, saba, ninafikiri vijana wetu wasingekosa ajira. Kwa hivyo Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Ujenzi na Nishati wahakikishe wanaweka sehemu ya kujengea viwanda ili wananchi wetu wapate manufaa, bila ya hivyo itakuwa hatwendi.

Mhe.Mwenyekiti, ninakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdi Mosi Kombo, anayefuata ni Mhe. Panya Ali Abdalla baada ya hapo ni Mhe. Mussa Ali Hassan na kama muda utatosha basi ni Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako hili Tukufu kujadili masuala yetu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kusema machache katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Waziri na Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imeweza kutufikisha hapa tulipo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu katika sekta hii ya mifugo ambapo hapa imeonekana kuna mafanikio yamepatikana. Penye mafanikio lazima na tuipongeze Wizara kwa juhudi za mafanikio hayo, lakini na penye matatizo itabidi tuseme kwa sababu Serikali ndiyo baba, ndiyo mama lazima matatizo yetu yote pamoja na kwamba tunajua iliopo, uchache uliopo lakini lazima maelekezo tuyaelekeze kwao.

Kwa hivyo, tunapongeza kwa haya mafanikio ya kwanza idadi hii ya wafugaji imeongezeka na bila shaka kutokana na ongezeko bila shaka kuna elimu fulani imewapatia ndiyo maana wakaweza kuhamasika wafugaji ili wakaendeleza mifugo hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa hapa uzalishaji wa nyama umeongezeka, nyama ya ng'ombe, nyama ya mbuzi na tani zimetajwa katika kitabu hichi kwamba tani elfu nne, mia tisa na sitini na sita katika mwaka 2013 na hadi kufikia elfu tano, mia moja na thalathini na tano sawa na asilimia 3.4 katika mwaka huu 2015.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatua nzuri na tunaishukuru na kuipongeza Wizara kwa juhudi ingawa kila penye mafanikio lazima matatizo yawepo, huwezi kuwa na mafanikio matupu; lazima penye mafanikio na matatizo yatakuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo yapo na wenyewe hawakuyaficha wameyaonesha, changamoto zao wameweza kuzionesha kama pamoja na mafanikio haya lakini zipo changamoto ambazo zinatukabili. Hivyo ni vyema tukaweza kukaa na Serikali kuona basi tunasaidiana mbinu na mawazo katika kuzitatua changamoto hizi ambazo zilizopo.

Kwa kweli kama Serikali ingeweza tu kuleta vitabu hivi na ikasema basi tupitishe bajeti hii kwa kuviona tu vitabu, lakini haikuweza kufanya hivyo imeweza kusema lazima vitabu hivyo viletwe ndani humu na tuvichangie, ili basi pamoja na juhudi

kubwa waliyoifanya wao katika kukitunga hichi kitabu, lakini bado wanahitaji msaada wa mawazo kutoka kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili wanasema Waswahili;

"Kinga na kinga huenda moto ukawaka".

Hapa Wajumbe michango wanayoitoa Serikali itaweza kuyazingatia na hatimaye mawazo hayo tukichanganya kwa pamoja tunaweza tukafanikiwa kufikia mafanikio mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende katika Idara hii ya Mazao ya Baharini. Mhe. Mwenyekiti, kuna malengo hapa ya mwaka 2014/2015, wameweza kutuonesha wenzetu, malengo ambayo wamekusudia.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kweli nchi yetu hii pamoja na udogo wake lakini inaonekana una utajiri mkubwa kabisa. Hili bado tu hatujaweza kulifikia kwa sababu kutokana na ufinyu wa fedha ambazo tunazozipata mapato yetu bado ni madogo na mambo tunayo mengi, kwa hivyo hatuwezi tukayatekeleza yote kwa pamoja. Lakini ninaamini kwa malengo haya ambayo tumeyaona katika kitabu hichi, mimi niseme imani yangu kubwa mafanikio yapo na tutaendelea kuyaona isipokuwa subra inahitajika.

Mhe. Mwenyekiti hata Mwenyezi Mungu anatuhimiza anasema "*Innallah maa-swabirina*", hakika Mwenyezi Mungu yupo pamoja na wenye kusubiri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo na tumeona hatua ambayo tumetoka huko nyuma kweli mafanikio yanaonekana pamoja na uchache wa hayo mafanikio lakini yanaonekana kila mwaka tunapata mafanikio kidogo kidogo. Kwa hivyo, hii mimi niseme Serikali bado isichoke kutoa elimu kwa wafugaji wa samaki, wafugaji wa ng'ombe, mbuzi na wapandaji wa mwani.

Mhe. Mwenyekiti, elimu hii Serikali bado iwe ni endelevu, inaendelea kwa sababu kuna usemi ambao unaosema;

"Mwenda pole hajikwai na akijikwaa haanguki na akianguka haumii".

Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, usemi huu unatufanya basi kwamba pole pole lakini ipo siku Mwenyezi Mungu atatujaalia tutaweza kufika mahala pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe Serikali kuhakikisha inawapatia wakulima wetu hawa mwani elimu ya kutosha, hasa kwa sababu tunaona wengi wanaojishughulisha na huu ukulima wa mwani ni wanawake. Kwa hivyo,

tuwafundishe wanawake usarifu huu mwani ambao unaonekana sasa kwamba unatoa bidhaa mbali mbali kutokana na mwani huu.

Pia Serikali ihakikishe basi iwasaidie wanawake hawa katika kutafuta masoko, kwa sababu tunajua tukiwasaidia wanawake, ukimsaidia mwanamke mmoja maana yake umeisaidia jamii. Wanawake tunawaona wanavyojishughulisha katika kazi zao hizi na hatimaye wameweza kufanikiwa kuwasaidia akinababa majumbani katika kuwasomesha watoto na hata wale wanawake wajane, basi kutokana na shughuli zao wanazojishughulisha wameweza kuendeleza familia zao kutokana na kazi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika hii sekta ya uvuvi; sekta hii kuna mafanikio pia yamepatikana, tumeona hapa kuna tani thalathini elfu, mia saba na kumi na mbili hadi pia tumefikia tani thalathini na mbili elfu, mia tisa na sabini na tatu. Hizi ni juhudi ambazo zimechukuliwa na ndiyo maana mafanikio haya yakaweza kupatikana.

Ndani ya mafanikio haya bado changamoto zipo na sote tunaelewa kwamba ndani ya mafanikio yote ambayo tunayajua basi lazima changamoto ziwepo. Kwa hivyo kwa kuwa changamoto zinaonekana zipo basi niombe sasa Serikali kuangalia hii sekta ya uvuvi, kwamba lazima Serikali ijipange katika kuhakikisha kama itajipanga yenyewe Serikali au kutafuta mwekezaji, lakini tuhakikishe uvuvi wa bahari kuu sasa Serikali unaufikia. Hii itaongeza kuinua kipato au kuinua uchumi wa nchi yetu, lakini pia tutaweza kutengeneza ajira nyingi kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia tujitahidi katika kupata boti hizi za doria. Kuwa na boti hizi za doria ni vyema kwa sababu tunakuwa tunayaona meli saa nyengine zimeegesha huko pembeni, lakini kumbe wanatuibia raslimali zetu. Kwa hivyo, lazima juu ya hili tuangalie tujipange katika kutafuta boti hizi ili tuhakikishe raslimali zetu hazipotei.

Mhe. Mwenyekiti, niende na mimi katika hawa waanikaji wa dagaa. Kwanza mimi nichukue fursa ya kuipongeza sana Serikali kwa kuweza kukaa na mwekezaji huyu ambaye alijitokeza katika upande ule wa Nyanjale ambapo kunaonekana kuna mgogoro na waanikaji wa dagaa. Lakini tumeona changamoto ambazo walikuwa wakizipata waanikaji wa dagaa, lakini baada ya Serikali kukaa na mwekezaji ina maana amewatengenezea vizuri hawa waanikaji wa dagaa sehemu ya kuanikia dagaa ambapo kule alikupokuwa yeye mwenyewe ametaka waondoke, basi wameondoka na wapo katika eneo jengine wanafanya shughuli zao hizo kama kawaida.

Mwekezaji huyu pia aliwaahidi kuwajengea soko na tayari hilo soko limejengwa, lakini pia amewapa vifaa, kama gari za kuweza kushughulikia. Kwa hivyo sasa ni hatua nzuri ya kupongeza na tuombe tu hawa waanikaji wetu wa dagaa waendelee na shughuli yao hiyo ambayo imekuwa ni sehemu ya ajira katika maisha yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Waziri kupitia hawa waanikaji wa dagaa. Pamoja na mafanikio ambayo wanayapata lakini bado na changamoto wanazo. Nimuomba Mhe. Waziri kufanya ziara ya makusudi kwenda kuwaona waanikaji wa madagaa hawa, ili waweze kumpa changamoto ambazo bado zinawakabili, waweze kutatuliwa matatizo yao.

Mhe. Mwenyekiti, ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika ya kumalizia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Haya. Mhe. Mwenyekiti, pia wasi wasi wangu mkubwa katika waanikaji hawa wa dagaa ni soko la uhakika. Kwa sababu inaonekana wanakuja watu kulinunua lakini isije ikawa watu wetu wanafanya kazi kubwa na gharama lakini kumbe kipato kinachopatikana ni kidogo. Sasa niiombe Serikali basi iweze kwenda kupeleleza soko huko nje ili waje wawasaidie wafanyabiashara wetu hawa kuwatafutia soko zuri na lenye uhakika ambalo litakuwa na tija wao.

Mhe. Mwenyekiti, niende kidogo katika kuelezea shamba la mifugo Pangeni. Shamba hili lipo na lilipimwa tangu mwaka 1951. Shamba hili mara baada ya mapinduzi huwa kunafanyiwa uhakika tena wa kupata hati mpya kutokana na ile ya mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, shamba hili lilikwenda likapimwa na baadae watu wa Idara hii ya Mifugo walikwenda wakaweka uzio, uzio huo ukajengwa wa senyenge na mimi nilishuhudia kuuona uzio huo, lakini kuna baadhi ya maeneo uzio huo ulikuwa haukufika. Kwa hivyo, wananchi wakaona labda serikali imeishia hapa, kwa hivyo wakaona na wao sasa hili eneo lililobaki basi linaweza likawasaidia na wao kwa njia moja ya kilimo kwa maisha ya kuishi.

Mhe. Mwenyekiti, walichukua juhudi hizo za kupeleka maombi kwa Mkuu wa Wilaya na maombi haya pia yakafika Idara ya Ardhi. Mimi kitu ambacho sikifahamu labda ni yale majibu tu ambayo waliyapata kutoka huko Idara ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali ilikaa kimpya kwa muda mwingi sana bila ya kuwaambia chochote wananchi hawa, mpaka wakaweza kulima na kufanikiwa kupanda miembe mikubwa inazaa, minazi na kadhalika. Kwa hivyo, kwa hivi sasa

tukisema tuwanyan'ganye itakuwa hatukuwatendea haki. Lazima serikali ikae ipange na iwafikirie wananchi wake kuona suala hili basi wanalimaliza katika njia nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi hawa wameshapata shida sana katika kulihudumia hili shamba na sasa mazao yanapatikana. Mimi niiombe serikali iangalie kwa sababu ndio yenyewe na mimi huwa nahimiza hapa kila siku, jamani mashamba ya serikali tunayawacha kiholela, mashamba yanawachwa hayawekewi uzio, matokeo yake yanakuja kuvamiwa. Hata katika maskuli yetu tunahimiza Wawakilishi kila siku hapa, jamani jengeni uzio, kwa sababu wanakuja watu wengine kuvamia na kuchukua maeneo yale halafu sisi tunakuja kulalamika, na wakati eneo lile sisi tulilimiliki kwa muda mrefu. Kwa hivyo, sio busara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasemea shamba lile la Kipange ambalo lilikuwa shamba zuri na likitoa ndama wazuri. Shamba lile sasa hivi walikuwa wananchi wengi wakilima na wakifaidika kwa kupitia shamba lile. Lakini baadae shamba lile limekuja kuchukuliwa na serikali, wakaambiwa hapa patazalishwa ng'ombe, na kwa kuwa wananchi wetu sio wakaidi wakakubali na kweli maendeleo yalionekana na yalipatikana. Lakini shamba lile sasa limekuja kumilikiwa na mtu mmoja tu, ambapo wananchi hawaendei kufaidika.

Kwa hivyo, serikali ione kwamba kuna umuhimu kabisa wa kudhibiti hizi mali za serikali na tukazichunga, ili zisifikie kuvamiwa na tunapoona mtu anavamia basi serikali ichukuwe hatua mara moja ili kuona yule mtu anazuiliwa na tusiwache mpaka ikafikia hatua kama hii iliyofikia hapa. Matokeo yake tunapomdhulumu mtu yule tunamdhoofisha na kumuacha pengine anaweza akafa kihoro. Kwa hivyo, mimi naomba serikali izingatie juu ya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu haukuwa mkubwa sana isipokuwa nilitaka tu kuisisitiza serikali, kwamba sisi tunaelewa kuwa serikali yetu ina uwezo mdogo na inahitaji kutufanyia mambo mengi. Basi mimi niiombe pamoja na udogo wake huo, tuangalie lipi litakalokuwa la umuhimu zaidi basi tuweze kulitekeleza ili wananchi waweze kupata maslahi mazuri katika kuitegemea serikali yao hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichukuwe fursa hii kuunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa nafasi na mimi nikaweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hapa kuweza kuendelea na shughuli zetu za leo.

Vile vile nimpe hongera zaidi Mhe. Waziri kwa juhudi kubwa ya kuweza kupanga mipango mizuri ya shughuli zake pamoja na watendaji wa shughuli hizi. Kwanza sina budi Mhe. Mwenyekiti, niweze kuchangia katika ukurasa namba 3 kuhusu tatizo la biashara ya mwani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wajumbe wenzangu wengi ambao wamechangia walizungumzia suala hili la mwani. Ukulima wa mwani tunaufahamu ni mgumu sana lakini utaona biashara hii hadi leo haijapata bei ambayo ni muafaka inayoweza kuwasaidia wajasiriamali wetu wakaweza na wao kutokana na hali mbaya ya umaskini kutokana na biashara hii ama kilimo wanacholima kwa muda mrefu.

Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri kuhakikisha wanapata soko la kudumu na lenye uwezo wa kuweza kuwasaidia wananchi wetu, wakapata bei ambayo inafanana na kazi ambazo wanazifanya. Kwa muda mrefu sana wananchi wanahangaika kutafuta bei, lakini hata leo biashara hii utakuta haijaweza kufikia hata kilo moja wakaweza kuhakikisha wanapata hiyo kilo moja wanayouza wakapata nusu kilo ya mchele, wananchi wanaumia na kuhangaika sana.

Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri ahakikishe kwamba wananchi wanapata soko la nje pamoja na la ndani, ili waweze kufikia angalau kilo moja ya mwani iwe ni shilingi 2,000 mpaka 5,000. Kwa sababu mpaka leo kilo ya mwani haijaweza kuwakidhi wananchi angalau kuweza kufika bei ambayo inastahili.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mwani una faida nyingi sana, hasa kutengeneza virutubishi kwa ajili ya binadamu pamoja na wanyama, ambapo faida kubwa inategemea mwani. Utakuta mwani huo utashangaa kwamba kwa nini hauna bei hadi leo. Hapa sasa hivi utakuta chakula cha kuku bila ya mwani hakiwi chakula kizuri, utakuta virutubishi vingi vinatokana na mwani.

Kwa hivyo, mwani unafaida kubwa kwa binadamu ama wanyama, hivyo kwa nini isiwe bei yake inaridhisha kuweza kuwasaidia wananchi wetu, ambao wanahangaika sana kwa ajili ya ukulima wa mwani ambao unapatikana kwa ugumu sana.

Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri akija atueleze ni lini atalifuatilia suala hili, ama kulirejesha kwa Wawakilishi wenyewe waweze kwenda nje na kutafuta bei ya mwani kwa ajili ya wananchi wao. Siamini kutokana na mwani wenye faida zake ikawa bei yake iwe ndogo kiasi hiki. Kwa hivyo, hilo ni tatizo kubwa kwa ajili ya wananchi ambao wanahangaika kwa muda mwingi sana bila ya kupata faida ya mwani. Hivi sasa mara nyingi wanapata hasara kutokana na kwamba kazi wanayofanya ni kubwa, lakini faida wanayopata, ni ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende kwenye ukurasa wa 4 kuhusu sekta ya mifugo. Sekta hii hivi sasa imekuwa hapa nchini, hasa vijijini. Lakini utawakuta wananchi wanapata tabu sana kuhusu kufanikisha kuweza kufuga kwa usalama hao wanyama ambao wanafugwa, mbuzi pamoja na ng'ombe.

Mhe. Mwenyekiti, utakuta ng'ombe hana hatia, lakini kwa vile hakuna sehemu iliyotengwa na wizara kuweza kupata malisho, utakuta ng'ombe huyo ana matatizo amekuwa mlemavu kwa sababu hana hatia yoyote. Utamkuta ng'ombe amekatwa maskio yote mawili, kwa sababu ameingia katika shamba la mkulima, ama utakuta ng'ombe huyo amekatwa mkia wakati mkia ule ndio silaha yake ya kuweza kuhakikisha kwamba chofuo hawamuumizi mwili wake. Lakini utamuona ng'ombe yule amedhulumiwa kwa sababu hana mkia, inabidi hata akitafunwa na chofuo hana vya kujitetea anapiga teke la mguu, wakati chofuo anawindwa kwa mkia.

Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri ahakikishe kwamba anapata maeneo mazuri katika kila Mkoa, afuatilie na kuona kuna maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wafugaji, ili kuona ng'ombe wale hawapati hatia ambazo haziwahusu. Kwa sababu leo wewe unamchukua ng'ombe na kumkata mkia, ama unamkata masikio, tunaelewa upepo unavyovuma na kuingia kwenye maskio wakati yule ng'ombe alipangiwa maalum asipate matatizo na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, wizara ikiwa haitowapatia maeneo wafugaji basi itakuwa inafanya sio haki kuhusu wafugaji wetu.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akija atuambie ni lini ataweza kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wafugaji, ili kuona kwamba matatizo haya yanaondokana na wananchi wanapata yale ambayo yamepangwa na serikali. Serikali kwa kweli haikubali kuona ng'ombe wake wawe hawana mikia ama hawana masikio. Kwa sababu kulikuwa kuna mzungu mmoja, yeye akimkuta ng'ombe au punda anateswa, basi anamlipa yule ili aweze kuona yule mnyama hapati mateso.

Mhe. Mwenyekiti, nitashangaa kuona serikali inaachia tu na ng'ombe wanaendelea kupata matatizo na kwamba hakuna maeneo ambayo yametengwa.

Kwa hivyo, serikali yetu isifanye kosa kama hili, ione kwamba inapata maeneo ya kuhakikisha kwamba wanyama wetu wanastiriwa kama tunavyotaka mifugo iendelee nchini kwa faida ya wananchi, ili kuona tunapata vitoweo tulivyopangiwa kuliko kuona kila siku tunaagiza nyama kutoka nje. Hakuna sababu ya kwamba tusiwe na ng'ombe wetu wenyewe wa kututosheleza kuweza kupata vitoweo hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, lakini inatakiwa wizara ihakikishe inakakamaa sana kuona wafugaji wanapata haki yao ya kupata maeneo ya kulisha ng'ombe, ili kupata uhakika wa maisha ya ng'ombe wetu wanaishi kwa usalama.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika ukurasa namba 7 kuhusu sekta ya uvuvi. Mara kwa mara wananchi hukamatwa bahari kwa sababu ya kuvua katika maeneo ya kina kidogo cha maji. Hiyo inasababishwa na kuwa wananchi wanakwenda katika kina kidogo cha maji na hata zile nyavu wanazovulia ni zile ambazo hazihitajiki na wala hazitakiwi na serikali ili wavuwe. Hiyo ni sababu kwamba serikali haijafanya yale ambayo ameeleza muda mrefu kwamba watayatekeleza, ambapo serikali yetu imetenga pesa kwa muda mrefu, ili kuona tunapata meli za kisasa na kuondoa usumbufu huu kwa wananchi. Lakini hadi leo utakuta serikali bado haijatimiza ahadi zake kama kununua meli za uvuvi kwa ajili ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni muda mrefu sana mimi niko katika kamati hii, kulikuwa na pesa ambazo tulikwisha tenga kwa ajili ya kununua meli, lakini kila baada ya mwaka ukisha unakuta mnapigwa danadana kwamba meli ile sijaiona hata moja kufika hapa, ili tuona kuwa tumeshapata meli ya kileo kwa ajili ya uvuvi wa kileo ambayo inakwenda katika kina kikubwa cha maji.

Kwa hivyo, naishauri wizara kwa vile imemaliza miaka mitano bila ya kuweza kupata meli, basi wizara ifanye juhudi za makusudi, ili tuone kwamba angalau meli mbili zinapatikana kwa haraka kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016.
Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hivi sasa wizara itakuwa na deni kubwa sana kwa vijana ambao wanataka kupata uhakika wa ajira. Vijana wanategemea sana serikali yao na serikali ndio iliyochukua jukumu la kutaja kuwa ni lini au mwezi gani itaweza kupata meli.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe dakika tano za kumalizia.

Mhe. Mussa Ali Hassan: ...itapata meli ambazo wananchi wetu wataweza kupata ajira. Sasa utakuta kipindi chote ajira zimekuwa ngumu na serikali haijatoa tamko lolote kwamba hili suala litamalizika muda gani, ili kuweza kuwa na meli zetu za uvuvi. Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri akija atuambie kwamba ni lini tutaweza kupata meli kwa ajili ya faida ya wananchi pamoja na ajira za vijana wetu, ili kuona kwamba tatizo la umaskini kwa upande wa bahari limeondoka. Au wao ndio watakuwa na jukumu la kutowakamata wale wananchi wanaovua katika kina kidogo cha maji na wanatumia nyavu ndogo ambazo hazikubaliki. Wao ndio wahakikishe kwamba wananchi hawaendi kule kunakotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo ndio mchango wangu kwa hii leo, naweza kuiunga mkono kwa asilimia mia kama Mhe. Waziri atakuja kutoa tamko ni lini atahakikisha kwamba meli za uvuvi zimepatikana katika nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu wenu wakati wa majadiliano. Lakini ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe, wizara hii tunaikamilisha leo, hivyo tutapitisha vifungu jioni, hivyo ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe na Wajumbe wengine ambao wako nje wananisikia, ningewaomba waje, wanajua utaratibu wa kupitisha vifungu. Ikiwa hawatokuja ina maana tutashindwa kupitisha vifungu. Kwa hivyo, nawaomba sana wahudhurie ili tuweze kumaliza wizara hii leo.

Waheshimiwa Wajumbe, nimebakisha wachangiaji wawili, akiwemo Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ningemuomba sana aje mapema, na Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii na yeye atachangia baada ya hapo tutapata majumuisho kutoka kwa Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa leo tutaonana jioni saa 11:00 *Inshaallah*.

(Saa 7:00 mchana Kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa sote kuwa katika hali ya uzima na afya njema jioni hii.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri Abdillahi Jihad Hassan kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/16 kwa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wake mzuri wa ripoti yake, pia nawapongeza Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi yao nzuri wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme sekta hii ya Mifugo na Uvuvi ni kama uti wa mgongo wa nchi yetu kama ilivyo ile Wizara ya Kilimo, iliyokwisha jana. Basi sekta hii nayo ni muhimu sana katika haya mambo yake, ambayo yanaendeleza kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee katika ukurasa wa nne kifugu namba 2.1.1 mafanikio katika sekta ya mifugo, katika mwaka wa fedha 2014/2015, sekta ya mifugo imeweza kupata mafanikio mazuri. Mimi naipongeza sana Wizara kwa jitihada yake kubwa iliyoonesha hata kupata mafanikio mazuri.

Mhe. Mwenyekiti niendelee kwa kusema kuongeza idadi ya wafugaji hili ni jambo zuri na wafugaji wameshawishika kuendelea kufuga hawa wanyama, hasa kama ng'ombe, mbuzi na kuku wa kisasa. Hawa ukitizama takwimu zinaonesha kitabu chetu 2013 ilikuwa ni 46,000 hadi kufikia 47,058, mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Hii inaonesha kabisa kama Wizara inajitahidi sana kushajihisha watu kuweza kuongeza idadi kubwa ya wafugaji hao na hili ni jambo zuri na jambo jema kabisa. Mimi naipongeza sana Serikali pamoja na Wizara kwa juhudi zao walizozitumia.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wafugaji wetu na wavuvi wetu wanajitahidi sana kuweka hii mifugo yao katika hali nzuri na kuweza kuuza, lakini niseme kitu kimoja kinasikitisha sana; ukitizama hawa wafugaji wetu wanapata tabu wakishakufuga katika soko lao katika kuuza hawa wanyama, hasa kuku. Ukitizama wanakuwa wanapata usumbufu hasa katika mahoteli. Yule mfugaji mnyonge anahangaika kulea wale kuku karibu miezi sita, hata kuku wanakuwa wakubwa wa kuchinja au kuku wa nyama kwa kuliwa, lakini wanapopeleka mahoteli, ninaomba sana Serikali kupitia Wizara yetu hii, hawa mahoteli wasiwahangaishe kuwalipa bidhaa zao, wafugaji wetu.

Yule mnyonge masikini ya mungu anaweza kupeleka pale kuku wake mia moja au mia mbili, lakini anaambiwa pesa njoo baada ya wiki moja, baada ya wiki moja anakwenda anaambiwa bado subiri kwanza na kitu kinachosikitisha sana yule mfugaji anakuwa anakwenda pale kwenye hoteli kwanza anawekwa nje, anaambiwa subiri meneja hayupo, kwa kweli kama anakwenda kuomba pale.

Mimi naomba Wizara iangalie hili soko hasa hawa hoteli, wanaweza kuitwa wakafahamishwa jinsi ya wenzetu hawa wananchi wetu wanavyopata tabu, waangaliwe sana wasidhalilike kudai mapato yao. Inafika wakati mwengine mpaka mtu anakwenda polisi kudai mapato yake. Mfugaji yule kashahangaika miezi sita huku, anaambiwa pesa hamna yeye mwenyewe anataka kujiendesha na anataka kutumika, anashindwa kununua vyakula mwisho wake anafilisika.

Kwa hivyo mimi naomba sana, Wizara iangalie suala hili wafugaji wetu hawa walipwe kwa wakati wanaopeleka mazao yao na yule mwenye hoteli awe na uhakika wa kuwalipa asifanye mchezo wakati yeye anauza chakula pesa nyingi sana na anaingiza faida kwenye hoteli yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee niseme ongezeko kubwa la uzalishaji wa maziwa kutoka lita milioni 27,243,351 mwaka 2013 hadi kufikia lita karibu milioni 29 mwaka 2014 sawa na ongezeko la 8%. Mimi naipongeza Sana Wizara kwa juhudi zake hizi na tumeona hapa haya maziwa yameongezeka kutoka lita milioni 27 imeongezeka mpaka milioni 29 karibu ongezeko la lita milioni mbili kwa mwaka imeongeza.

Kwa kweli hii ni jitihada kubwa pamoja na Serikali, niipongeze na Mhe. Waziri Jihadi pia nimpongeze kwa juhudi zake alizotumia. Kusema kweli mtu ukweli umwambie, panapo maharibiko useme na panapo faida na ongezeko useme, kwa sababu kumpa moyo pia Mhe. Waziri afanye kazi kwa bidii zaidi kwa kuwasaidia wananchi wetu na Serikali pia.

Mhe. Mwenyekiti mimi niendelee katika suala hili la ongezeko la maziwa; tumepata kama milioni mbili kwa mwaka, hili ni jambo zuri, lakini ongezeko jengine la nyama ya ng'ombe kutoka tani 4,966 kwa mwaka 2013 hadi kufikia tani 5,155 kwa mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Hili jambo pia zuri na mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi zake alizofanya, hivi kwani ongezeko hili linaonesha kabisa hapa karibu tani elfu moja zimeongezeka za nyama. Hili jambo zuri na naamini kila mwaka inavyoendelea haya matunda tutayapata na maongezeko yatafanikiwa kwa ajili ya wananchi wetu na wafugaji wetu wafaidike katika mifugo yao.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na kuku kutoka nje pia niseme juu ya faida wanazozipata kwa wafugaji wetu lakini bado soko halitoshi, ukiangalia sasa hivi soko kubwa tunahitaji kuku mpaka kutoka nje ukiangalia mayai hivyo hivyo mpaka yanatoka nje kwa soko letu halitoshi. Japo wafugaji wetu wanajitahidi lakini bado soko halitoshi, sasa mimi nasema hapa hawa wafugaji wetu bado nyezo zao ndogo na bado wanataka kuwezeshwa zaidi, ili tuweze kumiliki lile soko hasa la ukweli.

Mimi inaniuma sana kusikia kuku wametoka nje wamekuja kuuzwa hapa wakati hawa wananchi wetu wanajitahidi kufuga lakini bado inakuwa haitoshelezi, sasa mimi nasema hebu Mheshimiwa Waziri nijibu kwa nini wanakuwa mpaka kuku watoke nje au kwa nini wafugaji wetu wasiweze kutosheleza soko lao la hapa, tatizo lao ni nini Mhe. Waziri ulizoziona wewe, hili uweze kunisaidia.

Pia tukiendelea mayai mengi sana yanatoka Dar es Salaam sasa hivi trea moja ya mayai tunakwenda sawa na elfu tano, lakini nafikiri kwenye kipindi hiki inafika mpaka shilingi elfu tisa au elfu nane mia tano.

Kwa hivyo naamini ongezeko linaloongezeka la watumiaji wakati wananchi wetu hawawezi kutosheleza hili soko, kwa kweli inasikitisha sana hali hii na mimi ningeomba sana Serikali iangalie sana kwa undani kabisa, kwa nini tushindwe kuzalisha wenyewe mayai na kuku hawa bila ya kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti mimi niseme sasa hivi hawa kuku wanaokuja wanaoitwa peduu wanauzwa elfu nne mia tano tu, kuku mkubwa kuku mzuri ukimtizama kanona kabisa, lakini hawa wafugaji wetu wanauza karibu elfu sita mpaka elfu saba kwa kuku yule yule. Lakini mimi nasema tu wananchi wetu hawajui, lakini kuku wanatoka nje kama Brazil au wanatoka nchi nyengine wanakuja mpaka hapa kwetu anachukua karibu miezi miwili kwenye meli kawekwa kwenye baridi, hata yule kuku mwenyewe ukimla hupati *test* ile yenyewe hasa.

Hawa kuku wanaoliwa hapa kwa kweli wana *test* nzuri na unafurahi hata ukila kile chakula, lakini mimi niseme kuna kipindi fulani mimi kule Canada, nilikaa muda mrefu na mara yangu ya kwanza nilikwenda *super market* nikaona kuku mkubwa tu anauzwa keshachinjwa kila kitu, dola moja haikufika senti 99, nikauliza kuku huyu mbona rahisi, nikaambiwa huyu kutoka nje na ameshakaa muda mrefu, kwa hivyo dola moja haikufika.

Kuku anatoka kwenye banda akachinjwa, yule unaweza kununua hata dola saba kule. Sasa tizama tofauti ya dola moja na dola saba lakini *test* tofauti ukitaka yule *chicken* mwenyewe hawa wanatoka kwenye banda *fresh* wanakuwa dola saba karibu shilingi elfu kumi kwa pesa zetu za Tanzania, lakini hawa wanaokaa kwenye mafriji, kwa kweli hata ukitizama kiafya sijui madhara yake.

Mhe. Waziri uangalie pia zaidi afya yake, inakuwaje kuku kutoka nje na kuku wanaofugwa hapa na ukitizama wananchi wetu wanakula hawajui madhara yake vipi. Hawa kuku wanapigwa mashindano mpaka wanapekiwa, wanakuja hapa hatujui madhara yake. Kwa kuwa wananchi wetu masikini wanahitaji kitu kilichokuwa rahisi, lakini hawajui madhara yake.

Kwa hivyo mimi naomba Mhe. Waziri muangalie suala hili la kuku wanaotoka nje kuja hapa kuuzwa na soko letu la hapa tuwawezeshe hawa wananchi wetu waweze kuwafanya huu ufugaji, ukawa mzuri haina haja kuweza kuagiza nje. Tungetumia soko hili la ndani ili kuweza kuwastawisha hawa wafugaji wetu, ili wawe katika hali nzuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee katika fursa hii wafugaji kupata mitaji kidogo. Fursa zao ni ndogo katika Serikali waangaliwe wanafaidika vipi hawa wafugaji wetu, ili waweze kupata fursa ya kujenga mabanda mazuri, kuweza kuwa na kuku wengi. Fursa hii ni ndogo, hasa ya mitaji au mikopo, kwa hivyo mimi nilikuwa

naomba sana Mhe. Waziri muangalie sana wafugaji wetu fursa zao waweze kupata vizuri kwa kujiendeleza.

Mimi nitoe mfano mdogo, ambacho hicho kitu mimi sijakifurahia nacho Mhe. Waziri, katika kitabu hiki nimeangalia kwa mfano mumeandika hawa mbwa kichaa wameingiziwa karibu milioni ishirini sawa na asilimia 80 ya pesa kwa ajili ya mbwa kichaa, ukiangalia mbwa kichaa na ukiangalia hawa wafugaji wetu wepi wana uzito zaidi.

Mimi nakumbuka zamani mbwa kichaa walikuwa wanapigwa risasi tu, wanapita polisi usiku wakiona mbwa wanampiga risasi kwa sababu yule mbwa ana madhara, anaweza kuwa kichaa ukamtibu, lakini anaweza akakutafuna akakutia madhara makubwa zaidi ikawa hata kujitibu kwenyewe huwezi na ukahatarisha maisha ya wananchi. Kwa hivyo mimi naangali mumeingiza milioni 20 wakati wananchi wetu wana shida ya kupata mitaji ya mikopo kwa ajili ya kuku wao na kuweza kuwawezesha zaidi. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri uangalie zaidi vizuri, kitu kilichombele sana kwa hawa wananchi wetu wafugaji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nije ukurasa wa nane; kwanza niipongeze sana Wizara pamoja na Serikali kwa juhudi yake kubwa inayofanya kwa kukamilika kwa ujenzi wa soko la samaki na mboga mboga la Tumbe Pemba. Hili ni wazo zuri na mimi nashukuru sana Serikali kuweza kulimaliza, nilipokwenda kipindi fulani lilikuwa halijamalizika. Kwa hivyo wananchi wataweza kutumia soko hili kwa ajili ya kuweka mazao yao, mifugo yao na kuuza vizuri katika soko lililokuwa la uhakika na kuwa usafi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa wa 21; kwa mwaka wa fedha 2014/15 Idara ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi milioni tisa yatokanayo na huduma za uzalishaji wa mifugo, hadi kufikia mwezi wa March, 2015 jumla ya shilingi 1,634,200 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 18 ya lengo lililowekwa. Lakini mimi niipongeze sana Serikali kwa kujitahidi na kuona suala hili ambalo wameweza kukusanya fedha hizi. Hili jambo jema na inaonesha wazi kama moyo huo upo na ufanyaji kazi pia unaendelea vizuri kabisa na Serikali kwa ujumla inajitahidi kutatua changamoto zilizokuwepo.

Nije katika Idara imeanza kulipa deni la matrekta ambayo walinunua kwa ajili ya kutayarisha malisho kwa ajili ya mifugo. Lakini nimuulize haya matrekta yako mangapi na yamegawiwa vipi kwa ajili ya kuwapa hawa wananchi wetu kwa ajili ya kuwajengea uwezo zaidi, kwa ajili ya mifugo yao na utayarishaji wa mashamba kwa ajili ya malisho yao. Na kama ulivyosema Serikali ina nia njema kabisa kusaidia wananchi wake na moja ishara hii ya kununua matrekta na tayari wameweza kulipa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie kwenye sekta hii ya uvuvi katika ukurasa wa 8; shughuli za uvuvi zimekua kutoka asilimia 3.6 kwa mwaka 2013 hadi asilimia 8.9 kwa mwaka 2014; hali hii inaonekana kuwa kuimarika kwa maeneo ya hifadhi, aidha mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la taifa imepungua kutoka 6.5 kwa mwaka 2013 hadi 6.4 mwaka 2014. Hii inaonesha wazi kabisa kama sekta ya uvuvi imepungua katika nchi yetu. Mafanikio yanapatikana, lakini kwa mwaka huu ukweli imeshuka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nije kwa pato la wavuvi wetu hawa wanaovua kwa kila siku kujipatia rizki zao katika ukurasa wa 7 kifungu namba 2.21 mafanikio katika Sekta ya Uvuvi. Kwa upande wa sekta ya uvuvi mafanikio yaliyopatikana uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka tani 30,712 mwaka 2013 zenye thamani ya Shs. 11,872,937 hadi tani 32,973 mwaka 2014 zenye thamani ya Shs. milioni 126. Hili jambo jema na nashukuru sana Serikali inaona hili na mafanikio yanapatikana katika sekta ya uvuvi nawapongeza sana Serikali kwa juhudi zake hizo na kwa kuweka kwenye bajeti hii kutuonesha jinsi gani wavuvi wetu wamnavyofaidika katika kupata fedha hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 5; katika utafiti nilioufanya bajeti ya mwaka jana 2014/15 Sekta ya uvuvi pato lake, wavuvi wetu ukitizama kitabu kile cha mwaka jana kuvuliwa kwa tani 41,952 za samaki kwa kipindi cha miezi sita tu...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiza dakika tano kumalizia.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Haya ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka ambao zimeingizia wavuvi jumla ya bilioni 53,460 kwa muda huo wa miezi tisa. Hii inaonesha sekta hii kwa taifa ukiangalia mwaka jana na mwaka huu, kwa kweli imeshuka. Mwaka jana tulikuwa tupo juu katika pato la wavuvi wetu.

Katika ukurasa wa 33; ukiangalia kifungu 4.1 kwa mwaka wa fedha 2014/15 Serikali imeweza kupata karibu milioni 613 kutokana na leseni za uvuvi wa bahari kuu na shilingi milioni 213 kutokana na mapato ya ndani ya Wizara ikiwemo ada ya leseni za uvuvi wa ndani, pia ada za wanyama na mazao baharini.

Hadi kufikia Machi, 2015 Wizara ilifikia lengo na kukusanya jumla ya shilingi milioni 571 sawa na asilimia 43. Mimi naipongeza sana Serikali kwa juhudi zake hizi kuweza kukusanya fedha hizi. Lakini niseme kuna matatizo ya wavuvi wetu. Ukiangalia uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi hasa ukitizama doria katika bandari zetu hizi; doria kwa wavuvi haramu kitu hicho kinakuwa tabu sana kuweza kuwakamata hawa.

Nikiangalia kwenye ukurasa wa 9 kukosekana kwa vifaranga vya samaki, ukiukwaji wa sheria za uvuvi, ongezeko la shindikizo la uvuvi katika maji madogo. Hili ni tatizo kubwa kwa wananchi wetu, haya matatizo yote yanasababishwa na hii doria iliyokuwa haiwezi kufanywa. Kuna wavuvi wanavua uvuvi haramu, wanahujumu uchumi wetu kwa kweli kwa kukamata hawa samaki wadogo wadogo, mwisho inakuwa shida hata kuwapata samaki wakubwa.

Kwa hivyo mimi naomba sana Mhe. Waziri uangalie sana uvuvi haramu na bado unafanyika katika nchi yetu, maeneo mbali mbali wanawatega samaki tena kwa uzio ule wanakuwa samaki wadogo wanawapata kweli. Inaumiza uchumi sana katika jamii yetu.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika ukurasa wa 10. namba 2.2.3 kuwawezesha wavuvi vijana kuvua katika kima kirefu cha maji makubwa haya. Niseme tu hawa vijana wetu kwa kweli wanaweza kuvua sana na wanajitahidi. Ukitizama kuvua maji marefu, kina kirefu kama hichi hawawezi kufika, hasa hawa vijana wa sasa hivi. Hawa vijana wa sasa hivi tofauti na wazee wetu wa zamani.

Mimi nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, baba angu mzazi keshawahi kunichukua baharini na alikuwa na ushawishi mkubwa, alikuwa anahamu mimi niwe mvuvi mzuri tu wa bahari. Lakini kwa kweli kazi ile imenishinda, mimi nilikuwa siwezi. Nikipanda kwenye boti na nikikaa muda mwingi naona kizunguzungu na nataka kutapika. Lakini kwa kweli naweza kusema wale wazee walikuwa na upewa mkubwa na Mungu kawajaalia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakumbuka tulikuwa tunakwenda baharini, tukifika anakwenda maji mengi ambayo huwoni huku huwoni huku. Ukifika kule baharini anakwambia tia nanga hapo. Ukitia nanga pale anakwambia hata tumeshafika Mwatima pengine. Hapo Mwatima utakuta kuna samaki anavua kama koana, tasi au changu, lakini wana alama zao, sijui wanajuwaje Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli Mungu kawapa uwezo mkubwa wazee wale.

Kwa hivyo, akitia nanga pale samaki atakaewavua pale watakuwa ni changu tu au atakuwa ni tasi tu. Ukitoka pale anakwambia twende sehemu nyengine kwenye mwamba wetu au kwenye sehemu yetu. Unakwenda na boti ya mashine ukifika pahali anakwambia tia nanga, ukitia nanga anakwambia hapa tumeshafika tuko Lanyuni sasa hapa. Lanyuni ukitia mshipi tu unavua samaki wa dizaini ile ile aliyesema yeye kama tasi au changu. Yaani wanajua kwa upeo mkubwa sana, hata sijui walikuwa wanatumia vigezo gani. Lakini vijana wetu wa sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, inakuwa tabu sana.

Mimi juzi nilikwenda pale Bandari yangu moja hapa jimboni kwangu Sharifumsa na Kibweni. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, wavuvi wale wapo wengi pale Kibweni. Lakini shida yao kubwa ilikuwa ni kupata lile banda lao la kupumzika, wakitoka baharini wanakuwa hawana pa kupumzika. Kilio chao kilikuwa kile, lakini kwa uwezo wake Mungu na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, nimeweza kuwajengea banda lile wale wavuvi wetu wa pale Kibweni. Nikawajengea banda lao dogo na sasa hivi wanalitumia kwa ajili ya kupumzika. Lakini kuna wavuvi wengi na ndio ajira kubwa kwa eneo la watu wa pale.

Pia, wiki iliyokwisha nilikwenda Bandari ya Sharifumsa wavuvi wapo wengi sana vijana wengi, lakini kilio chao kikubwa pia ni banda la kuwajengea wavuvi. Sasa Mhe. Waziri, nakuomba kama kunampango wowote wa kusaidia basi wa kujenga hilo banda, mimi niko tayari kutoa mchango kwa ajili ya hawa wavuvi wetu wa Bandari hii ya Sharifumsa tuwasaidie kupata banda lao. Ukenda kuangalia hali halisi utawaonea huruma pale, hawana pa kujifichia, wakitoka kazini wakirudi inakuwa pale juwa kali, saa nyengine inakuwa mvua wanashindwa kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, muda wako umekwisha malizia.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi namalizia lakini naomba sana serikali kwa ujumla kabisa. Zamani tulikuwa tuna duka moja la Fisharizi linauzwa vifaa vya mashine, zinauzwa mashine za boti, inauza mishipi ndowana, vyavu, lakini sasa hivi duka lile halipo sijui limekwenda wapi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana serikali iliangalie sana suala hili la kuweza kuwafungulia duka. Wizara naomba iwafungulie duka iwe bei nafuu kwa wananchi wetu ili waweze kupata ajira. Sekta hii ya Uvuvi imechukuwa vijana wengi na wanapata kipato chao kila siku cha kuweza kuendeshea maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tuweze kuwasaidia kwa kuwepo duka hili na liwe bei nafuu hasa kwa mashine. Ukiangalia wanapata tabu sana, hata kuuza samaki hawa, wengine wanatoka shamba. Wavuvi wetu hali zao zinakuwa ni duni, utamkuta mtu anatoka na baskeli shamba anatembea maili kumi au kumi tano, anakwenda kuuza samaki kwenye Mahoteli, akifika pale samaki kakauka. Mimi naomba sana wizara iangalie jinsi gani soko lao hawa wavuvi wetu wanaweza wakafikisha vizuri bidhaa zao bila ya kuwasumbua, ili kuwasaidia kupata usafiri hasa katika kupeleka samaki wao katika mahoteli. Mhe. Mwenyekiti, samaki akikaa muda mrefu kidogo anaharibika, kwa hivyo, nilikuwa naomba liangaliwe sana suala hili.

Baada ya hapo mimi naunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia. Mhe. Waziri, sina pingamizi nayo yoyote. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa muda wako.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa wema ulionifanyia wa muda huu, ili niweze nami kujibu angalau hoja za Waheshimiwa Wajumbe, waliokuwepo. Lakini hata waliokuwa hawapo nitaweza kuzijibu kwa manufaa ya wananchi wetu.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu ningeomba unipe angalau dakika mbili ili niseme chochote kwa sababu tu sina uhakika hata mmoja kuwa nitarudi katika Baraza lijalo au nitapata nafasi nyengine kama hii ya kusema.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini mpaka sasa na akanipa kazi hii muhimu. (*Makofi*)

Lakini la pili, nataka nimshukuru Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais. Lakini kwa aina ya kipekee, nimshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa mawazo yake na ushauri wake katika kutekeleza majukumu yake. Vile vile, nimshukuru Waziri wangu wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Jihad Abdillahi Hassan kwa mashirikiano makubwa anayonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Vile vile, nimshukuru Katibu Mkuu Dokta Kassim Gharib Juma, Dokta Omar Ali Amir, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Wakurugenzi wote kwa kunipa ushirikiano na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi zetu ziwe rahisi sana.

Vile vile, niendelee kuwashukuru wananchi wa jimbo la Mpendae kwa kuendelea kuniunga mkono na mimi tu nawambia nitajitahidi kadri ya uwezo wangu katika kipindi hichi nilichobaki. Lakini vile vile niwashukuru sana familia yangu kwa kuwa na subira wakati nikitekeleza majukumu yangu. Lakini mwisho kwa aina ya pekee niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili lako tukufu kwa kuweza kutupa ushirikiano mkubwa tangu mwanzo wa bajeti yetu mpaka leo tunahitimisha. Nawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, nianze hoja kwa mjumbe ambaye amemalizia hapa Mhe. Husein Ibrahim Makungu, Mwakilishi wa kudumu wa jimbo la Bububu kama ifuatavyo. Nataka niseme tu matrekta haya yapo na matrekta haya yapo sita ambayo nitayataja kwa mpangilio wake yaliopo.

Idadi ya Trekta	Mahali lilipo
1	Kisakasaka
1	kupandishia ng'ombe AI pale Maruhubi juu
1	Kituo cha Uzalishaji wa Majani Kizimbani
1	Chamanangwe Pemba
1	Shamba la Pangeni
1	Shamba la Karantini la Nziwengi
Jumla 6	

Matrekta haya yanafanyakazi kama yalivyotegemewa.

Lakini vile vile Mhe. Hussein, ameelezea suala la wafugaji hawa wa kuku kuweza kwenda wanapatiwa tabu na Mahoteli. Nataka niseme suala hili sio suala la Wizara kwa ujumla. Kwa sababu hii ni biashara huria iliyokuwepo na mapatano yao wanapatana wao wafugaji wenyewe pamoja na wafanyabiashara. Hivyo, tungewaomba tu wafugaji wetu wote wawe na tahadhari kubwa katika au waweke mikataba wanapokwenda kuuza katika mahoteli ili wasiweze kuhangaishwa. Nadhani siku hizi vyombo vya sheria vipo tele vya kuwahudumia. Sasa wanapokwenda waweke mikataba ya kudumu ili waone kisheria jinsi gani wanaweza wakafaidika.

Jambo jengine nilijibu kwa Mhe. Panya Ali Abdalla, yeye alitaka kujua wavuvi wa dagaa wa Nyanjale, wamepatiwa kiasi gani na wamefanyiwa nini. Nataka kusema yule muwekezaji wa pale amefanya mambo makubwa sana.

1) Amewapatia wavuvi wale gari la tani tatu,
2) Amewatengezea uwanja ule kwa kuanikia dagaa,
3) Amewatengezea soko,
4) Amewatengezea vyoo viwili, lakini isitoshe,
5) Amewasogezea maji katika eneo lao pale, jengine kubwa zaidi, na
6) Amewapa shilingi milioni 27 kwa ushirika wao wa pale.

Mambo mengine yatakuwa ni mambo ya kibinaadamu, lakini vile vile anaendelea muwezeshaji yule kuwa karibu sana na wale wananchi wa pale.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na hoja nyengine ya Mhe. Ashura Ali Sharif, Viti Maalum Kaskazini Unguja, yeye alitaka kujua mradi wa ajiwa kwa vijana, je, vijana wanapatiwa mbuzi au fedha taslim.

Nataka niseme tu mradi wa ajira kwa vijana umeanzishwa kwa lengo la kuwapatia vijana ajira. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Kaskazini na Kusini kwa Unguja na Wilaya ya Micheweni na Mkowani kwa Pemba. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mjumbe kama ifuatavyo.

Vijana hao walipatiwa jumla ya kuku kumi na mbuzi mmoja mmoja kwa kila mtu mmoja. Aidha, ilitoa mafunzo katika mfumo wa shamba darasa pamoja na wahusika kupatiwa dawa, chakula, mifugo na kuanzisha kuchangia gharama za ujenzi ya mabanda ambayo wanayafugia.

Alitaka kujua vijana hao walipatikana kwa njia gani.

Jibu: Ni kwamba vijana washiriki wa mradi huu walipatikana na kushirikiana na Wilaya kupitia Shehia ambazo huteuwa vijana wao waliokuwa na hamu ya kuweza kufuga. Mhe. Mwenyekiti, hapa nitasema kwamba waliokuwa na hamu kwa sababu sio kila moja tu ana hamu ya kufuga. Kila mtu ana hobi yake, lakini vijana waliopatikana hapa Shehia zilitizama jinsi gani za kuweza vijana wetu wanaohamu ya kufuga ndio waliopatiwa mradi huo.

Hoja ya tatu alitaka kusema Wizara inafanya utafiti wa wanyama wanaoingizwa Zanzibar na kupewa vikundi vya wafugaji kumiliki mazingira yale. Alitaka kujua, kwa sababu tunaingiza wanyama kutoka sehemu mbali mbali, je, pengine hali ya hewa wanaweza kudhibiti maradhi au vipi, lakini jibu ni kwamba.

Jibu: Uingizaji wa mifugo nchini unafanyika kwa kufuata taratibu zote za kiafya ambazo huthibitishwa na daktari wa Mifugo wa eneo la wananyama wanapotoka. Uzoefu tulionao ni kuwa wanyama wanaoletwa na hupewa vikundi wanatoka katika maeneo ambayo hali yake inalingana na hali ya Unguja. Utafiti unafanyika na unaonesha kuwa vifo vya uzalishaji inategemea na juhusi za mfugaji mwenyewe. Nilitembelea mara moja Pemba, nikamuona mfugaji mwenyewe hajaweka vizuri wale ng'ombe wake. Ng'ombe wamekonda lakini isitoshe na yeye mwenyewe wamemkondesha, kwa sababu hana umakini wa kufuga ng'ombe wale. Sasa hii tuiyone kwa karibu zaidi. Yule mfugaji mwenyewe awe na hamu kwanza ya kuweza kuwahudumia wale ng'ombe husika.

Hoja ya nne alitaka kujua serikali imejipangaje, kuiangalia bajeti ya Idara ya Mazao Baharini kati ya milioni 176 na imepatikana milioni 5 tu sawa na silimia 3.

Jibu: Kazi zilizopangwa ni shilingi milioni 176 zilihusiana na ujenzi wa kituo cha uzalishaji vifaranga vya samaki. Kazi hizo ni tathmini ya mazingira kulipa fidia mazao ya wananchi na kupeleka huduma za umeme, maji na mawasiliano. Kwa

kuwa ujenzi huo haujaanza kupitia Shirika la *KOICA*, ndio maana fedha hizo hazikuombwa.

Vile vile, hoja ya tano, alitaka kujua ili kupunguza tatizo la wataalamu wa Mifugo na Uvuvi, wizara inaendelezaje kitaalamu, wafanyakazi wake na kuwaajiri wataalamu wengine.

Jibu: Katika kupunguza tatizo hilo, wizara hivi sasa inaprogram maalum ya kuwasomesha vijana fani za mifugo na uvuvi, kwa kuanzia mwaka huu tulipeleka China vijana watano kusomea udaktari wa wanyana, vijana watatu wapo Chuo cha Uvuvi Mbegani wanaosoma kuhusu uvuvi wa bahari kuu. Aidha, Wizara inaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake katika ngazi mbali mbali ya cheti hadi Shahada hadi *PhD* katika fani mbali mbali.

Lakini hoja hii ilikuwa ina mnasaba sana na Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwahani. Yeye alitaka kujua wale vijana ambao wamepelekwa kule *SUWA* watano, mbona wamefeli kuna nini?

Nataka kusema vijana tulijitahidi sana na tuishukuru sana Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu iliwalipia kwa mwaka mzima na maposho yote walipatiwa na pale walipokuwa wanakwama basi Wizara au mtu binafsi hata mimi mwenyewe nilikuwa nikiwasaidia. Lakini bahati mbaya sana vijana wetu wamefeli vibaya na utaratibu tunaendelea labda tutafute vijana wengine wano hamu ya kuweza kwenda katika fani ya *VET medicine* kwa wale ambao watakaomaliza *form Six* mara hii.

Lakini hii nataka niseme Waheshimiwa Wawakilishi, kwenye Baraza lako hili Tukufu ni hasara kubwa sana ambayo tumeipata. Tunawaomba basi, Waheshimiwa Wawakilishi kama mpo na vijana ambao wana-*qualify* kuingia kwenye udaktari wa Mifugo (*VET medicine)* mtuletee ili tuone basi tunawasaidia vipi. Serikali ipo tayari kutoa *full sponsorship* kwa vijana ambao watachukua *VET medicine* na kuwahakikishia ajira yao watakaporudi. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Ashura, alitaka kujua tumezungukwa na bahari, je, kuna haja ya kufuga samaki wa maji baridi.
Haja ipo kwa sababu kupanga ni kuchagua. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ni mmoja katika wawekezaji wa samaki wa maji baridi na ana mabwawa yake mazuri, na sasa hivi anaendelea na ufugaji mzuri sana. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwa hatua yake ya kufuga samaki.

Hoja nyengine alitaka kujua kwa sasa samaki wanaovuliwa bahari Kuu hawajatosheleza mahitaji ya wananchi. Hivyo, ni ufugaji wa samaki wa maji ya

chumvi na maji ya baridi utasaidia kuongeza samaki ili kukidhi haja. Hili ndio jibu lake. Sasa lazima tukidhi haja ya sote sehemu mbili. Kuna wengine watapenda wanaovua maji ya chumvi lakini wengine wanatependa sana wale wa maji ya baridi na wapo wazuri tu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya saba ilikuwa Wizara kukusudia kusomesha vijana wangapi katika mafunzo ya kina kirefu cha maji. Wizara tayari imeshawasomesha vijana 50 na hii wenzetu Mamlaka ya Bahari Kuu ndio waliotusaidia. Wamesomeshwa 25 na sasa vijana wengine 25 wapo. Lakini bado tutaendelea na programu hii kila *time* itakavyoturuhusu, yaani bajeti itakavyoturuhusu tutawasomesha. Hii inaonesha hata Mhe. Hassan wa Kojani vijana wake watatu walikwenda kwenye programu hii. Mwaka jana aliililia sana programu hii. Lakini vile vile tumewachukua vijana hao na wanafanya kazi kwa pamoja na wanasoma sasa kwa bidii zote.

Hoja ya nane ilikuwa idadi gani ya serikali imeajiri katika sekta ya dagaa, watu wa Maruhubi wamepelekwa wapi. Serikali imetembelea sehemu ya kuanika dagaa na kuangalia huduma hizo. Hizi zote ni hoja ambazo zilikuwa zimetoka kwa Mhe. Ashura Sharif.

Jibu: Serikali haijaajiri watu kwenye shughuli za uwanikaji dagaa. Inatumia waajiri wake katika kuwapatia mafunzo ya ukaushaji wa dagaa lenye ubora na kutafuta takwimu na uwanikani wa dagaa. Watu walioajiriwa kwenye kuanika dagaa ni kama ifuatavyo:

Sehemu	**Idadi**
Maruhubi	2500
Mangapwani	2200
Fungu Refu	3000
Nyanjale	500
Potoa Bwekunduni	900.

Watu waliojishughulisha na uwanikaji wa dagaa waliopo Maruhubi watahamishwa eneo hilo la kuhama ambalo tayari limeshapimwa. Wizara ya Mifugo imetembelea sehemu zote zinazoshughulishwa na uwanikaji wa dagaa na kuangalia huduma muhimu. Kwa bahati mbaya huduma nyingi hazipatikani kwenye maeneo hayo. Hata hivyo mpango wa kuweka huduma hizo utasimamiwa na Halmashauri husika. Hii vile vile, wizara sasa imejipanga kama yale madiko yaliyoanzishwa hivi karibuni, kwenda kufanya kule basi kuona na zile kodi zinapatikana ili serikali iweze kupata kodi zinazohusiana na mambo hayo.

Jengine lilikuwa ni la Mhe. Fatma Said Mbarouk wa jimbo la Amani, mwakilishi wa wananchi kama ifuatavyo. Yeye alitaka kujua utafiti juu ya kiwango cha

samaki katika maeneo ya maji ya ndani unafanyika. Na ufatiliaje wa tathmini ya Matumbawe yaliyowekwa Chwaka na Maruhubi yale matumbawe ya *artificial*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema utafiti huu na kiwango cha samaki cha ufatiliaji wa tathmin ya matumbawe unafanyika kutokana na ufinyu wa bajeti unafanyika kidogo sana. Kazi zote hizi mbili zenye gharama kubwa na mara nyingi hufanyika pale serikali inapoona pana haja ya kufanya vile au kupata nguvu kutoka kwa wahisani.

Lakini jengine Mhe. Bikame Yussuf Hamad Mwakilishi wa Viti Maalum Kaskazini Pemba yeye alionyesha hoja kama ifuatavyo. Kwa nini wafugaji wa Kiuyu Mbuyuni wafanyiwe utafiti wa kufuga mbuzi badala ya kupewa taaluma.

Jibu: Wanakiuyu Mbuyuni hawafugi mbuzi kwa muda mrefu na sababu za msingi hazikueleweka. Wizara imeamua kufanya utafiti ili ieleweke iwapo zipo sababu zinazoletea wananchi kuwa na ufugaji wa mbuzi walio bora. Lengo la tafiti hizi ni kuwatafutia wananchi wa Kiuyu Mbuyuni shughuli nyengine za kiuchumi zaidi ya zile za uvuvi na ukulima wa mwani. Kwa sababu wakati wa bavua hawawezi kupata kitu chochote kilichokuwepo pale. Sasa Wizara tu ikaona kuwa ifanye mbinu mbadala kwa wale wafugaji wake ili ione basi manufaa yamepatikana na kupata kipato kilichokuwa bora na cha rahisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ilikuwa utoaji wa elimu ya usarifu wa mwani hasa katika Wilaya ya Micheweni. Jibu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa muda mrefu ilikuwa na kawaida yake ya kutoa taaluma mbali mbali zikiwemo usarifu wa mazao ya baharini. Ni kweli kwamba uzalishaji wa mwani Wilaya ya Micheweni inaongoza na taaluma ya usarifu wa mwani ni muhimu kwa uzalishaji huo. Wizara yangu itaendelea kutoa taaluma ili waweze kujiongezea tija inayotokana na mwani.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya tatu, ilikuwa je, ufugaji unafatilia kutoka Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Wizara hizi mbili pamoja zimeweza kuandaa mpango wa kusaidia, je, tunao kuku na ng'ombe wa kisasa kwa nini tusiendelee kubadilishana vinasaba kwa mifugo yetu ya kienyeji.

Jibu ni kwamba Wizara ikishirikiana na Wizara ya Uwezeshaji imewapatia mikopo wafugaji wetu, mikopo hii hutolewa kwa ushindani na masharti maalum wizara haijafikia lengo la kukusudiwa ambalo ni kuchanganya damu ya mifugo yetu kwa asilimia 20 na asilimia 30 tu ndio ibakie mifugo ya asili. Tukifikia hapo tutakuwa na mifugo yenye uzalishaji mkubwa na kujitosheleza bidhaa zetu za maziwa, nyama na mayai. Mhe. Mwenyekiti, hapa nimezungumzia nyama ya ng'ombe na mbuzi kwa sababu ndio tuliyoifanya hivyo.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, Jimbo la Mtambile naye alieleza mambo mengi lakini majibu yatakuwa kama ifuatavyo:

Uzalishaji wa nyama, kuku mwaka 2014 umepungua kwa asilimia 3 hii kutokana na wafugaji kuwa na hofu ya soko kutokana na kuwepo kwa nyama ya kuku kutoka nje ya nchi, suala hili ni changamoto kwetu. Hata hivyo tunaendelea kuhamasisha jamii kutumia bidhaa za mifugo zilizozalishwa nchini. Takwimu za uzalishaji wa nyama ya ng'ombe na mbuzi hizi nyama za ndani inatokana na Tanzania Bara kwa mwaka 2014 inazalishwa Zanzibar asilimia 32, asilimia 64 ni wanyama kutoka Tanzania Bara. Sasa naomba ieleweke tutakapozalisha sisi kwa wingi, tutapofuga sisi kwa wingi basi na uletaji wa kuku kutoka nje utapungua, lakini tusifuge kuku ambao sio bora. Sasa wizara yangu itaendelea kuwashajihisha wafugaji ili kuona basi hatua gani inafanyika lakini na kuku wale ambao tunawazalisha hapa nchini wawe na kiwango bora kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Mbwana wa Jimbo la Chambani Mwakilishi wa kudumu yeye alisema tu mambo yafuatayo:

Kwa nini Serikali imeshajihisha watu kufuga samaki kisha ikawatelekeza wafugaji hao. Nataka niseme tu Serikali haiwezi kuandaa jambo ikesha ikawatelekeza wananchi wake, nataka anisikilize makini sana hapa, Serikali kushindwa kuwaendeleza wafugaji wapya wa samaki si kwa sababu Serikali imewatelekeza bali ni kutokana na changamoto kubwa ya ukosefu wa vifaranga, changamoto ambayo hivi sasa Serikali inajitahidi kulingana na changamoto hiyo kwa ujenzi wa *hatchery* yenye lengo la kuzalisha vifaranga vya samaki, kaa na majongoo.

Nadhani nimezungumza mwanzo kama *hatchery* hii tayari tumeshatiliana saini na itajengwa katika eneo lile la Beit el Ras. Sasa ili kuwapatia vifaranga na vifaranga hivi vitakuwa vya samaki, kaa na majongoo ili wananchi wetu waweze kufaidika. Sasa hii ni jitihada ya Serikali kuona kwamba wale wafugaji wake wanafaidika na tuliiona changamoto hii sana tunapotembea kwa vifaranga. Lakini ningewaomba sana vifaranga hivi vya maji ya baridi wote wanaotaka vifaranga hivi wamuone Mhe. Mshimba, yeye anavyo vya kudumu na vingi zaidi. Lakini hivi vyengine wasubiri tu hatua itakapokuwa tayari basi tutajitahidi nao kugawa kadri ya uwezo unavyoruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja namba mbili ilikuwa Serikali ina mkakati gani kufanya vikundi vya ufugaji wa mazao ya baharini vinavyojitegemea zaidi. Nadhani Mhe. Mohammed Mbwana, yeye atakuwa shahidi tulipofanya ziara katika jimbo lake na kuona jitihada gani Serikali inavyokuwa pale na vikundi vingapi tuliwapa misaada mbali mbali ya kuweza kuvisaidia ili kuona wafugaji wetu wanapata mafunzo bora na wao wanapata tija katika ufugaji wao.

Hoja nyengine ya tatu, alitaka kujua mashirikiano gani yaliyoanzishwa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo ya Oman. Wizara ya Kilimo ya Mifugo ya Oman ina nia ya kusaidia Wizara ya Mifugo na Uvuvi Zanzibar katika maeneo yafuatayo:-

Kuwapatia mafunzo ya takwimu watendaji wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Uvuvi;

Kuanzisha *database* mfumo wa kisasa wa uchukuaji takwimu ili ziwe sahihi; na

Kuwapatia vifaa vya kuchukua takwimu kama mezani, *calculator* na kadhalika.

Haya ndio mashirikiano ambayo tunakwenda nayo na kuna wafanyakazi wetu tayari waliondoka kwenda Oman kwa *study tours*, nadhani wamerudi na hii ndio muendelezo wa mahusiano mema na Wizara hiyo ya huko.

Hoja nyengine ilikuwa hoja ya Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Mwakilishi wa Koani kama ifuatavyo:-

Yeye alikuwa na hoja tu kusema wafugaji wapatiwe maeneo maalum kwa ajili ya kufugia mifugo yao. Jibu, ninampongeza mjumbe kwa ushauri huo ambao wizara yangu inalielewa umuhimu wake, siwezi kuahidi ni lini wizara yangu itatekeleza kwa vile ni suala linalohitaji wadau tofauti, hivyo, ushauri umechukuliwa na tunasema tu Mhe. Mussa, ushauri wako Serikali itaufanyia kazi ili kuona basi wafugaji wanatengewa maeneo yao ili wapate basi ufugaji bora. Tutashauriana na wizara husika ya Upimaji na Ardhi ili kuona basi kama itaelekea na wadau mbali mbali na tunakuomba tu usichoke kutupa ushauri mbali mbali ili tuone basi ushauri wako tunaufanyia kazi kwa hatua kubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na niseme tu mambo ambayo mengine waliyokuwa hawajayasikia Mhe. Waziri, atakuja kujibu hapa na niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 moja.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho kuhusiana na michango yote ambayo wametoa Waheshimiwa Wajumbe, nianze kwa kusema kwamba, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha kwa mara nyengine tukiwa wazima na wenye afya nzuri. Pili, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa michango yenu, michango yote iliyotokewa ilikuwa na nia ya kunisaidia mimi pamoja na

watendaji wa wizara yangu katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na kufikia malengo ambayo tulijiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nichukue fursa hii nitoe shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, kwa ushauri nasaha na maelekezo waliotoa katika kuielekeza wizara yangu na watendaji wake ili kufikia malengo yetu ya kuwahudumia wafugaji, wavuvi na wakulima wa mwani, tunaahidi wizara yangu itafuata maelekezo ya kamati kwa kadri uwezo utapokua.

Mhe. Mwenyekiti, michango iliyotolewa na kamati hii ilijikita katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, ilikuwa ni kuimarisha Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kuangalia njia bora za kisasa ili kuongeza pato la wafugaji na wavuvi na wananchi kwa ujumla;

Lakini pili, kuimarisha Sekta ya Ufugaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa ili kukidhi mahitaji ya soko;

Tatu, ilikuwa kuandaa utaratibu mzuri utaosaidia kupatikana kwa takwimu sahihi;

Nne, ilikuwa kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wavuvi;

Tano, kutumiwa kwa eneo la Pangeni kwa ajili ya shughuli za ufugaji ili kuimarisha Sekta ya Ufugaji;

Sita, kuzungumza na muekezaji Bakhresa juu ya kuekeza katika ufugaji wa ng'ombe;

Saba, Wizara itoe kipa umbele usarifu wa maziwa;

Nane, kuimarisha upatikanaji wa chakula na lishe bora kwa mifugo;

Tisa, ilikuwa wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, iangalie namna ya kuongeza vianzio vya kukusanya mapato;

Kumi, kuchukua hatua ya kukabiliana na uzururaji ovyo wa mbwa;

Kumi na moja, kuhamasisha uekezaji katika uvuvi wa bahari kuu;

Kumi na mbili, kuzuia uvuvi haramu;

Kumi na tatu, kuimarisha doria; na

Kumi na nne, kuharakishwa suala la kuimarishwa uvuvi wa bahari kuu kwa kuwawezesha wananchi kwenda kuvua huko.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba ya wizara yangu ilichangiwa na jumla ya wajumbe 18 ambao wote walichangia moja kwa moja, naomba uniruhusu niwataje wale wote waliochangia hotuba hii nikianzia na waliochangia moja kwa moja kama ifuatavyo:-

1) Mhe. Amina Iddi Mabrouk
2) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3) Mhe. Hassan Hamad Omar
4) Mhe. Salim Abdalla
5) Mhe. Subeit Khamis Faki
6) Mhe. Saleh Nassor Juma
7) Mhe. Mohammedraza Hassanali
8) Mhe. Farida Amour Mohammed
9) Mhe. Hija Hassan Hija
10) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
11) Mhe. Ashura Shariff Ali
12) Mhe. Fatma Mbarouk Said
13) Mhe. Bikame Yussuf Hamad
14) Mhe. Mohammed Haji Khalid
15) Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
16) Mhe. Mussa Ali Hassan
17) Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
18) Mhe. Mohammed Said Dimwa ambaye ndie Naibu Waziri wangu wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba michango, maelekezo, maoni, ushauri na mapendekezo ambayo wameyatoa tutayafanyia kazi ipasavyo kwani yatatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ili kukidhi matakwa ya wadau wote wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu sasa naomba niainishe maeneo yaliyochangiwa kwa ujumla kama ifuatavyo:-
Eneo la kwanza, lilikuwa ni uhaba wa wataalam na vitendea kazi.

Eneo la pili, ilikuwa wananchi wa Pangeni kupatiwa eneo hilo.

La tatu, ilikuwa upandishaji wa ng'ombe kwa sindano.

La nne, ukiukwaji wa sheria za uvuvi na la mwisho ilikuwa

Uanikaji au ukaushaji wa madagaa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe pamoja na kuwasilisha majibu kwa hoja zilizotolewa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa, kwanza ambaye alitoa hoja hii alikuwa ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mwakilishi wa Jimbo la Kitope na yeye alikuwa na hoja kadhaa na hoja ya kwanza ilikuwa ombi la wananchi wa Pangeni wapatiwe eneo waliopanda miti yao.

Jawabu ni kwamba naungana mkono na yeye kuwaonea huruma wapiga kura wake na wananchi wetu, lakini ombi lake kwa ufupi ni kusema kwamba ni la muhali kwa sababu eneo la shamba la Pangeni ndio eneo pekee lililobakia kwa hivi sasa, hakuna maeneo mengine. Kwa hivyo, hili ni eneo ambalo tumelitenga mahsusi kwa ajili ya utafiti katika sekta ya mifugo ambao utekelezaji uko katika mpango mkakati wa wizara. Kwa hivyo, sijui nimwambie vipi lakini hilo ndio shamba ambalo peke yake lililobakia, mashamba yote takriban yamevamiwa, kwa hivyo, tukaona bora hili shamba la Pangeni basi tulitumie kwa masuala mazima ya utafiti.

Hoja yake ya pili Mhe. Mshimba, ilikuwa ufugaji wa samaki una tatizo la upatikanaji wa chakula cha samaki. Hili nimjibu tu kwamba kwa kweli tumefanya mafunzo mengi kwa ajili ya wafugaji wetu namna gani ya kutengeneza chakula cha samaki. Kwa hivyo, mafunzo hayo ni endelevu na yanaendelea kutolewa ili wafugaji waweze kutengeneza chakula cha samaki chenyewe ambacho chenye ubora. Kwa hivyo, mafunzo yametolewa ya kutosha, kwa hivyo, ninafikiri hakuna haja zaidi isipokuwa ni hiyo taaluma ambayo tumetoa kwa wafugaji ili wajitengenezee chakula chao wenyewe. Aidha, wizara inahamasisha wawekezaji katika kutengeneza chakula cha samaki ili wafugaji waweze kujitengenezea chakula cha samaki ambacho chenye ubora.

Hoja yake ya tatu, ilikuwa suala la mashamba darasa yapo anauliza. Mashamba darasa yapo na moja liko Jozani kwa hapa Unguja na kwa Pemba ni Pujini na pengine lako vile vile kwa jinsi tulivyoliona huenda baadae likawa ni shamba darasa kwa sababu tumeona linakaribia vile viwango ambavyo tumejiwekea, hongera sana.

Hoja yake ya nne, ilikuwa wizara itawasaidiaje waanikaji madagaa wakati wa mvua. Jibu ni kwamba tayari tumeshatoa mafunzo hayo, Wizara imetoa vifaa na mafunzo ya uanikiaji wa madagaa kwa kutumia chanja. Chanja hizo zinaweza kutumika hata wakati wa mvua bila ya dagaa hilo kuharibika kwani zimewekewa plastik maalum ambazo zinazuia mvua na vile vile kutoa joto ambalo linafanya dagaa hili liweze kuishi muda mrefu na liweze kuuzika. Kwa hivyo, Mhe. Mshimba, usiwe na wasiwasi tayari tumeshatoa vifaa hivyo kwa ajili ya waanika madagaa wetu. Vile vile, ni kwamba kwa kuanzia chanja hizo zimejengwa Maruhubi tayari zipo na Mangapwani.

Hoja yake ya tano, Kanuni za kusimamia maeneo ya hifadhi zimeongeza ada ya maeneo ya hifadhi bila ya kuongeza huduma. Kwa kweli napenda tu labda kukufahamisha Mhe. Mwakilishi, kwamba lengo la kuanzisha kitengo cha hifadhi ni kutekeleza matakwa ya sheria ya Uvuvi Nam. 7 ya mwaka 2010. Aidha, Kanuni hizo zimetungwa ili kuimarisha usimamizi wa maeneo hayo ya hifadhi. Kanuni hizo zimefanywa kwa mashauriano na wadau wote wakiwemo ya sekta ya utalii vile vile tumewashirikisha.

Kuongeza ada maeneo ya hifadhi ni kusaidia upatikanaji wa fedha ambazo zitasaidia kuimarisha huduma za uhifadhi, utafiti, ufatiliaji wa raslimali, mafunzo pamoja na doria yenyewe.

Mjumbe mwengine alikuwa ni Hassan Hamad Omar wa Jimbo la Kojani, ambaye hayupo lakini hata hivyo tutatoa majibu yake anasema unapozuia matumizi ya nyavu za macho madogo, je, dagaa la shungishungi watavuliwa vipi au ni kosa kuvua dagaa. Jawabu ni kwamba matumizi ya nyavu za macho madogo yamezuiliwa katika maeneo maalum, sio yote, ambayo yanajumuisha maeneo ya maji ya ndani, mafungu, matumbawe na maeneo ya hifadhi, hivyo, uvuvi wa dagaa unaruhusika katika maeneo yasiyokuwa hai.

Pia, ikumbukwe kwamba kupatikana kwa samaki wakubwa ni lazima kuwe na madagaa kwa sababu wao samaki wakubwa chakula chao kikubwa ni madagaa. Kwa hivyo, hatuwezi kuzuia kila eneo kwamba lisivuliwe hapana. Kuna maeneo maalum ambayo unaweza ukavua madagaa ili kuvutia samaki wakubwa. Pia, ikumbukwe kwamba hali hii inategemea kuwepo kwa dagaa baharini kwani hutumika kuwa ni chakula cha samaki wakubwa kama nilivyoeleza awali, unapomaliza dagaa uhamasishaji samaki wakubwa baharini. Kwa hivyo, unapokuwa na dagaa bila shaka samaki wakubwa baharini ndipo inakuwa ni kivutio kikubwa kwao.

Hoja yake ya pili tusidhibiti shughuli zas uvuvi. Jawabu ni kwamba kudhibiti sio kuzuia shughuli za uvuvi zisifanyike, lakini tudhibiti shughuli za uvuvi,

tusipodhibiti shughuli za uvuvi watu watavua kwa kutumia njia za uvuvi haramu na kuharibu mazingira ya bahari, hivyo, kupunguza raslimali za samaki baharini na kipato cha wavuvi.

Hoja yake ya tatu, wanafunzi waliorudi China hawatumiwi ipasavyo. Jawabu ni kwamba wanafunzi wanatumiwa ipasavyo, wanafunzi hao walitolewa katika vikundi vya ufugaji na wanaendelea kutoa taaluma katika vikundi vyao na vikundi vya jirani.

Mjumbe mwengine alikuwa Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Wawi na yeye alikuwa na hoja kadhaa, Serikali ina mpango gani ili kuimarisha ku-*stabilize* bei ya mazao ya baharini, bila kujali bamvua. Naye tulimjibu kama ifuatavyo kwamba kupitia mpango wa kuendeleza uvuvi wa bahari kuu unaoandaliwa na serikali hivi sasa, serikali itajenga vyumba vya kuhifadhia samaki (*cold rooms*) na sehemu za kutengenezea barafu za chenga pamoja na vinoo vya barafu ili kuepuka upotevu wa samaki wanaovuliwa baharini.

Hoja yake ya pili ilikuwa kuimarishwa kwa wanaanikaji wa dagaa maeneo ambayo wameyaoea, hoja hii pia ilichangiwa na Mhe. Ashura Sharif Ali wa Viti Maalum na jawabu ni kwamba waanikaji madagaa kwenye maeneo ambayo hayakupimwa na serikali imepanga kuyatumia maeneo hayo kwa shguhuli nyengine. Wajasiriamali hao sasa wametengewa maeneo mengine huko Kama ambayo kwa sasa serikali imeshapima eneo hilo kwa kazi hiyo peke yake.

Eneo la Maruhubi lilipimwa kwa ajili ya kupanua eneo la bandari ya Mpigaduri, waanikaji wa Maruhubi wamepewa muda wa kutosha kujiandaa na zoezi la kuhama kwenda huko Kama.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yake ya tatu matumizi ya vijiti kwa kupalia mwani yanachangia ukataji wa miti, je, hakuna mbadala wa kutumia vijiti? Mbadala wa matumizi wa vijiti umeanza kutumika wakulima wa eneo la Ng'ambwa Unguja Ukuu wameanza kutumia na mawe na mipira (*rubber band*) kupanda mwani. Matumizi ya kamba, nanga na maboya yameanza kutumika zoezi hili limeanza huko Jambiani. Matumizi ya mawe na kamba yameanza kutumika katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Hoja yake ya nne, lini serikali itaanzisha viwanda vya kusarifu minofu ya samaki, hoja hii pia ilichangiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Muyuni. Jawabu ni kwamba kupitia mpango wa kuendeleza uvuvi wa bahari kuu unaoandaliwa na serikali hivi sasa, serikali itajenga viwanda vya kusarifu samaki.

Hoja ya tano, serikali itachukua jitihada gani za kukinga maradhi ya mifugo Vitongoji (*Deep litter system)* husababisha maradhi ya ndui, kwa nini serikali haishajihishi ufugaji wa *battery cages* kwa njia ya mkopo. Na hoja nyengine matumizi ya gobore kwa kuwadhibiti mbwa wadhururaji.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imefanya kila jitihada za kupambana na maradhi ya mifugo kwa kuendeleza kinga na tiba ya mifugo. Vile vile, elimu ya ugani imeendelezwa ili wafugaji wazidi kuwa na mwamko juu ya namna bora ya ufugaji wa kisasa. *Deep litter system* haisababishi maradhi ya ndui, wafugaji wanashauriwa kufuata maelekezo ya wataalamu ili waepukane na athari za maradhi ya ndui. *Battery Cages System* husababisha udhalilishaji wa wanyama kwa kuwaweka kwenye sehemu ndogo kwa umri wao wote, hii ni kwenda kinyume na Sheria za haki za wanyama ambazo nchi yetu imeridhia.

Matumizi ya gobore kwa kuuliwa mbwa haikubaliki kimataifa kwa sababu ni kuwafanyia ukatili wa wanyama.

Mjumbe mwengine alikuwa ni Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni, nae alikuwa na hoja kadhaa, kwanza ufugaji wa samaki wizara imesaidia vifaranga vingapi?

Jawabu ni kwamba wizara imesaidia wafugaji wa samaki jumla ya vifaranga 23,724 kati ya hivyo, vifaranga 4892 vimetolewa Unguja na vifaranga 14,832 vimetolewa kwa Pemba.

Hoja yake ya pili, serikali isaidie kutafute soko la mwani, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane na Wizara ya Biashara ili kupata soko hilo.

Jawabu ni kwamba serikali inalifanyia kazi suala hilo la soko la mwani. Wizara ya Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea na utafiti na maamuzi ya mwani ndani ya nchi kwa kupata mbolea ili kupata soko la ndani badala ya kutegemea soko la nje pekee. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Duniani (*FAO)* inafanya utafiti ili kuongeza thamani ya soko la mwani.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yake ya tatu, kwa nini soko la Tumbe haliendeshwi na Halmashauri peke yake.

Jawabu ni kwamba ni kweli soko la Tumbe limepangiwa kuendeshwa kwa utatu, yaani Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, Kamati ya Uwiani Peka, Kamati ya Jumuiya ya Maendeleo ya Tumbe Mashariki na Magharibi. Hii ni kwa sababu serikali itapata mapato yake kupitia Halmashauri, lakini wavuvi wa maeneo hayo

na wao watapata mapato yao ili kuweza kufanikisha shughuli za uvuvi katika maeneo yao kwa vile wao wametoa mchango mkubwa katika mapato hayo ya uvuvi. Na hii ndio maana hawakupewa Halmashauri ya Wilaya peke yao na mapato yatachangiwa au yatagaiwa kwa utaratibu maalum, yaani asilimia yake maalum.

Hoja yake ya nne, majosho ya ng'ombe Wilaya ya Micheweni ina majosho mawili ambayo yamejengwa kutokana na wingi wa mifugo katika maeneo hayo. Wizara kwa sasa haina mpango wa kujenga majosho mapya kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, huduma za uogeshaji wa mifugo hupatikana kwa kutumia mabomba, sindano au dawa za kupe za kunyunyiza migongoni (*sputum)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Jimbo la Mtambwe nae alikuwa na hoja kadhaa, takwimu za uzalishaji wa samaki inaonesha kuongeza samaki wakati wenye mabwawa ya kufugia samaki wamekata tamaa na kupungua.

Hoja yake ya pili. vifaranga vya samaki vitazalishwa vya maji baridi au maji chumvi. Ya tatu. kutofikiwa malengo ya upandishaji ng'ombe kwa sindano, kupungua uzalishaji wa gesi ya *liquid nitrogen* na mtambo wa *bio gas*. Na mwisho, ilikuwa kuboresha uzalishaji wa mifugo ya kienyeji kwa kubadilisha vinasaba.

Jawabu ni kwamba…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, nakupa dakika kama saba umalizie.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Nakupa dakika saba umalizie hotuba yako.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Sawa wacha nimalize kumjibu Mhe. Salim Abdalla wa Jimbo la Mtambwe.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu za uzalishaji wa samaki zilizotolewa katika kitabu ni za samaki waliovuliwa baharini na sio wale wa kufuga. Aidha, samaki wa kufuga wamevunwa jumla ya tani 7, tani 5 Pemba na tani 2 Unguja. Vifaranga vitakavyozalishwa Beit el Rais kwa kuanzia ni vya maji ya chumvi. Aidha, baadae itaangaliwa uwezekano wa vifaranga vya maji baridi.

Malengo yaliwekwa ni ya mwaka lakini utekelezaji ulioripotiwa ni wa kipindi cha miezi tisa tu, hivyo, utaonesha upungufu wa takwimu. Zoezi hili linatekelezwa kwa kuchanganywa damu ya mifugo yetu ya kienyeji na ya kisasa kwa mifugo ya ng'ombe, mbuzi, mbwa na kuku.

Hoja yake ya pili, kwa nini mwelekeo ni kuwawezesha wavuvi vijana tu kuvua katika kina kirefu cha maji.

Jawabu ni kwamba napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi, kwamba msisitizo mkubwa umeelekezwa kwa vijana kuwawezesha kuvua kina kirefu cha maji ni pamoja na ukweli kwamba idadi ya wavuvi vijana imeongezeka kwa kasi na pia uvuvi katika eneo hilo unahitaji utaalamu na elimu ili kuvua katika eneo hilo. Wavuvi wanaopewa kipaumbele ni mpaka wale wenye umri wa miaka 40 na ambao wanaonesha kuwa na hamu ya kutaka kujiendeleza kujihusisha na uvuvi wa bahari kuu.

Vile vile, uvuvi katika eneo la bahari kuu unahitaji kujifunza fani nyengine muhimu za bahari ambapo vijana wenye elimu ndio wanaoweza kufahamu haraka fani hiyo.

Hoja yake ya tatu, kwa nini shughuli za uvuvi zinaongezeka kwa asilimia 3.6 mpaka 8.9 wakati mchango wa uvuvi katika pato la Taifa umeshuka kutoka asilimia 6.5 hadi asilimia 6.4.

Jibu ni kwamba, pato la Taifa linachangiwa na sekta nyingi ambazo katika kipindi cha mwaka 2013/2014 ongezeko lao ni kubwa zaidi kuliko ongezeko la sekta ya uvuvi.

Hoja yake ya nne, kwa nini vijiji vya Chwaka na Marumbi tu viwe ni vya mfano kwa mambo ya uvuvi.

Jawabu ni kwamba, vijiji hivi vimepakana na vina uhaba wa rasilimali ya samaki, jambo hili linasababisha wavuvi kuvua kwa kutumia nyavu na kuharibu mazingira ya bahari na eneo lao. Kutokana na hilo, serikali imeagiza kutengeneza mpango maalum wa kuviendeleza vijiji hivi kwa vijiji vya uvuvi vya mfano.

Mhe. Farida Amour Mohammed Viti Maalum na yeye anasema muda gani na lini ujenzi wa kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki utakuwa tayari. Kwa muda huu Shirika la *KOICA* la Korea kwa kushirikiana na *FAO* wanaendelea na utafiti wa awali kabla ya kuanza ujenzi. Ujumbe wa wataalamu huo utafika Zanzibar na kukutana na wadau wa sekta wa mazao ya baharini Jumatatu tarehe 15/06/2015. Baada ya hapo kwa sababu ya muda, naomba kutoa hoja. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ametoa hoja sasa niwaulize Waheshimiwa Wajumbe waliokubaliana na hiyo hoja wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi na kupitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU M01 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 03 Idara ya Mazao Baharini	Shs.150,000,000
Kifungu 04 Idara ya Uzalishaji Wanyama	Shs. 20,000,000
Kifungu 05 Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo	Shs.100,000,000
Kifungu 06 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi	Shs.686,362,000
Jumla Kuu:	**Shs.956,362,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU M01 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

KIFUNGU P01 PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

Kifungu S01 Uzalishaji wa Mifugo	Shs.1,050,259,000
Kifungu S02	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, namsikiliza tokea mapema lakini alijibu hoja moja tu, lakini nafikiri kutokana na muda wala siwezi kumlaumu kwa hilo, sasa nije katika huduma za utibabu wa mifugo, hili suala nililipigia kelele kabla ya bajeti humu ndani, niliuliza suala madaktari hasa Jimbo la Muyuni wakipata huduma kutoka Muungoni kufata Fuoni na kutoka Muungoni kwenda Makunduchi. Nimeishauri serikali wamtafutie usafiri angalau daktkari wa mifugo aweze kutembelea kwa wiki mara mbili, anasemaje Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nimesikia hoja ya Mjumbe na kwa sababu ni kama ushauri, kwa hivyo, sisi tutalichukua hilo

na yeye mwenyewe aliahidi kwamba atatoa nyumba, kwa hivyo, na hilo suala la usafiri tutalitekeleza kama alivyotaka mwenyewe. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sikumwambia kama nimeahidi nyumba, nimesema nitatoa kiwanja, sasa anasemaje yeye atajenga?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakumbuka ulisema nyumba au tukachukue *Hansard*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Niko tayari kwenda kufatilia *Hansard* Mhe. Waziri. (*Kicheko*)

Kifungu S02 Huduma za Utatibu wa Mifugo Shs. 883,354,000

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, tumeshapitisha umechelewa, tayari tunakwenda kwenye jumla ya fungu, kimeshapita kifungu. Kwa hiyo, tunaendelea.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad:...

(*Mjumbe hakutumia kipaza sauti*)

Mhe. Mwenyekiti: Tuko kwenye jumla ya kifungu Mheshimiwa…

Mhe. Bikame Yussuf Hamad:...

(*Mjumbe hakutumia kipaza sauti*)

Mhe. Mwenyekiti: Umechelewa Mheshimiwa basi hujafika.

Jumla ya Kifungu: **Shs.1,933,613,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kama hukuwa *sharp* kama hivi unaweza kuja kuanguka chini na utasema mtu ameshapotea njia. Kuimarisha kilimo cha shughuli za mwani Zanzibar. Mheshimiwa, kama kuna watu wanyonge na dhalili wanaopata shida ni wakulima wa mwani, ni kwa pesa hizi zilizotengwa milioni 10,999,000, *we are not serious*, Mhe. Waziri, aweze kulifikiria fungu hili.

Mhe. Rais ameagiza wizara nne zikae; Wizara ya Biashara, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na hii iliyokuwepo leo ili kuwatumia wananchi. Kwanza niendelee kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa jitihada kubwa anazozifanya kwa wananchi, ameagiza na leo ni bajeti yetu hii, wengine pengine ndio ya mwisho, nataka maelezo ya kina ambayo yanaweza kuridhisha kwa bajeti hii ya milioni 10 haikidhi hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku, lakini kwa utaratibu ungesubiri mpaka kifungu kikatajwa, hujakisubiri kifungu kutajwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ukija kufika unasema tushapita, sasa tukamate wapi sisi.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru, kwa kweli naelewa nini *concern* ya Mhe. Jaku, lakini hili suala nimelieleza hapa kwamba kwa kweli hivi sasa tunakaa na Wizara ya Biashara ili kulifikiria hili suala, sio kwamba hili suala hatulioni. Tunaliona lakini linahitaji muda, linahitaji utafiti kukaa na wawekezaji ili kuona kwamba hawa wakulima wetu wa mwani wanapata tija katika hili zao lao. Sio kwamba hatuyafanyi nimeeleza hapa kwamba tutashirikiana na Wizara ya Biashara na tayari tumeshazungumza kuhusu suala hili ili kuona bei nzuri ya wakulima wa mwani na uwezeshaji pamoja nimekumbushwa hapa. Kwa hivyo, Mhe. Jaku, nakuomba uwe na subra. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, subira ina mpaka wake na kusubiri kuna mwisho wake, hili suala ni la muda mrefu na Mhe. Rais tangu aagize haipungui karibu mwaka hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kwa kikao hiki. Sasa Mhe. Waziri, mimi nia yangu ni kutaka kumsaidia yeye na wananchi wetu, hebu alifikirie fungu hili angalau kuliongeza, ameniomba na mimi nimuombe, wananchi wetu wanyonge wanaumia hasa maeneo tunayoongoza sisi huku na huu uongozi wetu unatokana na dhamana, kama hatukuja kuwatetea hapa kwa shilingi milioni kumi hizi, hatuko *serious* kabisa. Sisi tuna jukumu kwa wananchi, leo mwani umeharibika kule Jambiani huwezi kuamini, kazi yenyewe ya kutwa nzima.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, tumekuelewa, sasa unataka nini?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi nataka kifungu kiongezwe tu basi, kutoka shilingi milioni kumi angalau iwe mara mbili shilingi milioni thalathini ifike hatua hiyo, pesa hizi ni kidogo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Jaku Hashim, lakini akumbuke tu kwamba haya mambo yanakwenda hatua baada ya

hatua. Nafikiri ameshuhudia jinsi nilivyoshirikiana na wakulima wa mwani kwamba tayari wameshapewa vihori, sasa tunaelekea katika hatua hiyo nyengine ambayo ni muhimu sana. Kwa hivyo, awe na subira. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi wala sitaki kuonesha ubabe wala umwamba, lakini anayebebwa naye hujikaza. Mhe. Mwenyekiti, hebu nisaidie kweli shilingi milioni kumi hizi tunawafanyia haki wananchi kweli? Hebu tuangalieni binadamu shilingi milioni kumi zitawafanyia haki kweli wananchi angalau zizidishwe kidogo atafute kifungu chengine azidishe. Rais kaagiza na wizara nne zimekaa kuwafikiria wananchi hawa, wizara nne zinaagizwa na Mhe. Rais sio maneno yangu mimi, leo shilingi milioni kumi tunawafanyia haki kweli, hebu tupime wananchi wanatusikia.

Mimi nimuombe Mhe. Waziri kwa heshima na taadhima kabisa ya hali ya juu azidishe kifungu hiki, atafute pahali kuongeza fungu hili. Nimuombe sana Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, mimi namfahamu sana Mhe. Jaku Hashim, tunatamani sana kuongeza hilo lakini hii mantiki ya kushirikiana wizara hizi tatu ni kwa sababgu hiyo. Kwa sababu sisi bajeti yenu mnaielewa, kwa hivyo, hii maana ya kushirikiana na uwezeshaji ni kwa sababu ya hiyo kuwaongezea hawa wananchi kuwapunguzia makali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim, turuhusu tuendelee Mhe. Waziri, amekufahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo kuna wataalamu wananishauri na kufikiria kwenye kichaa cha mbwa kuna pesa nyingi sana zimewekwa, hebu zipunguzwe huko kwenye kichaa cha mbwa shilingi milioni mia moja arobaini na saba karibu, zipunguzwe.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Pesa zile kwa kweli ni za wahisani, kwa hivyo, hatuwezi tukazipunguza tukazipeleka huko, namuomba Mhe. Jaku Hashim, atuamini tutashirikiana na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ili kuona suala hili linamalizika, zile ni pesa za wahisani hatuwezi kufanya hilo. Nakuomba Mhe. Jaku Hashim, niamini na uridhike, nakuomba kwa hisani yako tumalize hili suala. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali lakini nakuombeni, nitamuomba kwa kumpima yeye kweli atakuwa tayari kunisaidia? Tupitishe.

KIFUNGU P02 MAENDELEO YA UVUVI

Kifungu S01 Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini Shs. 882,710,000

Kifungu S02

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, sasa hapa nitamtizama Mhe. Waziri, kweli ana nia ya kusaidiwa na mimi anisaidie? Chombo hiki hiki *Hansard* zipo niliahidiwa boti kwa wananchi wa Jimbo la Muyuni, vimeshakaa vikao vinne kwamba kuna harufu nzuri inakuja na sasa hivi ishakuwa harufu mbaya, si nzuri tena. Kwa hiyo, hapa nitahitaji msaada wake nipate maelezo ya kina kuhusu boti ya wananchi wa Jimbo la Muyuni, kikao cha nne hiki napiga wimbo huu wa Taifa mpaka leo, wananchi wenyewe wananisikia kule. Halafu walikuwa na kilio cha banda.

Mhe. Mwenyekiti, kama hoja nyengine ya pili kuwekwa hapo hapo kuhusu soko la Malindi. Mwaka jana ilikuwa *issue* humu kuhusu Mji Mkongwe walizuia eneo lile. Eneo lile ni hatarishi kwa usalama wa wananchi wa visiwa hivi kwa namna samaki wanavyouzwa. Pana mradi wa msaada wa Japani, ujenzi ule umefikia wapi Mhe. Waziri, hoja zangu ni mbili. Ujenzi wa soko la Malindi la samaki na hoja ya boti ya wavuvi ya watu wa Muyuni. Mhe. Waziri, nafikiri amenielewa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Kuhusiana na suala la boti kweli lakini namuomba Mhe. Mwakilishi kwamba awe na subira, kama tulivyoeleza kwamba tayari kutakuwa na Mradi wa *SWIOfish* ambao tutazindua karibuni hivi ambao mantiki moja ni hiyo kugawa maboti. Lakini vile vile tayari tumeshatiliana saini utakapoanzishwa uvuvi wa bahari kuu ambao tayari watakuwa na vituo maalum katika kila kona ya Unguja ili kuwakopesha maboti wananchi wetu ili wavue na halafu baadae watakuwa wanauza samaki kwa ile kampuni. Kwa hivyo, moja katika mikakati yetu ni kulifikiria hilo suala la Mhe. Jaku Hashim, kijiji cha Muyuni nacho vile vile kiwemo ndani ya mikakati hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim, elewa kwamba umo ndani ya mkakati huu.

Suala la soko la Malindi nalo vile vile liko njiani halina muda mrefu, tayari Rais ameshatoa *go ahead*, kwa hivyo, wakati wowote litaanza ujenzi wake. Nakushukuru Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini kusubiri huu mwaka wa nne Mhe. Waziri na mimi ni muajiri tu na muda wangu unakaribika kwisha hivi sasa, kila siku naambiwa kesho, kesho, kesho kama mtoto wa kuku anayetaka kunyonya kwa mama yake kufikia kuku mpaka akawa

mkubwa. Hebu Mhe. Waziri, anipe jawabu la ufasaha kuhusu boti kama kuna hakiba kule japo kwenda ku-*repair* angalau tukawapelekea wale watu. Mimi namaliza muda wangu Mheshimiwa, nikuombe sana, hatujui kama kesho tutafika, hii bajeti ya nne Mhe. Waziri, ananipa ahadi hiyo, hebu anieleze kwa udugu wetu uliokuwepo, kwa sababu huwezi kufika Makunduchi kama hujapita Muyuni.

Halafu suala la soko huu ni mwaka wa pili basi hakuna dalili yoyote mpaka muda huu kuhusu soko lile. Mwaka jana tuliambiwa kisingizio Mji Mkongwe, nafikiri Mji Mkongwe wameshaidhinisha kuna dalili gani ya ujenzi ule tujue. Nafikiri amenielewa Mhe. Waziri huu mwaka wa pili tunaokwenda nao kuhusu soko lile kujengwa, pale soko haliridhishi hali ile kigezo kiko wapi au tatizo liko wapi la ujenzi ule, pesa hazipo ili wananchi wapate kujua, aeleze kama pesa hazipo wananchi wapate kujua au huyo mfadhili kaingia mitini tupate kujua, isijekuwa kama ule mradi wa kusarifu mazao kule Kizimbani, aeleze ukweli wananchi wapate kuelewa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim, ujenzi wa soko utaanza wala hauna muda. Kwa sababu kikwazo ilikuwa ni *UNESCO* na tayari wameshatoa *go ahead* na Rais tayari ameshatoa *go ahead*, kwa hivyo, hakuna kikwazo tena cha kuanza ujenzi. Hivyo, wakati wowote unaanza ujenzi, kikwazo ilikuwa ni *UNESCO* tayari wao wameshatoa ile *objection*, kwa hivyo, tatizo liko wapi sasa, ni *tender* tu iliyobakia basi, tupe muda tufanye kazi Mhe. Jaku, kuwa na subira ndugu yangu. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kajibu moja, lile suala la boti hajajibu na hili suala la ujenzi leo mwaka mzima tusubiri mpaka lini? Haya ndio majibu ya serikali siku zote, serikali iko mbioni, wakati wowote, mara tu, haya ndio majibu ya serikali siku zote kwa *back bencher*, hebu tuseme mwakani, baada ya miaka miwili, kesho kutwa, aeleze tu Mheshimiwa ili watu wapate kufahamu, hii ni kazi ya wananchi tupo kwa niaba ya wananchi, hebu atueleze tu Mhe. Waziri, sote tunazungumza Kiswahili humu ndani mwakani, baada ya miezi sita, baada ya miaka miwili ili wananchi wapate kufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, na suala la boti bado mimi nataka ufumbuzi.

Mhe Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hili ni suala la *tender, tender* itapojiri basi wakati wowote tunaanza, hata na wewe mwenyewe kama utaleta basi hakuna tatizo, ni suala la *tender* tu, *tender* ikishamaliza basi. Umenielewa? Basi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kajibu suala la *tender,* sasa hiyo *tender* lini ataitangaza, lini itapitishwa hiyo *tender*?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, naomba umwambie Mhe. Jaku Hashim, lini hiyo *tender* itakuja?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, jamani taratibu za *tender* zinaeleweka. Kwa hivyo, *within three months* tutaitisha *tender*, kwa hivyo, kama yeye atakuwa na *interest* basi, muache aje a-*deal*, halas. Ahsante *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nikushukuru sana tena sana kabisa kwa uvumilivu wako na ustahamilivu wako. Mhe. Waziri, hili wananchi wameshasikia na jawabu yake wameshasikia, nakuja kwenye suala langu la boti sasa. Huu ni mwaka wa nne...

Mhe Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim, jibu lako limeshapatikana, sasa muache waziri uwape nafasi wengine na wao tuendelee. Mhe. Saleh Nassor Juma.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi ni mtumishi wa wananchi kutoka Jimbo la Muyuni na hii ni dhama niliyoibeba, uongozi ni dhama na tunakwenda kuulizwa mbele ya safari tunakokwenda, umewatumikia vipi wananchi wako? Je, uliwahimiza waswali, ni moja ya majukumu yetu. Sasa mimi anieleze huu mwaka wa nne hiyo boti iko wapi na boti wameichukua wao hawa ilikuweko kwa wananchi wa Muyuni wakaichukua, wameipeleka wapi? Sasa hii kama haiwezekani basi mimi anambie tu ataipeleka boti kesho au keshokutwa na kama haipo ajibu wananchi wasikie kuwa ile boti haipatikani tena kwa mwaka wa nne huwezi kumdangaya mtu tena. Kama ni mtoto kazaliwa hutambaa, akapata miguu, akakweta mpaka akenda mbio, leo mwaka wa nne haiwezekani hiki kitu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, tumekusikia, tuendelee. Mhe. Saleh Nassor Juma. Aka! kakujibu Mhe. Waziri, Mhe. Jaku, umeuliza suala moja mara tano kinyume na utaratibu, umepewa nafasi umeuliza, sasa kaa na wengine waulize. Mhe. Saleh Nassor.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, wakati nachangia hapa jana ile kwa masikitiko makubwa Mheshimiwa, nilielezea jinsi ya wavuvi wa dagaa wanavyopata shida sana katika suala zima wanapofanya shughuli zao za kuanika dagaa pale Maruhubi. Sasa Mheshimiwa, mara leo wanaondoshwa hapa Maruhubi, kesho wanapelekwa Nyanjale, Nyanjale wanaondoshwa wanapelekwa Mto Mkuu kiasi ambacho sasa hivi wako taabani na wale wamepewa ajira karibu watu 400 pale.

Sasa namuomba Mhe. Waziri, je, ni lini yeye kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo wataweza kuondosha japo mahoteli kwa sababu wengi ni wageni wakapatiwa hawa wenyeji eneo la kuanika dagaa na kuweza kutupatia ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hilo suala nililijibu kwamba tayari tumeshatenda hilo eneo ili waweze kutumia watu waanikaji madagaa na vifaa tumeshawapa, Maruhubi pamoja na Mangapwani. Tumeshawapelekea chanja pamoja na vifaa vingine ili kuona kwamba uanikaji dagaa unafanikiwa. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe alitaka tuwasaidie kiasi gani na hapo utapofika muda wa kwamba labda kuhamishwa tutawaeleza, tutashirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ili tuone wapi tunaweza kuwapeleka, lakini *so far* ni kwamba pale pale Maruhubi pamoja na Mangapwani tumeshawapelekea vifaa kama chanja ili kuona ule uanikaji wa dagaa unakwenda ipasavyo.

Kwa hivyo, itapofika muda wa kuwahamisha tutawaeleza vile vile, tutashirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tuone maeneo gani tunaweza tukawapa waanikaji wa dagaa letu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimelisikia jibu lake, lakini vile vile nimekwenda kwa hawa waanikaji madagaa ni kwamba eneo la Maruhubi ambacho hicho kipande walichopewa ni kidogo sana na wakati wowote utakapoanza ujenzi wa ile bandari pale hata kule kuna wasiwasi wa kuondoshwa. Sasa hiyo sehemu waliyowapatia sijui Mangapwani ni ndogo, atueleze kwamba kama yuko tayari Mheshimiwa, kuondoka hapa na kamati ile inayoshughulikia mambo haya wakenda wakaangalia eneo ambalo linatosha na la kudumu kabisa ili wasiyumbishwe yumbishwe kama wanavyoyumbishwa hivi sasa. Kwa sababu hata huko Mto mkubwa sijui wapi kule Kaskazini, nako vile vile tunaambiwa hilo eneo lina mwenyewe na wakati wowote wataondoshwa wale, sasa wapate pahala watulie.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe Mwenyekiti, ni kweli lakini hilo suala la kujenga hiyo bandari kwa kweli litachukua muda mrefu, sio kwamba leo na kesho, hiyo *within this time* kwamba sisi tunawafikiria wapi pa kuwapeleka hawa watu. Kwa hivyo, itachukua muda sio kwamba kesho kutwa au usiku wa kucha tu, hapana. Kwa hivyo, tutashirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ili kufikiria wapi utapofika muda huo tujue wapi pa kuwapeleka, lakini tuelewe kwamba sio leo na kesho. Eneo tumeshaliona kweli ni dogo na tuko tayari tutashirikiana na kamati ili kwenda kuona tukishirikiana tuone nini cha kufanya ili kuwasaidia waanikaji madagaa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi, naomba tukubaliane kwamba tunaelewa hili suala na *Inshaallah* madhali tuna nia njema basi tutalitekeleza tu, waache waendelee hiyo sehemu ndogo lakini tunakaa na tunafikiria wapi pa kuwapeleka na tutakaa na kamati kama ulivyoelekeza ili tuone waanikaji wa madagaa yetu nao wanaishi kama tunavyoishi sisi. Nakushukuru sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana mimi sitaki nionekane mkaidi katika hili, lakini nataka tuone kwamba wazawa nao wana nafasi katika ku-*enjoy* hii keki ya nchi ikiwa ni pamoja na matumizi ya ardhi. Sasa mimi nilikuwa nina *concern* yangu ni kwamba badala ya kuwaruhusu Wataliana kujenga mahoteli tu katika ufukwe, basi na hawa wavuvi wapewe sehemu ya kudumu katika ufukwe huu waweze kuweka biashara yao ya dagaa na waweze kutoa ajira. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa hii na mimi. Mimi nilitaka Mhe. Waziri, anipe maelezo tu, si mkaidi wala sina tabu na yeye, namwambia kwa upole kabisa. Nilipochangia nilizungumza na nikatoa *concern* ya Mhe. Hija Hassan Hija na kumpa pole kwa yule mvuvi wake aliyeliwa na papa na nikatoa ile historia ya mvuvi aliyeliwa mkono na papa akafa, nikasema ingekuwa kuna chombo cha kumuhani kule baharini basi angeliwahiwa, pamoja na kwamba siku yake ilikuwa ndio ishafika angekufa, lakini nilimwambia Mheshimiwa, kwamba kuna haja ya kuweka faiba za wavuvi za kuokolea maisha wanapopata matatizo baharini. Kwa hiyo, kuna haja ya kulifikiria hili suala zikawekwa faiba maalum ambazo ni za kwenda mwendo wa kasi wanapopata matatizo wavuvi wetu wakaokolewa ili kuona kwamba na wao serikali yao inawathamini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala Mhe. Waziri, sijui alisahau lakini naona jibu hajanipa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru inawezekana labda nimesahau, unajua tena uliponikumbusha habari ya *time* pale, tena mimi nikawa nina-*rush*. Lakini kwa kweli ni ushauri mzuri sana na ni suala ambalo tunalifikiria vile vile, tumeyafikiria mengi na tumeyatekeleza. Kwa mfano, kama hii kuwapelekea vihori wakulima wetu, kwa hivyo, na hilo suala la kuweka faiba kwa ajili ya kuwaokoa *in case* ya ajali yoyote basi nalo tunalifikiria vile vile kwa sababu ni moja katika mikakati yetu ya wizara. Mhe. Subeit Khamis, naomba unipe subira tumo katika harakati nalo tutalitekeleza kama tulivyotekeleza mengine.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri, kasema kuwa hili suala ni zuri, nafikiri na serikali kule nawaona Waziri wa Fedha na

viongozi wengine wakishika shika vichwa kuona kwamba hili suala wamelibariki. Kwa hiyo, naomba tuendelee.

Kifungu S02 Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi Shs. 11,953,638,000/=

Jumla ya Kifungu: **Shs.12,836,348,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KIFUNGU P03 UTAWALA WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu S01 Utawala na Mafunzo Shs.1,010,377,000/=
Kifungu S02 Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti Shs. 376,961,000/=

Kifungu Kidogo A03 Programu ndogo Uratibu wa Afisi Kuu Pemba Shs. 970,201,000/=

Jumla ya Kifungu P03 Programu ya Utawala wa Maendeleo ya Mifugo Na uvuvi Shs. 2,357,539,000/=

JUMLA KUU **Shs. 17,127,500,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo Juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe.Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwa Baraza liyakubali Makadirio haya, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ameshatoa hoja wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makazi Maji na Nishati kwa mwaka wa Fedha 2015/2016

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba utulivu. Anayetoka atoke taratibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, aidha, naomba nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kutujaalia uzima na afya njema na kwa kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu kuwasilisha hotuba ya Wizara hii mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jinsi alivyokuwa karibu sana na Wizara yangu kwa kutupa miongozo na maelekezo ambayo yamechangia sana katika kuziendeleza Sekta zilizomo katika Wizara yangu. Vile vile, napenda kutoa shukuran zetu za dhati kwa Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa ushauri na maelekezo yao juu ya utekelezaji wa kazi za Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kutumia fursa hii kuonesha hisia za pekee kwa niaba ya Wizara yangu kutoa Mkono wa rambi rambi kwa Baraza la Wawakilishi, Familia pamoja na Wazanzibari wote kwa kifo cha aliekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha ya Baraza, Marehemu Salmin Awadh Salmin Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni ambacho kimetokea takriban miezi mitatu iliopita.

Marehemu Salmin Awadh Salmin ameweza kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha utendaji wa shughuli za Baraza pamoja na kuisaidia Wizara hii kuwa na ufanisi wa hali ya juu, na kwamba kifo chake kimeacha huzuni na pengo sio tu kwa Baraza na familia yake bali pia kwa Wizara yangu na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (*S.W*) ailaze roho ya Marehemu mahala pema peponi. *Amin*.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba pia niungane na Mawaziri wenzangu kutoa mkono wa pole kwa Wananchi wote walioathirika kutokana na maafa yaliotokana na mvua kubwa zilizonyesha katika visiwa vyetu. Sote tunaamini kwamba mvua ni neema, lakini haya yote yametokea kutokana na kudra ya Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi. Hivyo, tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subira wale wote ambao kwa namna moja au nyengine wameguswa na maafa haya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kuelezea utekelezaji wa kazi za kawaida na za maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na muelekeo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kama ifuatavyo:-

Mapato na Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, suala la ukusanyaji wa mapato ni kiashiria muhimu sana katika kupima mafanikio ya utekelezaji. Wizara yangu katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 4,416,900,000/= kutokana na vyanzo mbali mbali vya Taasisi zake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2015 jumla ya Tsh 2,941,212,789 zimekusanywa. Kiwango hichi ni sawa na asilimia 67 ya makadirio.

Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia Kiambatanisho “A”.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya Mwaka wa Fedha 2014/15, Wizara yangu imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 34,558,958,000/=. Kati ya Fedha hizo, kazi za kawaida ni Tsh 7,760, 100,000/= na kazi za maendeleo ni Tsh 26,798,858,000/=.

Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2015 Wizara yangu ilikwishapatiwa Tsh 4,268,534,677.00 kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia 15.92 na Tsh 4,958,566,207.00 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 64 ya makadirio, hivyo, kufanya jumla ya fedha zote tulizozipata kuwa ni Tsh 9,227,100,884.00 sawa na asilimia 27 ya makisio yote.

Kwa ufafanuzi zaidi angalia Kiambatanisho “B1, B2 na B3”.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imewajibika katika kusimamia na kuratibu kazi zote za Wizara zikiwemo za kawaida na za Maendeleo. Kwa upande wa kazi za Maendeleo Idara hii ilisimamia Utekelezaji wa

miradi ya maendeleo ambapo ulijumuisha kazi za ufuatiliaji na Tathmini (*Monitoring and Evaluation*) ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo inatekelezwa ipasavyo. Miradi iliyosimamiwa na idara hii ni pamoja na ifuatayo:-

i. Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Mjini Magharibi
ii. Uhuishaji na Upanuzi wa shughuli za Maji Mijini
iii. Usambazaji wa Maji Vijijini
iv. Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji
v. Usambazaji Umeme Vijijini
vi. Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme Unguja na Pemba
vii. Utekelezaji wa Sera ya Nishati
viii. Utafiti wa Nishati Mbadala
ix. Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE II*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa shughuli za uratibu, Idara ipo katika hatua za mwisho za uratibu wa mradi wa *MCC* awamu ya pili ambao unategemewa kuimarisha sekta ya Nishati kwa kuimarisha huduma za usambazaji wa umeme, kuimarisha *Management* ya Shirirka na mifumo ya uendeshaji pamoja na kuimarisha Mamlaka ya Udhibiti wa bei (*ZURA*) kwa kuijengea uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mikakati ya kuhakikisha kwamba Sekta ya Ardhi inasimamiwa vizuri, Wizara imeendeleza hatua ya mapitio ya Sera ya Ardhi ambapo mapitio kwa hatua ya awali yamekamilika na kitakachofuata ni kuwasilishwa kwa Rasimu katika vikao vya ngazi za juu Serikalini. Kwa upande mwengine Sheria ya Uundwaji wa Kamisheni ya ardhi na Sheria ya Wadhamini zimekamilika na kupitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa kazi za uchambuzi wa maeneo ya kuendelezwa utafiti kwa Sekta za Wizara, tayari idara imeanza kutekeleza utafiti juu ya sababu zinazopelekea ongezeko la migogoro ya ardhi nchini ambapo hatua za ukusanyaji wa taarifa kutoka maeneo mbali mbali zinaendelea.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kusimamia Rasilimali Watu na uendeshaji wa kazi za Wizara za kila siku. Wizara yangu kupitia Tume ya Utumishi Serikalini imeweza kufanya uajiri wa wafanyakazi wapya 15 kwa Mwaka Fedha 2014/2015, ikiwa ni ujazaji wa nafasi zilizokuwa wazi kwa sababu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Uimarishaji wa mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi na maslahi yao pamoja na kuwajengea uwezo yanaonekana kuanzia *paragraph* ya 14 hadi 16 ya hotuba yangu.

IDARA ARDHI NA USAJILI

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Idara hii imetekeleza yafuatayo;-
Kuandaa Hati Za Matumizi Ya Ardhi Na Kutengeza Mfumo Wa Kumbukumbu Za Ardhi (*Database*)

Mhe. Mwenyekiti, Katika kuhakikisha kuwa kila mwananchi mwenye haki ya matumizi ya ardhi anaipata haki hiyo, Wizara yangu imefanikiwa kutengeneza na kuzitia saini jumla ya Hati 850 zikiwa ni hati za kudumu. Hati hizo ni kwa mwananchi mmoja mmoja na pia zinazohusu Taasisi za Serikali na Kiraia. Aidha, tumeendelea na Kazi ya uwekaji wa kumbukumbu sahihi za ardhi ili kurahisisha upatikanaji wa Taarifa za Ardhi kwa wakati.

Ukodishaji Wa Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka 2014/2015 Wizara kupitia Idara ya Ardhi iliyafanyia kazi maombi ya *extension* yanayohusu wawekezaji wanaoomba kuongeza maeneo waliyokuwa nayo awali ambapo jumla ya *Lease Extension* 15 zilitiwa saini na kupewa wawekezaji. Aidha, kwa upande wa mikataba mipya, jumla ya mikataba 47 ilitiwa saini na kukabidhiwa wahusika.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo zaidi ya utekelezaji idara hii yanapatikana katika *paragraph* ya 20 hadi 22 ya hotuba hii.

MAHAKAMA YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi imeendelea na kazi zake kwa kupokea, kusikiliza na kuamua kesi zinazohusiana na migogoro ya ardhi inayowasilishwa na wananchi na taasisi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mahakama imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Mahakama ya ardhi imepokea kesi mpya 223 ambazo zimefunguliwa Unguja na pemba pamoja na kesi za awali Mahakama imeendesha vikao 12,460 vya kusikiliza kesi ambapo kesi 200 zimetolewa maamuzi kwa mchanganuo ufuatao:-

   Unguja: Kesi mpya 122 zimepokelewa na kesi 109 zimetolewa maamuzi.

Pemba: Kesi mpya 101 zimepokelewa na kesi 91 zimetolewa maamuzi.

ii. Hadi kufikia Machi, 2015 Mahakama ya Ardhi imefikia lengo la kesi zilizotolewa maamuzi kwa kutoa maamuzi ya kesi 200 sawa na asilimia mia moja (100%) ya lengo lililokusudiwa.

iii. Mahakama ya Ardhi Mkoa wa Kusini Unguja (Koani) tayari imeshaanza kazi.

AFISI YA MRAJIS WA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mrajis wa Ardhi ni Taasisi yenye jukumu la kusajili ardhi yote ya Zanzibar pamoja na kuweka kumbukumbu za uhakiki kwa wenye haki ya matumizi ya ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi hii imeweza kutekeleza kazi zifuatazao:-

i. Kusajili jumla ya maeneo 4,000 katika Shehia 19 za Mji Mkongwe na Ng'ambo na Shehia ya Nungwi kwa Upande wa Unguja. Kwa upande wa Pemba jumla ya maeneo 500 katika Shehia ya Mkoroshoni yamesajiliwa na hatua zinaendelea katika Shehia ya Kiungoni;

ii. Jumla ya Nyumba, viwanja na mashamba 22,398 kwa Unguja na Pemba yameshatambuliwa na yanaendelea na hatua za usajili;

iii. Jumla ya kadi 395 zimetolewa kwa wananchi ambao ardhi zao zimekwisha kusajiliwa kwa Mjini na Ng'ambo;

iv. Kutoa elimu ya usajili wa ardhi kwa wananchi ambapo jumla ya vipindi 9 vya redio, semina 4 ambazo ziliwasishirikisha waandishi wa habari, wanafunzi, taasisi mbali mbali za Serikali na Binafsi, Masheha na Jamii kwa Ujumla;

v. Kwa kushirikiana na Idara za Ardhi, Afisi ya Mrajis wa Ardhi imeandaa Jarida la Mwaka la ardhi ambalo litatoa habari kwa Wananchi juu ya maendeleo ya Sekta ya Ardhi Nchini pamoja na kutoa taaluma ya Sheria mbali mbali za Ardhi;

vi. Kuwajengea uwezo Wafanyakazi wa Sekta ya Ardhi kuhusiana na Usajili wa Ardhi ambapo Semina moja iliandaliwa na kuendeshwa na wakufunzi kutoka Kenya;

vii. Kuweka kumbukumbu za Usajili kwa njia za Kisasa (*computerization*);

viii. Kushajihisha wanafunzi kujifunza masuala ya Ardhi na Usajili kwa njia za Utungaji na Uandishi wa Insha ambapo jumla ya wanafunzi 10 waliofanya vizuri katika mashindano ya Uandishi kuhusiana na Usajili wa Ardhi walipatiwa zawadi.

IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Upimaji na Ramani inajukumu la kusimamia upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani mbali mbali za ardhi katika visiwa vya Unguja na Pemba, vile vile Idara hii inajukumu la kuendeleza mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa kumbukumbu muhimu zinazohusiana na ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Upimaji na Ramani katika Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2014/2015 imeweza kutekeleza kazi zifuatazao:-

Kuandaa Mfumo Wa Uwekezaji Na Utumiaji Wa Taarifa Za Ardhi Kwa Manufaa Ya Wadau Mbalimbali (*ZALIS*)

Mhe. Mwenyekiti, katika kuuandaa mfumo wa *ZALIS (Zanzibar Land Information System)* ili uweze kutoa taarifa kwa ufanisi, miundombinu ya *IT* imeimarishwa, mfumo (*Surveying plugin QGIS*) wa upimaji ndani ya *ZALIS* umeandaliwa kwa majaribio ya kazi za Upimaji na Ramani. Aidha, wafanyakazi 12 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa ajili kuendesha mfumo wa *ZALIS*.

Kuandaa Na Kuimarisha Utendaji Wa Shughuli Za Upimaji Ardhi Kwa Matumizi Mbalimbali.

Mhe. Mwenyekiti, Upimaji Ardhi nchini umeendelea kuimarishwa kwa kuzipitia upya alama za upimaji pamoja na kuipitia mipaka ya kiutawala Unguja na Pemba ambapo jumla ya alama 89 za upimaji zimewekwa. Aidha, Idara ya Upimaji na Ramani kwa kushirikiana na Idara nyengine za Ardhi imefanikisha kazi za upimaji kwa ajili ya Utambuzi na Usajilli wa ardhi katika maeneo ya Mijini na Vijijini.
Vile vile, Idara imeendelea na kazi za Upimaji wa viwanja kwa maeneo mbali mbali kama inavyoonekana katika Jaduweli nambari 1

Jaduweli Nambari 1:Idadi ya Maeneo Yaliyopwimwa Julai 2014 –Machi 2015

Namb.	AINA YA MAENEO YALIYOPIMWA	IDADI
1	Makaazi	123
2	Viwanja vya huduma mbali mbali	44
3	Vitega uchumi	32

4	Taasisi	39
5	Mashamba ya kilimo na ya watu binafsi	271
JUMLA		**509**

Kuimarisha Shughuli Za Kuzipitia Ramani Za Msingi (*Base Mape*) Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo zaidi kuhusiana na shughuli za upimaji wa ramani pamoja na kuwajengea wananchi wa uwelewa juu ya utawala wa ardhi yanaonekana katika *paragraph* ya 28 hadi 30 ya hotuba yangu.

IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango Miji na Vijiji ni chombo chenye dhamana ya Upangaji wa Matumizi bora ya Ardhi pamoja na kuratibu utekelezalezaji wake. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ilitekeleza majukumu yafuatavyo:-

Kupanga Matumizi Ya Ardhi Ya Miji Miwili Na Vijiji Vinne Na Kuendelea Kuratibu Na Kushajihisha Utekelezaji Wa Mipango Na Mikakati Ya Matumizi Ya Ardhi Kwa Miji Na Vijiji Mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo hili, Idara imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kutayarisha Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi Zanzibar (*National Spatial Development Strategy - NSDS*).

Mhe. Mwenyekiti, Ninafuraha kukujulisha kuwa, tarehe 24 Machi 2015, Baraza la Mapinduzi lilipitisha rasmi Mpango Mkakati wa Maendeleo ya ardhi Zanzibar (*National Spatial Development Strategy*). Idara ya Mipango Miji, tayari imeshaanza utekelazaji wa Mpango huu kwa kutoa elimu kwa jamii na taasisi za Serikali na za Kiraia. Aidha, sambamba na kazi hii Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mikoa yote Mitano ya Zanzibar imeshatayarishwa.

ii. Kutayarisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ya Mji wa Zanzibar (*Zanzibar Master Plan*)

Mhe. Mwenyekiti, Kwa muda mrefu sasa suala la ujenzi holela katika Mji wa Zanzibar limekuwa likipigiwa kelele. Zipo sababu nyingi zinazopeleka ujenzi holela katika Miji na Vijiji. Miongoni mwao ni ukosefu wa mipango ya matumzi bora ya ardhi na usimamizi mdogo wa shughuli zote za ujenzi ndani ya miji yetu.

Napenda kulijuilisha Baraza lako Tukufu kwamba, Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ya Mji wa Zanzibar (*Zanzibar Master Plan*) umekamilika. Idara ya Mipango Miji imeshaanza utekelzaji wake kwa kutoa elimu kwa jamii na Taasisi za Serikali.

iii. Kukamilisha utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi wa Mji wa Chake Chake na kutayarisha mikakati ya utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu bado inaendelea na jitihada za kutayarisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ya Mji wa Chake Chake. Suala hili litapewa tena kipaumbele katika bajeti ya 2015/2016 kwani kutokana na hali ya kifedha halikuweza kutekelezwa katika bajeti iliyopita ya mwaka 2014/2015.

iv. Kutayarisha Mpango wa Uendelezaji wa Ukanda wa Pwani kwa Mji wa Mkokotoni na Mji wa Chwaka Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kupitia Idara ya Mipango Miji tayari imeshatayarisha Mipango ya Miji mitatu midogo ambayo ni Mji wa Mkokotoni, Mji wa Chwaka na Mji wa Nungwi.

v. Kukamilisha uundwaji wa Mfuko wa maendeleo ya Mji *"Urban Development Fund".*

Mhe. Mwenyekiti, *paragraph* ya 33 hadi 37 inafafanua kwa kina kuhisiana na utekelezaji wa kazi za upangaji wa matumizi ya miji na vijiji.

Kukamilisha Utayarishaji Wa Sera Ya Uendelezaji Miji, Kupitia Sheria Ya Upangaji Miji Na Vijiji Na Kutayarisha Miongozo Ya Uendelezaji Miji Kwa Mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo hili, Idara ya Mipango Miji tayari imeshatayarisha Rasimu ya Sera, Sheria na Kanuni za Mipango Miji ambazo zinajadiliwa na wadau.

Kutekeleza Mkakati Wa Mawasiliano Wa Idara Kwa Kukuza Uwelewa Wa Jamii Katika Masuala Ya Upangaji Wa Matumizi Ya Ardhi Na Umuhimu Wake Na Kushajiisha Masuala Ya Ki-Jinsia Ndani Ya Utendaji Wa Idara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo hili, Wizara yangu kwa kupitia Idara ya Mipango Miji na Vijiji imefanya Semina, katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Shehia za Unguja na Pemba. Idara imeelimisha jamii kupitia vipindi vya redio na kutoa makala tofauti kuhusu kazi zake za kila leo.

IDARA YA UJENZI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Ujenzi imetekeleza kazi zifuatazo:-

Kufanya matengenezo katika nyumba za Mandeleo za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo hili, Idara imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Utawala Bora imesimamia ujenzi wa Jengo la Wizara hiyo.

ii. Idara imesimamia Ukarabati wa Jengo la Tume ya Sayansi liliopo Maruhubi.

Bodi ya Usajili wa Wakandarasi

Mhe. Mwenyekiti, Bodi hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 imetekeleza yafuatayo:-

i. Jumla ya Wakandaasi 59 tayari wamesajiliwa na hivyo kufanya idadi ya Wakandarasi wote waliosajiliwa na Bodi kufikia 142 hadi hivi sasa
.

ii. Bodi imeanza kuendesha vipindi kwenye televisheni kwa ajili ya kuelimisha Wakandarasi, wananchi na wadau mbali mbali juu ya kazi za Bodi, majukumu ya wakandarasi, na malengo ya Bodi katika kuhakikisha Ujenzi bora na salama nchini.

iii. Bodi imefanya ukaguzi katika maeneo mbali mbali katika kuangalia kazi zinazofanywa na Wakandarasi ili kuhakikisha wanafuata sheria. Jumla ya washukiwa 403 walikamatwa na wakaelekezwa na walioendelea kukaidi walichukuliwa hatua mbali mbali.

iv. Bodi pia imefanya juhudi za kuwashajiisha wanafunzi wa kidato cha nne kusoma masomo ya sayansi kwa kuwapatia zawadi wanafunzi wote waliofanikiwa kupata alama ya “A” katika masomo ya fizikia na hesabati Unguja na Pemba.

Bodi ya Kusajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi hii inaendelea na kusajili na kuratibu shughuli za Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo. Hadi kufikia mwezi Machi 2015, Bodi imetekeleza yafuatayo:-

i. Bodi imeweza kusajili miradi 97 ambayo imesimamiwa na wataalamu walio sajiliwa;

ii. Bodi imefanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali *(Site Inspections)* katika kuangalia kazi zinavyofanywa na Wataalamu wetu ili kuhakikisha wanafuata sheria. Jumla ya washukiwa 65 walikamatwa na wakaelekezwa jinsi ya kufuata sheria na walioendelea kukaidi wamechukuliwa hatua za kisheria; na

iii. Bodi imesajili wataalamu 56 wa daraja mbali mbali kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015.

IDARA YA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi inajukumu la kusimamia Nyumba za Serikali Unguja na Pemba, kwa kuzikodisha kwa Wananchi na kuzifanyia matengenezo yanayofaa. Pia, kuhakikisha kuwa Wananchi wa Unguja na Pemba wanapata makaazi bora na yalio salama. Katika Mwaka wa Fedha 2014/15 Idara imeweza kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Matayarisho Kwa Ajili Ya Uanzishaji Wa Shirika La Nyumba Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mwezi wa Oktoba 2014 Baraza lako Tukufu liliijadili na kuipitisha Sheria ya Uanzishaji wa Shirika la Nyumba Zanzibar. Hatua zinazoendelea kwa sasa ni Idara kuzikagua na kuzifanyia uhakiki na tathimini nyumba zake kwa lengo la kujua thamani ya kila nyumba na hali halisi ya ubovu na uimara kwa kila jengo ambapo zoezi limeanza kwa Nyumba za Serikali zilizopo Mji Mkongwe.

Kujua thamani ya kila nyumba hizo itasaidia kujua thamani ya mtaji wa Shirika la Nyumba litakapoanza, na vile vile kuweza kujua uzima na ukubwa wa mahitaji ya matengenezo.

2. Kuzifanyia matengenezo Nyumba za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2014/15, Idara imeweza kufanya matengenezo yafuatayo katika Nyumba za Maendeleo:

i. Kusafisha na kutoa maji machafu katika chemba *Block* namba 3 na 4 Michenzani;

ii. Kusafisha (kuzibua) bomba ya maji machafu kuanzia *Block* namba 9 hadi Maisara;
iii. Kuondoa maji yaliotuama *Block* namba 13 Kilimani na kuweka mabomba mapya ya maji machafu;
iv. Kusafisha baadhi ya chemba Mombasa 'A'; na

v. Kuweka bomba mpya ya maji machafu baada ya awali kuvunjwa *Block* namba 8 Michenzani.

Pia, katika ukaguzi uliofanywa katika Nyumba za Serikali Mji Mkongwe, Zanzibar imebainika kuwa nyumba 26 ziko katika hali mbaya na zinahitaji matengenezo makubwa na ya haraka. Hatua tayari zimechukuliwa za kuwajulisha Wapangaji juu ya ubovu wa majengo hayo na hatari ya kuendelea kuyatumia majengo hayo.

3. Kukusanya Mapato Yatokanayo Na Ardhi Ukodishaji Wa Nyumba Za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mwezi Machi 2015, Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi imeweza kukusanya jumla ya Tsh.400,285,695/=. *(*Mhe. Mwenyekiti, takwimu hii nina wasi wasi nayo, kwa hivyo, ndani ya kitabu itakuwa vyengine*)* ambazo ni sawa na asilimia sabini na sita (76%) ya lengo ambalo ni Tsh 524,000,000/=. Ni matumaini yetu kuwa tutafikia lengo hilo mwishoni mwa mwaka huu wa fedha.

4. Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imeendelea kusikiliza mashauri ya kuyatolea maamuzi. Hadi kufikia Mwezi Machi 2015, jumla ya mashauri 25 yamewasilishwa na kusikilizwa ambapo mashauri 10 yametolewa maamuzi.

MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ina jukumu la Uhifadhi wa Urithi wa Kimataifa wa eneo zima la Mji Mkongwe, ukijumuisha urithi wa kihistoria wa majengo, utamaduni wa asili, mandhari, na vivutio vyengine na kuhakikisha vinabakia katika hali yake ya asili kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Mamlaka ilifanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

Kusimamia Miradi ya Uhifadhi wa Majengo ya Mji Mkongwe

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka imeendelea kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa ukarabati wa jengo la *People's Palace*,Chawl Building na Beit-al Jaibu. Maelezo zaidi yanapatikana *paragraph* 21 hadi 23 ya hotuba yangu.

i. **Ukarabati wa Jengo la People's Palace**

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka imeliezua na kuliezeka upya paa lililokuwa linavuja katika afisi ya Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi iliopo Forodhani. Mamlaka pia imefanya matengenezo na marekebisho ya eneo linalotarajiwa kuwa ukumbi wa huduma ya chakula katika jengo la People's Palace na mazingira yake.

Aidha, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa jengo la People's Palace na kuona kuwa Ukuta wa kusini wa jengo hilo uko katika hali mbaya. Mamlaka imechukua hatua ya kuweka miega katika "*Coner*" ya Kusini /Magharibi ili kuzisaidia kuta hizo pamoja na kuweka mihimili (*vertical supports*) ndani ya chumba cha chini na cha ghorofa ya kwanza kuzuia dari za vyumba hivyo.

ii. **Ukarabati wa Jengo la Chawl Building**

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeunda kamati ya mawaziri watatu kwa ajili ya kuzungumza na wafanyabiashara wa jengo hilo juu ya namna ya kuhama na kurejeshwa pamoja na utaratibu mzima wa ukarabati wa jengo hilo, katika majadiliano hayo wafanyabiashara walitoa mapendekezo yao kwa Serikali ambayo kamati iliyoundwa inaendelea kuyafanyia kazi.

iii. **Ukarabati wa Jengo la Beit-al ajaib**

Mhe. Mwenyekiti, Mtaalamu wa masuala ya uhifadhi kutoka Oman Dr. Enrico alikuja mwezi Februari na kufanya majadiliano na uongozi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe pamoja na wataalamu wa makumbusho Zanzibar, majadiliano hayo yamepelekea mapendekezo ya ukarabati huo yawe kwa awamu (*phase*). Vile vile, mapendekezo haya yamepelekea marekebisho madogo madogo ya ramani pamoja na gharama ambayo Mamlaka imeshaikamilisha na kuiwasilisha nchini Oman

iv. **Ujenzi Wa Ukuta Wa Ukingo Wa Bahari Ya Mizingani**

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeshafunga Mkataba na Kampuni ya "*SEYANI BROTHERS & CO (T) LTD"* ya Tanzania kwa ajili ya ujenzi huo na kazi za maandalizi ya ujenzi zimeshaanza.

v. **Ukaguzi Wa Nyumba Zilizomo Ndani Ya Eneo La Mji Mkongwe.**

Mhe. Mwenyekiti, Ukaguzi wa eneo la Mji Mkonge umeendelea kufanyika katika shughuli za kila siku za Mamlaka na kubaini kuwepo kwa nyumba 89 zilizo katika hali mbaya, 40 kati ya hizo ziko katika hali mbaya sana . Jaduweli nambari 2 linafafanua zaidi.

Jaduweli Nambari 2: Ukaguzi Wa Nyumba Ndani ya Eneo La Mji Mkongwe

Mmiliki	**Nyumba Zilizo Katika Hali Mbaya**	**Nyumba Zilizo Katika Hali Mbaya Sana**	**Nyumba zilizoanguka**	
			Yote nzima	**Sehemu ndogo**
Serikali	21	4	-	-
Kamisheni ya wakfu	12	6	-	-
Watu binafsi	56	30	1	2
Jumla	**89**	**40**	**1**	**2**

MAMLAKA YA MAJI

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kuzingatia Malengo ya Milenia, Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II), Sera ya Maji ya Mwaka 2004, Sheria ya Maji ya Mwaka 2006 na Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 imetekeleza Programu na miradi ya maji ifuatayo:-

i. **Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini**

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuwapatia maji safi na salama wananchi waishio vijijini katika umbali usiozidi mita 250 kutoka kwenye makazi yao kupitia Programu ya usambazaji maji Vijijini kwa ukamilishaji wa miradi, ukarabati wa miundombinu, ulazaji mabomba, ufungaji mita, upelekaji umeme katika visima

vya maji, ulipaji fidia kwa maeneo yaliothiriwa na mradi, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu, uchimbaji visima, ujenzi wa uzio na ujenzi wa matangi katika maeneo mbali mbali ya Vijijini Unguja na Pemba. Kwa ufafanuzi zaidi angalia Jaduweli Nam. 3 lifuatalo:-

Jaduweli nambari 3: Kazi za Usambazaji wa Maji Vijijini

S/NO	KAZI ZILIZOFANYIKA	ENEO	UTEKELEZAJI
1.	Uchimbaji wa visima	Michamvi, Kinduni na Kibuteni Unguja.	Kazi imekamilika
2.	Ulazaji wa mabomba	Kijini na Nungwi kwa Unguja Kidundo, Chekea, Chambani na tumbe kwa Pemba	Kazi hii ni endelevu
3.	Uwekaji wa pampu na mota mpya	Kilindi, Donge, Mtende, Kizimkazi, Kitogani, Matemwe, Muyuni, Kilimbero, Bwejuu, Chaani masingini, Uroa, Kajengwa, Chaani Tasafu, Bambi na Kilimani Tazari kwa Unguja Mgagadu, Mchanga Mdogo, Shengejuu Ng'ambwa, Konde Kironjo A, na Michenzani kwa Pemba.	Kazi ya uwekaji pampu na mota ni endelevu
4	Ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu	Uroa, Donge (Tingatinga), Nungwi kae na Matemwe Kigomani na kilombero (Unguja) kiwani, Chambani na Mahuduthi kwa Pemba.	Kazi inaedelea
5	Ujenzi wa matangi	Makunduchi	Kazi imekalika.
6	Upelekaji wa umeme	Kilindi Unguja, Chambani na Kiwani kwa Pemba	Kazi imekamilika
7	Ujenzi wa uzio katika maeneo ya vianzio vya maji.	Kibuteni, Kianga (N7) Unguja.	Kazi inaendelea

8	Ujenzi wa vituo vya huduma kwa wateja na malipo ya maji	Paje.	Kazi inaendelea
		Mahonda	Kazi imekamilika
9.	Ufungaji wa Mita za wateja.	Chwaka, Marumbi, Jambiani, Pongwe, Dunga, Nungwi, Mjini, Kizimkazi, Matemwe na Bumbwini Kwa Unguja, Kojani, Kiuyu, Mjimbini, Muharitani, , Migombani, Chanjamjawiri, Kilindi,Tumbe, Micheweni, Mnarani, Mbuzini, Masota, Kitoi, Fundo, Mchangamdogo, Junguni, Kinyasini, Mtambwe, Kangagani, Mzambarau Takao, Chokocho, Unganda, Mkanyageni, Kengeja, Ukutini, Jundamiti, Muambe, Kendwa, Kiwani, Madungu na Ng'wachani Uwondwe,Timba, Raha na Mgagadu kwa Pemba.	Kazi hii ni endelevu

Aidha, kupitia Programu hii miradi mengine midogo iliyopangwa kutekelezwa ambayo haikuweza Kukamilika katika mwaka huu wa fedha ni pamoja na Mtende, Muyuni, Kinduni, Kibuteni – Makunduchi, Kidoti, Bumbwini Maji Mekundu, Moga-Mwembe Mkali, Uroa Ndijani, Bambi, Chaani Bandamaji ,Matuleni, Muambe, Shumba viamboni, Wingwi Mtemani, Wingwi, Mjananza, Mgongoni, Masipa, Mtambile na Mtambwe Kaskazini

ii. **Progarmu ya Uhuishaji Na Upanuzi Wa Shughuli za Maji Mijini**

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu katika programu hii imeweza kuchimba visima, kulaza mabomba mapya, kununua pampu na mota, ufungaji wa mita, ujenzi wa

vibanda vya kuendeshea pampu na ujenzi wa uzio katika maeneo mbali mbali kama inavyoonyeshwa katika jaduweli Nam. 4 lifuatalo:-

Jaduweli nambari 4: Kazi za Uhuishaji Na Upanuzi Wa Shughuli za Maji Mijini

S/no	KAZI ZILIZOFA-NYIKA	ENEO	UTEKELEZAJI
1.	Ufungaji wa Mita za maji	Bububu, Makadara, na Kijichi, Taveta na Magogoni kwa Unguja, na Wawi, Tibirizi, Madungu, Uwanja wa Ndege na Limbani, Jadida, Bopwe, Uweleni, Makadara, Bahanasa. Micheweni kwa Pemba.	Kazi ya ufungaji mita ni endelevu
2.	Uchimbaji wa visima	Mtofaani na Masingini kwa Unguja.	Kazi imekamilika
3.	Uwekaji wa pampu na Mota mpya	Kaburi Kikombe, Saateni, Kinumoshi N4, Mbweni matrekta, Ali Yussuf, Sebleni, Workshop Chumbuni Kihinani, Chukwani, na Kwa binti Amrani (Unguja) Sharif Ali namba-1,2 na 3, Darajani, Jondeni, Jamvini na Kwa Bi Mtumwa kwa Pemba.	kazi hii ni endelevu
4.	Ulazaji wa mabomba	Kikwajuin, Welezo Semuso, na Kilimani kwa (Unguja) na Mbiji, Mtuhaliwa Mkoani, Ng'ambwa, Sharifuali Chake Chake na Taifu, kwa Pemba	kazi hii ni endelevu
5.	Ujenzi wa Uzio	Chemchem ya Mwanyanya na Chemchem Ya Mto Pepo, Kianga N9(1) N9(2), kwa Unguja Chanjaani kwa Pemba.	Kazi inaendelea
6.	Ununuzi wa vidhibiti umeme	**Unguja**: Mombasa Ofisini, Kizimbani Sebleni na Saateni workshop **Pemba:** Kironjo Kijuki na Sizini, Mtambwe Kaskazini, Kwa Sharifuali, Darajani Mkoani kwa Pemba.	Kazi imekamilika
7.	Upelekaji wa umeme	Sebleni (SEMUSO)	Kazi imekamilika
8.	Ujenzi wa Tangi	Mnara wa Mbao na Saateni	Kazi imkamilika

iii. **Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)**

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada la *JICA*, umeendelea na kazi ya kuwapatia mafunzo wafanyakazi. Hadi kufikia Machi 2015, jumla ya wafanyakazi 5 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi na 4 nje ya nchi, na wafanyakazi 70 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi na 1 nje ya nchi. Kwa upande wa ukaguzi wa wateja *(Customer survey)* tayari umekamilika kwa Mkoa wa Mijini/Magharibi na kufanya kazi ya kuandaa michoro ambayo inaonesha maeneo yenye mtandao wa maji na yanayotarajiwa kupitishwa mtandao wa maji.

Aidha, kupitia mradi huu Mamlaka ya Maji inaendelea na kazi ya ununuzi na ulazaji wa mabomba na viungo vyake kwa ajili ya kuufanyia marekebisho mtandao wa maji katika maeneo ya Gulioni hadi Makadara.

iv. **Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha *(ADF 12)***

Mhe. Mwenyekiti, hatua za utekelezaji wa mradi huu zimeelezwa katika *paragraph* ya 60 ya hotuba yangu.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka kwa kushirikiana na Mshauri Muelekezi kutoka Kampuni ya *Howard Humphreys* imekamilisha kazi ya kukusanya taarifa na kuzichambua. Kazi ya usanifu wa mradi wa usambazaji maji safi na usafi wa mazingira inaendelea.

Aidha, kazi ya kufanya Tathmini kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa vyoo maskulini imekamilika na hatua zinaendelea ni kusubiri ruhusa ya kufungua nyaraka za zabuni (*financial proposal*) kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

v. **Mradi wa uchimbaji Visima wa *Ras al- Khaimah***

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Uchimbaji wa visima 50 unaofadhiliwa na Mtawala wa *Ras-al-Khaimah* tayari umekamilisha kazi ya uchimbaji wa visima 49 Unguja na Pemba, kazi zilizobakia ni pamoja na Ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji, vibanda vya kuendeshea pampu, ujenzi wa *"Well head"* pamoja na upelekaji wa umeme katika maeneo yote ya Mradi. Jadweli lifuatalo linaonesha idadi ya visima na kazi zilizofanyika:-

Jaduweli nambari 5: Kazi za Uchimbaji wa Visima vya Ras al - Khaimah

Na	Eneo		Idadi		Uchimbaji wa visima	Ujenzi wa matangi	
	Unguja	Pemba	Unguja	Pemba		Unguja	Pemba
1.	Welezo	Shumba viamboni	4	1	Kimekamilika	-	
2.	Kinuni	Mgogoni	3	2	Kimekamilika	-	
3.	Dole	Wingwi	3	1	Kimekamilika	-	
4.	Migombani	Kilindi	1	1	Kimekamilika	-	
5.	Kianga	Chonga	1	1	Kimekamilika	1	
6.	Chumbuni	Mahuduthi	1	2	Kimekamilika	1	
7.	Masingini	Ukutini	1	3	Kimekamilika	-	
8.	Chwaka	Kiwani	1	1	Kimekamilika	-	
9.	Michamvi		1	-	Kimekamilika	1	
10.	Makunduchi		1	-	Kimekamilika	-	
11.	Jumbi Kibonde mzungu		1	-	Kimekamilika	-	
12.	Bambi		1	-	Kimekamilika	-	
13.	Jendele – Marumbi – Chwaka		1	-	Kimekamilika	-	
14.							
15.	Tunguu – Kibele		1	-	Kimekamilika	1	
16.	Cheju		1	-	Kimekamilika	-	
17.	Mzuri		1	-	Kimekamilika	-	
18.	Mtende		1	-	Kimekamilika	1	
19.	Mwera – pongwe		1	-	Kimekamilika	-	
20.	Kiboje		1	-	Kimekamilika	-	
21.	Fuoni kibondeni		1	-		-	
22.	Makunduchi desalination		1	-	Kimekamilika	-	
23.	Banda maji		1	-	Kimekamilika	-	
24.	Upenja –		1	-	Kimekamilika	1	

	Kiwengwa						
25.	Mji mekundu		1	-	Kimekamilika	-	
26.	Kisongoni		1	-	Kimekamilika	-	
27.	Moga		1	-	Kimekamilika	-	
28.	Kitope		1	-	Kimekamilika	-	
29.	Kidanzini		1	-	Kimekamilika	-	
30.	Donge		1	-	Kimekamilika		
	JUMLA		**38**	**12**		**6**	

vi. **Kuvilinda na Kuviwekea Uzio Vianzio vya Maji.**

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa majukumu makuu ya Mamlaka ya Maji ni usimamizi, utunzaji na uhifadhi wa rasilimali maji ambapo hadi kufikia Machi 2015 kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa uzio katika vianzio vya maji katika maeneo ya Kianga N9 1, N9 2, Mwanyanya, Mtoni na Kibuteni kwa Unguja, na Chanjani kwa Pemba. Aidha, Mamlaka imepanda miti katika maeneo ya Kiashange, Nungwi, Machui Kibuteni, Kilombero na eneo la Bumbwini Maji Mekundu kwa Unguja na Tangi la Wambaa, Finya na Bonde la Taifu kwa Pemba.

KAZI ZA KAWAIDA

i. **Matengenezo Ya Miundombinu Ya Maji**

Mhe. Mwenyekiti, mbali na shughuli za kiutawala, Mamlaka ya Maji vile vile imeedeleza kazi utengenezaji wa miundombinu ya maji kwa kuifanyia matengenezo kama inavyoonekana katika jaduweli nambari 6.

Jaduweli nambari 6: Matengenezo Ya Miundo Mbinu Ya Maji

S/no	**Kazi**	**Eneo**
1.	**Kufanya matengenezo ya mabomba**	Migombani, Kianga, Jang'ombe, Mchangani, Dole, Bambi Kihinani, M/Makumbi, Kijangwani, M/Mchomeke, Shaurimoyo, Lumumba, Mpendae, Kijichi, Kwerekwe, Nungwi, Matemwe, Welezo, Kwamtipura, Magogoni, Chunga, Mbweni, Meya Mikunguni, Sogea, B/wawakilishi, Kilimani, Michenzani, Kilimahewa, M/Ladu, Pangawe, M/Miwili, Kinuni, Migombani ikulu, Mwanyanya, Kibweni, Kwamchina, Kombawapya, na Daraja bovu, Matemwe, kilimani, michenzani, Migombani, Meya, Welezo, Melitano, Mkunazini, Elimu Mbadala, Kwarara, Tunguu na Kianaga. Unguja na kwa upande wa Pemba Jamvini, Mjini Chake, Mkoani, Wete,

		Changaweni, Makangale, Kisiwapanza, Konde, Makongwe, Gando, Junguni, Kojani, Pandani na Ole.
3.	**Kufanya marekebisho ya umeme**	Visima vya Kiashange, Kaburi Kikombe, Mwembe Mchomeke No 56 Kibuteni Bumbwini Kidanzini Kiboje Bweleo, Manzese, Mgambo, Muyuni, Chunga No 09 Chwaka Chaani ,Dunga S.S.Metha, Chumbuni, Machui No 6 ,Kibele Mchomeke No 51, Bweleo, Mgambo, Msikiti Mzuri No 10, Msikiti Mzuri 12, Nungwi Kae, Matrekta, Mfenesini, Kinumoshi No 3,4,5, machui, welezo No 2,Mombasa Ofisini, Umbuji, Kitogani, Kianga No 7 na Salem 1.
4.	**Matengenezo ya pampu na mota zilizoungua**	visima vya Bweleo, Machui, KaburiKikombe, Bumbwini Kidanzini, Mombasa Afisini, Mgambo, Kitogani, Mwanyanya, Jendele, Maungani na usafishaji wa visima (Flushing) imefanyika katika maeneo ya M/Mchomeke, Kinyasini Kisongoni na Sebleni kwa wazee, kizimkazi, Masumbani.Bint Amrani no2, Kaburi Kikombe, kwa Unguja na Kwapweza, Gawani Wesha Kisima cha ZECO, Chambani, Ukutini, Kengeja, Michenzani,Ngwambwa, Sharifuali, Mgagadu, Kwabi Mtumwa, Ngombeni, Jondeni, Micheweni-Kironjo-D, Mlindo na Mtambile kwa Pemba.
5.	**Kutoa elimu kwa watumiaji wa maji**	Maeneo hayo ni Muyuni “A”, “B”na “C” Kitogani, Muungoni, Bwejuu, Paje, Mahonda, Kinyasini, Bumbwini Misufini, Kisongoni, Matemwe , Unguja Ukuu Tindini, Unguja Ukuu Kaebona ,Unguja Ukuu Kae Pwani, Dunga, Kizimkazi Dimbani, Kizimkazi Mkunguni, Mkwajuni, Bambi, Mpapa, Mchangani, Mgeni Haji, Uzini, Kiboje, Kigunda, Kivunge, Jambiani Kikadini, Jambiani Kibigija, Michenzani, Kizimbani, Kitogani , Jendele, Bungi, Nungwi, Makunduchi, Kijini na Mtende, kwa Unguja na Pondeani, Kiwani, Ziwani, Birikau, Sizini, Tumbe, Wawi Wesha, Gombani, Mkoroshoni, Chanjaani, Matuleni Madungu, Msingini, Mkanjuni, Kambini, Kangagani, Kiuyu Minungwini, Ole, Piki, Bahanasa, Vikunguni, Mtambwe, Mbuzini, Mfikiwa, Chambani, Uwandani, na Kianga.

ii. **Ukusanyanyaji Wa Mapato**

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2014/2015 ilijipangia kukusanya jumla ya TShs bilioni 4.2. kutokana na mauzo ya maji na

mauzo mengineyo. Hadi kufikia Machi, jumla ya TShs bilioni 2.14 zimekusanywa sawa na asilimia 74 ya makadirio ya makusanyo ya 2.9 kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2014 hadi Machi 2015).

IDARA YA NISHATI NA MADINI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nishati na Madini ni taasisi yenye jukumu la kusimamia Sekta ya Nishati na Madini hapa Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Idara hii ilisimamia na kutekeleza mambo yafuatayo:-

Utekelezaji Wa Mradi Wa Sera Ya Nishati Awamu Ya Pili *(Second Phase)* Na Kuendeleza Mradi Wa Mabadiliko Ya Tabianchi Na Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, Katika utekelezaji wa Sera ya Nishati awamu ya pili Idara ya Nishati kwa kushirikiana na Ubalozi wa Sweden, imetekeleza yafuatayo:-

i. Kukamilisha andiko la Mradi;

ii. Kumaliza taratibu za kuwapata Washauri elekezi; na

iii. Kufungua Akaunti ya Mradi tayari kwa kupokea Fedha za Mradi.

Aidha, Idara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais chini ya mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi chini ya ufadhili wa *UNDP* imeweza kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuweka mifumo *(Solar Panel)* 32 za umeme wa jua katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba;

ii. Kufanya ukaguzi katika maeneo yaliyofungwa mifumo hiyo kwa kutathmini ufanisi *(Monitoring and Evaluation);* na

iii. Kuandaa hati ya muongozo *(guidline document)* na kufanya semina ya kushajihisha matumizi ya miongozo hiyo *(guide-lines)* ya matumizi ya viwango vya kimataifa (*ISO standards)* katika sekta ya nishati.

Kuwapatia Elimu Wananchi Katika Masuala Ya Nishati (Mafuta, Gesi Asilia Na Nishati Mbadala)

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kupitia Idara ya Nishati imetekeleza lengo hilo kwa kuandaa semina za kutoa elimu kwa wananchi juu masuala ya Mafuta na Gesi ambapo jumla ya Semina mbili za ndani kwa wananchi zimefanyika. Aidha, semina tatu zimefanyika kwa kutoa elimu ya Nishati Mbadala kwa wananchi wa

Unguja na Pemba. Vile vile, mikutano maalum ilifanyika katika maeneo yaliyomo katika mradi wa Nishati Mbadala.

Uendelezaji wa utekelezaji wa Mradi wa Nishati Mbadala kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaendelea na azma yake ya kukamilisha Mradi wa Utafiti wa Nishati Mbadala ili kujua uwezekano wa Zanzibar kupata umeme kwa njia mbadala. Idara imekamilisha kazi ya kupatikana kwa mkandarasi (Kampuni ya *AGMIN* ya Italy) wa ujenzi wa minara ambae tayari ameanza kazi hiyo. Aidha, Mshauri elekezi wa ukusanyaji wa tarifa hizo pamoja na kutayarisha ripoti ya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* ambayo inatarajiwa kumalizika mwaka 2017.

Kushiriki katika masuala yote ya nishati ya Kitaifa, Kikanda, na Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa hili, Idara imeweza kushiriki katika mikutano mbali mbali iliyofanyika ndani na nje ya nchi kama vile;

i. Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika masuala ya Nishati ya Umeme (Nairobi, Entebe), Mkutano mkuu wa Mafuta na Gesi wa Afrika Mashariki *(EAPCE 2015)* uliofanyika Kigali - Rwanda.

ii. Kuhudhuria katika Mkutano wa kuitangaza Tanzania katika utekezaji wa masuala ya Nishati (Den Hague - Uholanzi).

iii. Ushiriki katika Maonesho na Warsha ya Nishati mbadala – Kahama, Tanzania.

Kuendelea Kusimamia Upatikanaji Wa Mafuta Zanzibar (Dizeli, Petroli Na Mafuta Ya Taa).

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya upatikanaji wa mafuta Zanzibar yameelezwa katika paragraph ya 70 hadi 72 ya hotuba yangu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha nishati ya mafuta inapatikana nchini, Idara ya Nishati inaendelea kufuatilia shughuli za kusimamia upatikanaji wa mafuta na kusimamia utekelezwaji wa ratiba za uagizaji wa mafuta nchini kwa makampuni yote manne makubwa *(GAPCO, UP, ZP* na *PUMA)*. Kwa ufafanuzi zaidi angalia Kiambatanisho ”F”

Mhe. Mwenyekiti, katika kulisimamia hili, dosari za uagizishaji wa bidhaa ya mafuta ya Petroli zilijitokeza baina ya mwezi wa Februari na Machi. Dosari hizo zilichangiwa na mambo yafuatayo;

i. Kuchelewa kwa meli ya mafuta ya pamoja (*Bulk Consignment)* inayoleta mafuta nchini Tanzania.

ii. Kushuka kwa kiasi kikubwa bei ya petroli kumechangia kwa kiasi fulani matatizo ya upatikanaji wa bidhaa hio kutokana na kuongezeka kwa matumizi na hasa baada ya kujitokeza uwezo mdogo wa makampuni kukabiliana na mahitaji katika kipindi hicho kwa kuzingatia makampuni hayo yalikwisha agiza bidhaa hio. Ni kawaida kuwa bidhaa hizi huagiziwa na kulipiwa kabla ili bidhaa hio ifike tarehe ilokusudiwa.

iii. Matengenezo makubwa ya matangi ya mafuta yaliyofanywa na kampuni ya *UP* katika kipindi hicho ambayo yalichangia kwa kiasi upungufu wa akiba ya mafuta.

iv. Kutokuwepo na miundombinu ya kutosha ya matangi ya akiba ya mafuta inayoweza kukabiliana na hali kama hiyo inapojitokeza.

v. Tatizo la miundombinu ya bandari ya Mtoni yenye kina kidogo na kutokukidhi meli zenye uwezo mkubwa zaidi kushusha bidhaa hizo. Hii hupelekea kutumika meli ndogo zilizopo ambazo hulazimika kufanya safari nyingi katika bandari za Dar es salaam na Mombasa na kukabiliwa na matatizo ya kufunga nanga katika bandari hizo kutokana na kuwepo na meli nyingi zinazosubiri huduma kama hio. Hii huwa tatizo kubwa katika kipindi kinachotokea uhaba wa bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, Hali hiyo iliyojitokeza ni kiashiria tosha cha kusisitiza umuhimu wa kuwepo kwa Taasisi Maalum ya kushughulikia sekta binafsi inayoendesha biashara ya mafuta kwa kutumia sheria yake. Hili kwa bahati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ililiona kabla na kuchukua uamuzi wa kuanzishwa kwa Mamlaka Maalum ambayo itadhibiti biashara ya Mafuta Nchini. Ni imani yangu kwamba kuanza kazi kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (*ZURA*) kutaweza kwa kiasi kikubwa kudhibiti hali hiyo hapo baadae.

Kukamilisha Utayarishaji Wa Sheria Ya Kusimamia Usambazaji Wa Mafuta *(Petroleum Supply Act)*.

Mhe. Mwenyekiti, Rasimu ya sheria hiyo ilifikishwa katika kikao cha Kamati ya Makatibu Wakuu ambao walitoa michango yao katika kuendeleza kazi hiyo mnamo mwezi wa Julai 2014. Katika kikao hicho kulipendekezwa marekebisho kadhaa kufanyika yakiwemo kuhamisha baadhi ya vifungu vya Rasimu ya sheria hiyo na kuvipeleka katika Kanuni za Sheria ya *ZURA*. Vifungu vilivyobakia vya sheria hiyo vitaingizwa katika sheria ya nishati inayotarajiwa kutayarishwa chini ya mradi wa *SIDA*.

Kuendelea Kushirikiana Na Washirika Wa Maendeleo Katika Kuimarisha Na Kutekeleza Mipango Ya Mafunzo Ya Mafuta Na Gesi Asilia Pamoja Na Matayarisho Ya Sera Na Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, Katika jitihada za kushirikiana na washirika mbali mbali wa maendeleo, Idara imefanikiwa kuendesha semina kumi (10) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 zinazohusiana na masuala ya Mafuta na Gesi Asilia ambazo ziliwashirikisha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na watendaji wa Taasisi mbali mbali za Serikali.

Kujiimarisha Na Utafiti Na Matumizi Ya Teknolojia Za Nishati Mbadala Kwa Kushirikiana Na Washirika Wa Maendeleo Na Taasisi Mbalimbali Za Nje Na Ndani Ya Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hatua ya mwanzo Serikali imeanza kushirikiana na Jumuiya ya *EU* katika kuendeleza utafiti wa nishati hizo. Vile vile, Idara imeanza mawasilisano ya awali na Taasisi ya Nishati mbadala Tanzania *"Tanzania Renewable Energy Association–TAREA"* na kushiriki katika warsha na maonesho yaliyofanywa na Taasisi hiyo katika jitihada ya mashirikiano baina ya Taasisi hizi mbili. Aidha, mafunzo maalum yanafanyika kwa kila mwaka nchini China na mara hii wataalamu wanane (8) walishiriki katika mafunzo hayo. Jitihada zaidi za mawasiliano zinaendelea kuchukuliwa kwa kufungua mawasiliano ya mashirikiano na Taasisi nyengine za Kimataifa katika nyanja za Teknolojia za Nishati mdala.

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika la Umeme lilijipanga kutekeleza kazi za Usambazaji, Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme Mjini na Vijijini kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2014-2015, Shirika lilikadiria kukusanya Tsh. 86,967,505,739.00 kutokana na Biashara ya kuuza umeme na huduma nyenginezo zinazotolewa kwa wananchi ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 Shirika limekusanya jumla ya Tsh. Billioni 58.2 sawa na asilimia 67 ya makadirio.

MATUMIZI

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilikadiria kutumia Tsh. 86,431,974,390.00. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 Shirika limetumia Tsh. Billioni 57.2 sawa na asilimia 66.2 ya makadirio kama inavyoonekana katika Jaduweli Nam.7 lifuatalo:-

Jaduweli nambari 7: Matumizi ya Shirika la Umeme

MAELEZO	**MAKADIRIO 2014-2015**	**MATUMIZI HALISI 2014-2015**
Ununuzi wa Umeme TANESCO	53,412,842,363.00	34,218,635,395.98
Kazi za Kawaida	25,595,723,447.00	12,062,405,592.28
Kazi za Maendeleo	7,423,408,580.00	10,947,731,002.00
Jumla	**86,431,974,390.00**	**57,228,771,990.26**

Utekelezaji wa Kazi za Kawaida:-

Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika limebadilisha waya chakavu kilomita 34.8 na nguzo mbovu 1,247 katika maeneo ya Mijini na Vijijini. Vile vile, limepima transfoma 385 na kuzifanyia marekebisho ili kuhakikisha kwamba hali ya upatikanaji wa huduma ya Umeme inakuwa bora wakati wote.

Utekelezaji wa Miradi

Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Jumla ya Tshs. 4,326,338,405.00 zilitumika kwa ununuzi wa vifaa vya umeme, waya, nguzo, transfoma pamoja na kulipa fidia ya mali na mazao ya wananchi. Kati ya fedha hizo, Tshs. 230,000,000.00 ni mchango wa mfuko wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tshs. 4,096,338,405.00 zimetokana na mfuko wa *ZECO*.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi hicho, Shirika limejenga kilomita 61.5 laini ndogo ya Umeme na kilomita 36.7 ya umeme mkubwa pamoja na uwekaji wa transfoma za kusambaza umeme katika Vijiji 62 kwa Unguja na Pemba. Sambamba na kazi hizo, Shirika limejenga kilomita 5.9 ya laini kubwa, kilomita 6 ya laini ndogo ya umeme pamoja na kuweka transfoma tatu (3) Kisiwa Panza na Makoongwe. Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali angalia Jaduweli Nam.8 lifuatalo:

Jaduweli nambari 8: Vijiji vilivyobahatika kusambaziwa Umeme

UNGUJA	**PEMBA**	
DOLE NDUNDUKE	BANANI	MICHUNGWANI
DONGONGWE	CHANJAANI MTAMBWE	MISOONI
FUKUCHANI	CHANJAMJAWIRI	MWAMKE KINUNDU
FUONI CHUNGA	CHOKOCHO KISIWA PANZA	MZAMBARAUNI
FUONI MELI TANO	GONGO MAWE	NG'AMBWA
FUONI MICHENZANI	JOJO	PIKI KISIMA CHA MAJI
GHANA	KIBOMANI KISIMA CHA MAJI	SHANGAFU KISIMA CHA MAJI
KIBELE	KIFUMBIKAI WETE	SUMBUKA OLE
KILOMBERO	KIMBUNI	TIRONI
KISAUNI	KISIWA PANZA	TUMBE
KIZIMBANI KISIMA CHA MAJI	KIVUNGO	VIKUNGUNI KISIMA CHA MAJI
KWA GWIJI	KOJANI	UCHOZINI
KWARARA KWA	KWA CHANGAWE	UWONDWE

TOBI		NAMAMOJA
MBIJI KISIMA CHA MAJI	KWASAANANI	UWONDWE
MKUKU DONGONGWE	LIKONI KENGEJA	WAMBAA KISIMA CHA MAJI
MVULENI	MAKOONGWE	WINGWI KIDODI
MWERA MABATINI	MANYAGA	WINGWI MJANAZA
TUNGUU MJI MPYA	MAWENI	WINGWI MJANANZA KILINENI
UPENJA KIPANDONI	MAZIWA NG'OMBE	WINGWI MTAKUJA
ZINGWEZINGWE	MCHANGA MDOGO	WAWI MJI WA CHINI
	MGAGADU KISIMA CHA MAJI	
	MICHEWENI	

Mradi wa Ufungaji wa Mita za TUKUZA

Mhe. Mwenyekiti, Lengo kuu la mradi ni kukuza ukusanyaji wa mapato ya Shirika na kupunguza malimbikizo ya madeni. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 Shirika limenunua mita 23,600 za TUKUZA kwa gharama ya Tshs. 2,048,037,756. Kati ya hizo, Mita 7,482 zimefungwa kwa Wateja wapya na Mita 5,685 zimebadilisha Mita za kawaida na mbovu.

MUELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeamua kufanya mageuzi ya bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma. Mageuzi hayo ni kutoka mfumo unaotumia vifungu *(line item)* kwenda katika mfumo unaotumia programu *(Programme Based Budgeting)* ambao unaangalia zaidi matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Inategemewa kuwa kuingia katika mageuzi hayo ya mfumo

wa bajeti italeta uwiano mzuri wa Sera za Taifa katika bajeti pamoja na kuweka uwazi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima naomba kuwasilisha muelekeo wa Bajeti yenye kuzingatia programu ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ina jumla ya Programu Kuu nne ambazo ni;

Programu 1:	Mipango, Sera na Utawala wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.
Programu 2:	Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi.
Programu 3:	Uhifadhi wa Mji Mkongwe, Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi na Nyumba za Serikali.
Programu 4:	Usimamizi wa Huduma za Uzalishaji na Usambazaji wa Nishati na Maji.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya Tsh bilioni 35,949,460,587.00 zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wa Programu hizi nne.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu kutoa maelezo kwa ufupi kuhusu Programu ndogo zinazohusiana na wizara yangu kama ifuatavyo.

Programu ya Mipango, Sera Na Utawala Wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inajukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa kazi za wizara ambapo matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kukuza ufanisi katika utawala wa rasilimali ardhi pamoja na utoaji huduma za kijamii.

Programu itasimamiwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Afisi Kuu Pemba ambapo jumla ya Tsh. 1,984,365,000.00 zinatarajiwa kutumika kwa utekelezaji wake.

Programu hii inatekeleza lengo la MKUZA II la kuhakikisha ushirikishwaji mkubwa wa watu katika serikali ya kidemokrasia. Aidha, programu hii imegawanyika katika Programu ndogondogo kama ifuatavyo:

i. **Mipango na Sera za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la Programu ndogo hii ni Uratibu wa Shughuli na Kazi za Wizara kwa Ufanisi, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni Kuratibu/Kuandaa Mipango na Miongozo ya Kisera ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Programu, Miradi na shughuli za Wizara na Kuandaa Tafiti kwa ajili ya Kuendeleza ufanisi katika utoaji wa huduma katika sekta za Wizara. Jumla ya Tsh 161,884,000.00 zinatarajiwa kutumika.

UTARATIBU

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kutenga Kanuni kando. Kwa idhini ya Baraza yoyote kati ya Kanuni hizi yanaweza kutengwa kando kwa madhumuni mahususi baada ya Mjumbe yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, humu ndani Wajumbe tumo kidogo na inaonekana kama tumechoka na muda tunao wa kutosha wa kuendelea na shughuli zetu. Kwa hivyo, mimi ningeomba tukapata muda mwingine kesho, Mhe. Waziri, akaahidi kuendelea na muda upo wa kutosha, Kanuni ya 156. Wajumbe tuliomo humu ndani ni kidogo, kwa hivyo, tuweke Kanuni kando na muda wa bajeti tunao wa kutosha kwa siku zilizokuwepo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Kanuni haijamruhusu Mhe. Waziri, kwamba asisome kwa mujibu wa alivyoona yeye inawezekana kufahamisha. Kitabu hiki tunaweza tukakisoma sisi wote baadae na sio lazima *exactly* Mhe. Waziri, asome kama ilivyo.

Kwa hivyo, tumuache Mhe. Waziri, aendelee, tunataka kumaliza muda unakwenda. Kwa hivyo, nakuomba tumuache waziri aendelee. Mhe. Waziri, endelea.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti,

i. **Mipango na Sera za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la Programu ndogo hii ni Uratibu wa Shughuli na Kazi za Wizara kwa Ufanisi, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni Kuratibu/Kuandaa Mipango na Miongozo ya Kisera ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Programu, Miradi na shughuli za Wizara na Kuandaa Tafiti kwa

ajili ya Kuendeleza ufanisi katika utoaji wa huduma katika sekta za Wizara. Jumla ya Tsh 161,884,000.00 zinatarajiwa kutumika.

ii. **Utawala na Maendeleo ya Rasilimali watu**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni kuhakikisha usimamizi thabiti na utawala wa rasilimali za Wizara, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii, ni Kukuza Viwango vya Wafanyakazi na kuhifadhi kumbukumbu na Taarifa za Wafanyakazi wa Wizara. Jumla ya Tsh 804,252,000.00 zinatarajiwa kutumika.

iii. **Uratibu wa Shughuli za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Pemba**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni Uratibu na Usimamizi Thabiti wa Kazi za Wizara kwa pemba, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii, ni Kuratibu Shughuli za Mipango na Utawala pamoja na Kuratibu na Kusimamia masuala ya Ardhi, Makaazi maji na Nishati Pemba. Jumla ya Tsh 1,018,229,000.00 zinatarajiwa kutumika.

Programu ya Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inajukumu la kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya nchi (*Security of land tenure*). Matokeo ya muda mrefu yanayotarijiwa ni kuwa na matumizi ya ardhi yaliyobora na fanisi.

Programu hii inasimamiwa na Idara ya Ardhi na Usajili, Afisi ya Msajili wa Ardhi, Mahakama ya Ardhi, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Mipango Miji na Vijiji ambapo jumla ya Tsh. 1, 281,996,000 zinatarajiwa kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekeleza lengo Kuu la MKUZA II la kuwa na mazingira bora ya ukuaji uchumi na kuwa na makaazi bora ya kutosheleza na endelevu. Aidha, programu hii imegawanyika katika Programu ndogo ndogo kama ifuatavyo:

i. **Utawala wa Ardhi**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la Programu ndogo hii ni kuhakikisha Usalama wa Umiliki wa Ardhi kwa Wananchi, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni ugawaji na usimamiaji wa ardhi kwa matumizi mbali mbali,Uthamini wa ardhi, Usimamiaji wa shughuli za

Upimaji na Ramani, Usajili wa ardhi pamoja na Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi. Jumla ya Tsh 1,011,941,000.00 zinatajaiwa kutumika.

ii. **Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni Kuhakiksha Kunakuwepo Uwiano wa matumizi ya Ardhi, kati ya Matumizi ya Uchumi na Kijamii, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii, ni kuwepo kwa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa Miji yote ya Zanzibar, Kusimamia Maendeleo ya Ardhi Mijini, Mikoani na maeneo ya Fukwe, Kuimarika kwa Miji ili Kukuza Uchumi na Kuleta Maisha Bora. Jumla ya Tsh 270,055,000.00 zinatajaiwa kutumika.

Programu ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe, Uratibu na Usimamizi wa Ujenzi na Nyumba za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina jukumu la kusimamia shughuli za ujenzi wa nyumba na uhifadhi wa Mji Mkongwe. Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni upatikanaji wa makaazi bora na yenye gharana nafuu kwa Wananchi wote pamoja na kulinda na kuhifadhi Mji Mkongwe kama urithi wa kihistoria.

Programu hii itasimamiwa na Idara ya Ujenzi, Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Jumla ya Tsh 1,117,901,000.00 zinatarajiwa kutumika kwa utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inatekeleza lengo la MKUZA II la kuwa na makaazi bora ya kutosheleza na endelevu na kushajihisha michezo, kuendeleza, kulinda na kuhifadhi urithi wa kihistoria na utamaduni wa asili. Aidha, programu hii imegawanyika katika Programu ndogo ndogo kama ifuatavyo:

i. **Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi na Nyumba za Serikali**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni kuhakikisha ujenzi wa makaazi bora, salama na nafuu kwa jamii, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii, ni usimamizi wa nyumba za serikali, kupokea na kutolea maamuzi mashauri ya nyumba yanayowasilishwa, kuratibu na kusimamia shughuli za ujenzi na kufanya matengenezo ya ofisi na nyumba za serikali. Jumla ya Tsh 757,854,000.00 zinatarajiwa kutumika.

ii. **Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar kiutamaduni na kihistoria, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wake, ni Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na usimamizi wa maeneo ya wazi ndani ya Mji Mkongwe. Jumla ya Tsh 360,047,000.00 zinatarajiwa kutumika.

Program ya Usimamizi wa Huduma za Uzalishaji na Usambazaji wa Nishati na Maji

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la programu hii ni kuhakikisha kunakuwepo upatikanaji wa Huduma za Nishati na Maji inayotosheleza mahitaji ya watu. Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni upatikanaji wa huduma bora za nishati, umeme na maji kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii itasimamiwa na Idara ya Nishati na Madini, Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Maji na Nishati, Shirika la Umeme na Mamlaka ya Maji ambapo jumla ya Tsh. 31,565,198,587.00 zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wake.

Programu hii inatekeleza lengo la MKUZA II la kuwa na mazingira bora ya ukuaji uchumi na kustawisha ukuaji wa uchumi uliyo endelevu na unaozingatia umaskini uliokithiri pamoja na lengo la kuimarisha huduma za maji na usafi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii ni usimamizi wa usambazaji wa mafuta nchini, usambazaji wa huduma za Umeme, uhifadhi wa maeneo ya vianzio vya maji, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa watumiaji mijini na vijijini.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuwatumikia wananchi wenzangu kupitia wizara hii kwa kipindi cha miaka mitatu kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wizara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mashirika ya Kimataifa na yasiyo ya Kimataifa, Sekta binafsi, *NGOs*, *CBOs* na wananchi kwa jumla kwa mashirikiano makubwa waliyoyaonesha kwa Wizara yangu kwa misaada yao ya hali na mali waliyoitoa na wanayoendelea kutoa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara hii. Washirika hao ni JAPAN, NORWAY,

SWEDEN, MAREKANI, CHINA, EGYPT, OMAN, FINLAND, *UNICEF*, *UNESCO*, *UNDP*, *JICA*, Sida, *UN HABITAT*, *AfDB*, *TASAF*, *NORAD*, *ACRA*, BENKI YA DUNIA, UBELGIJI, *RAK GAS* TANZANIA, *EU*, *MCC*, pamoja na wale wote ambao kwa bahati mbaya hatukuweza kuwataja. Tumepata faraja kubwa sana kwa michango yao kwa maendeleo ya nchi yetu, tunaahidi kuienzi na kuiendeleza na kuithamini michango hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa namalizia muda wangu katika Wizara hii, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein; kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kuiongoza wizara hii pamoja na miongozo yake mbali mbali aliyokuwa inaitowa, ambayo imeimarisha sekta muhimu zenye kugusa maisha ya kila siku kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Aidha, naomba kumshukuru Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad pamoja na Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa msaada wao na maelekezo walionipa katika kipindi chote cha uwongozi wangu katika Serikali ya Awamu ya Saba. Wote nawaombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na maisha marefu pamoja na familia zao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, shukurani za pekee kwa Mhe. Spika, Naibu Spika, Mhe. Mwenyekiti wa Baraza, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza na Waheshimiwa Wajumbe wote, kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, shukurani maalumu nazitoa kwanza kwa mwenzangu na ndugu yangu, Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ndugu Haji Mwadini Makame, kwa mashirikiano yake makubwa alionipa katika kuongoza wizara hii. *(Makofi)*

Vile Vile, shukurani kwa Katibu Mkuu ndugu Ali Khalil Mirza, Naibu Katibu Mkuu ndugu Mustafa Aboud Jumbe, Afisa Mdhamini ndugu Hemed Salim Hemed, ambao walinipa mashirikiano yao ya hali juu kwa wakati wote katika kuendesha, kutekeleza na kuongoza kazi ambazo wizara hii nilikabiliwa nazo. *(Makofi)*

Aidha, msaada mkubwa walionipa Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi, Mameneja, Mahakimu na viongozi wote wa ngazi za mbali mbali, pamoja na watendaji wote wa wizara ni ushahidi wa ukakamavu wao katika kuitumikia nchi hii, namuomba Mwenyezi Mungu awaajalie wote na familia zao afya njema na maisha marefu, *Amin*. Napenda kukiri mbele ya hadhara hii kuwa timu hii ya uongozi sitoweza kuisahau katika maisha yangu yote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sijatimiza wajibu wangu bila ya kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu, ambao kwa wakati wote walikuwa karibu sana katika kunishauri na kunipa nasaha, ambazo hatimae zimezaa matunda ya ufanisi katika wajibu wangu mbele ya Baraza lako tukufu na wananchi wa Zanzibar. Mwenyezi Mungu atujaalie tufanikiwe tena kurudi katika Baraza hili kwa adhma ya kuitumikia nchi hii, kwa moyo wa umoja na upendo, *Amin.* Aidha, kwa kuwa hakuna mkamilifu zaidi ya Mwenyezi Mungu, ninawaomba wenzagu mnisamehe pale nilipowakosea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba uniruhusu kuishukuru familia yangu yote kwa msaada walionipa na ustahamilivu wao, hasa pale nilipokosekana katika matukio ya kifamilia kutokana na wajibu wangu wa kuwatumikia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wayapokee, wayajadili kwa kina, watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, ili wizara yangu iweze kutekeleza programu kuu na programu ndogo nilizozieleza, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Tsh Bilioni 35,949,460,587.00 na pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Tsh Bilioni 4,799,625,000.00 kutokana na vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2015/2016.Kwa ufafanuzi zaidi nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, waangalie Kiambatanisho “G1 na G2”.Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja Ilitolewa iamuliwe)

KIAMBATANISHO "A"

MUHTASARI WA MAKUSANYO YA FEDHA ZA MAPATO
JULAI 2014 - MACHI 2015

	MAELEZO	MAKISIO 2014/15	MAKUSANY JULAI/M
	AFISI KUU PEMBA	233,600,000	
	IDARA YA UJENZI	11,300,000	
	MAMLAKA YA MJI MKONGWE	23,000,000	
	IDARA YA ARDHI NA USAJILI	3,510,000,000	2
	IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI	85,000,000	
	IDARA YA NYUMBA NA MAKAAZI	524,000,000	
	MRAJIS WA ARDHI	30,000,000	
	JUMLA	**4,416,900,000**	**2**

KIAMBATANISHO "B1"

MUHTASARI WA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA MAENDELEO
JULAI 2014- MACHI 2015 (MCHANGO WA SMZ)

	MAELEZO	MAKISIO 2014/15	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI	Z
	USAMBAZAJI MAJI VIJIJINI	550,000,000	428,792,261	
	UHUISHAJI NA UPANUZI WA MAJI MIJINI	600,000,000	100,000,000	
	UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA MAJI MJINI MAGHARIB	350,000,000	80,000,000	
	MRADI WA KUIJENGEA UWEZO M/MAJI	500,000,000	500,000,000	
	USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI	1,486,000,000	230,000,000	
	UTAFITI WA NISHATI MBADALA	219,000,000	70,000,000	

	SERA YA NISHATI	75,000,000	15,000,000	
	USIMAMIZI ENDELEVU WA A/MAZINGIRA (SMOLE)	170,000,000	70,000,000	
	JUMLA	**3,950,000,000**	**1,493,792,261**	

KIAMBATANISHO "B2"

MUHTASARI WA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA MAENDELEO
JULAI 2014- MACHI 2015 (MCHANGO WA WAHISANI)

AELEZO	**MAKISIO 2014/15**	**FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI**	**TAFAUTI YA ZILIZOPATIKANA**
A MIUNDOMBINU YA HARIBI	11,576,478,000	234,351,751	11,342,126,24
ENGEA UWEZO M/MAJI	92,910,000	0	92,910,00
A MIUNDOMBINU HIRIZI ZANZIBAR	4,200,000,000	0	4,200,000,00
ENGEA UWEZO NA YA MIUNDOMBINU YA	3,927,702,000	0	3,927,702,00
HATI MBADALA	1,621,600,000	262,269,986	1,359,330,01
TI	652,000,000	0	652,000,00
ELEVU WA MOLE)	778,168,000	2,278,120,679	-1,499,952,67
	22,848,858,000	**2,774,742,416**	20,074,115,58

KIAMBATANISHO "B3"

MUHTASARI WA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA KAWAIDA
JULAI 2014 - MACHI 2015

MAELEZO	MAKISIO 2014/15	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MARCH 2014/15	TAFAUTI YA FEDHA ZILIZO- PATIKANA	% Y ZIL
KUU PEMBA	1,174,445,600	613,069,300	561,376,300	
GO SERA NA UTAFITI	2,470,739,000	1,854,766,505	615972,495	
YA UJENZI	551,545,400	370,153,650	181,391,750	
KONGWE	372,465,600	256,868,816	115,596,784	
YA NISHATI	676,735,400	278,428,992	398,306,408	
YA ARDHI NA LI	263,051,600	167,664,100	95,387,500	
YA UPIMAJI	420,761,800	276,078,300	144,683,500	
YA NYUMBA	253,098,800	146,411,400	106,687,400	
AMA YA ARDHI	173,553,200	134,163,250	39,389,950	
ISHI NA UEMDESHAJI	941,798,600	585,467,709	356,330,891	
LI WA ARDHI	183,772,000	107,355,400	76,416,600	
GO MIJI NA VIJIJI	278,133,000	168,138,783	109,994,217	
A	**7,760,100,000**	**4,958,566,207**	**2,801,533,795**	

KIAMBATANISHO "C"

WAFANYAKAZI WALIOPATA MAFUNZO YA MUDA MREFU JULAI 2014 - MACHI 2015

NO	TAASISI	W/UME	W/WKE	JUMLA	CHUO	AINA YA MAFUNZO
1	**UTUMISHI NA UENDESHAJI**	1		**2**	ICPS ZANZIBAR	DIPLOMA IN HUMAN RESOURCE MANAGEMENT
		1			MUSLIM UNIVERSITY MOROGORO	DEGREEOF MASS COMMUNICATION
2	**NISHATI NA MADINI**	1	3	**4**	IPA	DIPLOMA IN IT
						DIPLOMA IN SECRETARY
						DIPLOMA IN PUBLIC ADMINISTRATION

					ZU	DEGREE PUBLIC ADMINISTRATION
3	**UPIMAJI NA RAMANI**	1		**2**	ARDHI UNIVERSITY	MASTER IN GEOMATICS
		1				DEGREE OF GEOMETRICS
4	**MAMLAKA YA MAJI**	2		**71**	KIU	BBA
		2			KARUME TECH	CHETI CHA UFUNDI BOMBA
		1			JKU	CHETI CHA UFUNDI BOMBA
			1		ICPS ZANZIBAR	RECORD MANAGEMENT
			1		INDIA	BBA
		1			KIU	MASTER IN PUBLIC ADMINISTRATION
		1			KARUME TECH	PLUMBER
		1			KIU	BBA
		31	3		WDS	WATER DEVELOPMENT
		26	1			
5	**MIPANGO MIJI NA VIJIJI**	1		**5**	CHUO CHA ARDHI	MASTER IN PLANNING
		1				DEGREE IN IT
			1		IPA	DIPLOMA IN BUSNESS AND IT
			1		SUZA	DEGREE IN IT
			1		UNIVERSITY IN COVENTRY MATER	FINANCE AND INVESTIMENT
6	**MRAJIS WA ARDHI**	1	1	**2**	OCEAN UNIVERSITY OF CHINA	MASTER OF ENVIROMENTAL & RESUORCE PROTECTION LAW
7	**IDARA YA UJENZI**	1		**2**	ICPS ZANZIBAR	PROCUREMENT AND SUPPLY
		1			ZANZIBAR UNIVERSITY	MASTER IN HUMAN RESOURCE
8	**MAHAKAMA YA ARDHI**	1		**11**	CHUO CHA UTALII	DIPLOMA IN IT AND ACCOUNTANTS
			1		ICPS ZANZIBAR	DIPLOMA IN SECRETARY
			1			CERTIFICATE IN ACCOUNT
			1			CERTIFICATE RECORD MANAGEMENT
		1			ISLAMIC UNIVERSITY OF MALAYSIA	DOCTOR PHYLOSOPHY IN LAW
		1			BAGAMOYO UNIVERSITY	DEGREE IN LAW

			1		ZANZIBAR UNIVERSITY	DEGREE IN LAW
			1			DEGREE IN LAW
			1		KIU	DEGREE IN LAW
			1		ZIBRET	ICT CERTIFICATE
			1		IPA	CERTIFICATE SECRETARY
9	**MAMLAKA YA MJI MKONGWE**	1		**1**	DIT	SHAHADA YA UHANDISI
			1	**1**	IPA	DIPLOMA IN HUMAN RESOURCE
		1		**1**		DIPLOMA IN IT
		1			ZANZIBAR UNIVERSITY	MASTER IN HUMAN RESOURCE
10	**NYUMBA NA MAKAAZI**	**1**			INSTITUTE OF SCIENCE AND TECHNOLOGY	BUILDING AND CIVIL ENGINEERING
		1		**3**	ZANZIBAR UNIVERSITY	BUSINESS INFORMATION TECHNOLOGY
			1		DAR ES SALAAM INSTITUTE OF SCIENCE AND TECHNOLOGY	BUILDING AND CIVIL ENGINEERING

11	**SHIRIKA LA UMEME**	1			ZANZBAR UNIVERSITY	TEL ENG
		1			INSTITUTE OF PROCUREMENT & SUPPLY	DIP
			1		ZANZIBAR UNIVERSITY	DIP FIN
		1			ALMAKTOUM COLLEGE OF ENGINEERING	DIP ENG
		3				
		1	1		OF HOTEL & BUSINESS STUDIES	CER ADM
			1	**25**	INSTITUTE OF PUBLIC ADMINISTRATION	DIP
		2			ST. JOSEPH UNIVERSITY	BAC ENG
			1		ZANZIBAR UNIVERSITY	BAC ADM
		1				BAC
			1			BAC ADM
		1			C.B.E	BAC
		1			ESAMI	MA ADM
		1			DAR-ES-SALAAM INSTITUTE OF	MA MA

					TECHNOLOGY	
		1			ZANZIBAR UNIVERSITY	MA ADM
		1			MZUMBE UNIVERSITY	MA
		1	1			MA SUP
		1			ZANZIBAR UNIVERSITY	DIP
		1			TUMAINI UNIVERSITY	DIP
		1			OPEN UNIVERSITY	PHD
12	**AFISI KUU PEMBA**	1			ZANZIBAR UNIVERSITY	MA ADM
			1			DEC ENC
		1			TMBI – DARE ES SALAAM	DEC
		1				DEC MA
		1			UNIVERSITY OF BAGAMOYO	DEC
		1			DAR ES SALAAM COLLEGE OF HOTEL AND BUSINESS STUDIES	DIP MA
			2			DIP ANI
		1	1			DIP
		1				DIP
			1			DIP SUP
			2	**24**		CER MA
		1	1			CER ANI
		1				CER MA
			1		IPA	DIP ADM
		1				CER ADM
			1		ZCBE – VITONGOJI	CER ANI
		1				DIP SUP
		1			CHUO CHA UFUNDI DODEANI	CER JOI
		1			CHUO CHA MAFUNZO YA AMALI VITONGOJI	CER BRI
			1		ARDHI UNIVERSITY	DIP ANI
	JUMLA KUU	**114**	**40**	**154**		

KIAMBATANISHO "D"

WAFANYAKAZI WALIOPATA MAFUNZO YA MUDA MFUPI KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015

	AINA YA MAFUNZO	W/UME	W/WAKE	JUMLA
	ICT		1	1
	PROCUREMENT		1	1
MEME	ADVANCE DRIVER INDUSTRIAL	3		3
	AUDITING FOR HR	1		1
	TELEPHONE OPERATOR	1		1
	NET WORK MANAGEMENT AND MONITORING	1		1
	RETIREMENT COURSE	7	3	10
	MANAGEMENT	1		1
	STORE MANAGEMENT SKILL AND METHOD	1	2	3
	PLANNING APPRAISAL AND FINANCE MANAGEMENT OF POWER PROJECT	2		2
	PROJECT DEVELOPMENTAND METHOD	1		1
	SAP PROGRAM	1	1	2
	SUPRIMA	3		3
	PERSONNEL SKILL PROCEDURE	1		1
	REGISTRY SKILL AND METHOD	1	5	6
	FIRE PROTECTION	49		49
	KEY PERFORMANCE INDICATOR	28	2	30
	KEY PERFORMANCE INDICATOR	1	1	2
	CUSTOMER CARE MANAGEMENT	41	19	60
	PRINCIPLES OF APPLICATION OF AUTO CARDS		1	1
	NBAA	1		1
	MANAGERIAL SKILLS	1		1
	ACCOUNTING STANDARD METHOD	1		1
	OFFICE SECRETARIAL METHOD		5	5
	ADVANCE BUGETING SKILLS AND METHODS	1	1	2
	ENTERPRENURSHIP		2	2
	SEMINAR	1		1
	ARTISAN	3		3
	ISP CENTER	1	1	2
	MAINTENANCE& PROTECTION OF EHU SUATATION	1		1
	RELAY SURVEY	6		6
	METERING BILLING AND LOSS REDUCTION	4		4
	RECORDING SKILLS	1		1
	COLLECTION OF ACCOUNTING RECEIVABLE	1	1	2
	RECORDS KEEPING		1	1
	INTERMIDIATE ELECTRICAL COURSE	1		1
	LAND SURVEY	2	2	4
	PROCUREMENT& SUPPLY CHAIN AUDIT	1		1
	EFFICIENT ENERGY USE & PLANNING	1		1
	OFFICE ASSISTANT	1		1
	SUPERVISORY SKILLS& METHODS	4		4

	OFFICE CLERK	1	1	2
	BEST PRACTICE IMPROVE DISRIBUTION	1		1
MAJI	TRAINING PASTEL	9	2	11
	INFRASTRUCTUREPROJECT RISK MANAGEMENT	1		1
	OPERATION AND MAINTENANCE OF URBAN WATER SUPPLY	1		1
	DATA BASE ADMINISTRATION	1		1
	CREDIT CONTROL AND ACCOUNT	1		1
	PIPE TECHNOLOGY	9		9
	MANAGEMENT INFORMATION SYSTEM	3	2	5
	IELTS PREPARATION WORK SHOP	1		1
	BLIND TOUCH TRAINING	3	3	6
	WORK SHOP SEMINOR CUSTOMER CARE		1	1
	AFRICAN REGION URBAN WATER WORKS ENGINEERING	1	1	2
	ENHANCE OF WATER SUPPLY MANAGEMENT OF ZAWA	1	1	2
	MANAGEMENT	1		1
	DATA LOG	3	3	6
AMANI	MAFUTA NA GESI	1		1
MBA	ENERGY SAVING AND EMISSION REDUCTION TECHNOLOGY	1	-	1
	TASAF	1		1
JUMLA KUU		**215**	**63**	**278**

KIAMBATANISHO "E"

TAARIFA ZA WAFANYAKAZI WALIOSTAAFU KAZI JULAI 2014 HADI MACHI 2015

	WAFANYAKAZI WALIOSTAAFU				**JINSIA**		**JUMLA**	**II**
	LAZIMA	HIARI	WALIOFARIKI	FANI	W/UME	W/WAKE		
		1		MSAIDIZI AFISA WA NYUMBA	1		1	
	-	-	-	-	-	-	-	
	2					2	2	
		1		MHUDUMU	1		1	
			1	DEREVA	1		1	
	1			TAARISHI	1		1	
	1	1		UTAWALA	2		2	
	11		1	UMEME	11	1	12	
	-	-	-	-	-	-		
	2				2		2	
	-	-	-	-	-	-		
		1	2	WALINZI WA KITUO	3	-	3	
	1			KATOGRAFA	1		1	
		2		WASAIDIZI WAPIMA	2		2	
	1			STORE KEEPER	1		1	
			1	MSAIDIZI MPIMA	1		1	
	-	-	-	-	-	-		
	19	**6**	**5**		**27**	**3**	**30**	

KIAMBATANISHO "F"

TAKWIMU ZA MAFUTA NCHINI KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 – MACHI 2015

A GAPCO – UNGUJA				
PETROL		**DIESEL**		**KERO**
OINGIZWA	**YALIOUZWA**	**YALIOINGIZWA**	**YALIOUZWA**	**YALIYOINGIZWA**
1,181,814	959,397	681,656	658,304	-
-	916,311	1,231,004	1,072,901	305,028
789,684	849,433	928,948	727,910	186,728
880,227	918,257	394,784	769,472	342,909
1,002,238	808,576	2,242,197	1,018,050	302,620
1,616,187	962,922	1,209,648	1,047,798	342,722
1,807,633	1,514,617	1,511,015	1,076,164	440,604
974,795	731,296	-	851,982	-
8,252,578	**7,660,809**	**8,199,252**	**7,222,581**	**1,920,611**
375,948	318,219	659,759	511,993	-
-	381,530	482,636	463,771	249,911
341,792	369,831	481,307	373,079	186,481
397,210	389,971	184,690	432,710	314,083
470,687	386,271	779,122	311,771	314,317
736,196	393,820	238,913	345,884	255,735
563,840	463,564	594,592	437,280	192,145
267,551	438,360	-	433,420	-

3,153,224	**3,141,566**	**3,421,019**	**3,309,908**	**1,512,672**

******** *Mwezi Machi kampuni haikuingiza mfuta*

2. ZANZIBAR PETROLEUM (ZP) – UNGUJA

OL		**DIESEL**		**KEROSENE**
OINGIZWA ted)	**YALIOUZWA (Soled)**	**YALIOINGIZWA (Imported)**	**YALIOUZWA (Soled)**	**YALIYOINGIZWA (Imported)**
996,292	849,947	1,261,955	711,963	631,58
626,693	934,793	-	704,600	
818,135	818,844	1,373,788	645,018	388,5
1,410,921	825,141	802,710	-	443,0
1,864,037	1,082,139	1,295,482	591,412	432,8
558,409	848,120		647,639	3,383,6
995,240	1,185,444	1,156,134	554,501	27,4
804,396	1,172,786	577,011	763,692	475,4
-	188,084	-	523,555	88,7
8,074,123	**7,905,298**	**6,467,080**	**5,142,380**	**5,871,2**

3. UNITED PETROLEUM (UP) – UNGUJA

	PETROL		**DIESEL**	
MONTH	**YALIOINGIZWA**	**YALIOUZWA**	**YALIOINGIZWA**	**YA**
JULAI	1,352,569	986,603	-	
AGOSI	1,566,041	1,120,219	2,473,625	
SEPTEMBA	-	953,305	-	1
OKTOBA	892,893	1,197,250	2,641,675	1
NOVEMBA	785,279	927,032		1
DISEMBA	888,399	1,074,874	2,608,577	1
JANUARI	573,268	762,640	1,237,513	1
FEBUARI	2,097,946	1,398,653	1,247,920	1
MACHI	1,178,407	1,166,306	1,138,066	1
TOTAL	**9,334,802**	**9,586,882**	**11,347,376**	

4. PUMA

	IK		**JET A - 1**	
MONTH	**YALIOINGIZWA**	**YALIOUZWA**	**YALIOINGIZWA**	**YA**
JULAI	-	-	-	

AGOSI	101,357	-	3,676,888	
SEPTEMBA	-	77,665	-	
OKTOBA	19,217	13,940	1,864,020	
NOVEMBA	-	29,859	-	
DISEMBA	45,147	1,384,597	1,853,904	
JANUARI	1,867,542	1,790,331	20,670	
FEBUARI	1,387,312	1,418,936	17,624	
MACHI	1,358,197	1,376,292	22,217	
TOTAL	**4,778,772**	**6,091,620**	**7,455,323**	

KIAMBATANISHO "G1"

MUHTASARI WA MATUMIZI KWA PROGRAMU KUU NA NDOGO 2015/2016

PROGRAMU		**PROGRAMU NDOGO**		**MAKADIRIO 2015/2016**	
				KAZI ZA KAWAIDA	**RUZUKU**
1	Mipango Utawala wa Ardhi	1	Mipango na Sera za Ardhi, Makazi, Maji na Nishati	161,884,000	-

	Makaazi Maji na Nishati	2	Utawala na Maendeleo ya Rasilimali Watu	804,252,000	-
		3	Uratibu wa Shughuli za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Pemba	1,018,229,000	-
		Jumla Ndogo		**1,984,365,000**	**-**
2	Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi	1	Utawala wa Ardhi	1,011,941,000	-
		2	Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi	270,055,000	-
		Jumla Ndogo		**1,281,996,000**	**-**
3	Uhifadhi wa Mji Mkonngwe, Uratibu na Usimamizi wa Ujenzi na Nyumba	1	Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi na Nyumba za Serikali	749,554,000	8,300,0
		2	Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe	360,047,000	-
		Jumla Ndogo		**1,109,601,000**	**8,300,0**
4	Usimamizi wa Huduma za Usambazaji wa Nishati na Maji		Usimamizi na Usambazaji wa Huduma za Maji na Nishati	271,638,000	2,543,000,0
		Jumla Ndogo		**271,638,000**	**2,543,000,0**
		JUMLA KUU		**4,647,600,000**	**2,551,300,0**

KIAMBATANISHO "G2"

MUHUTASARI KWA MIRADI 2015/2016

PROGRAMU		MRADI		MAKADIRIOY SMZ
1	Usimamizi wa Huduma za Usambazaji wa Nishati na Maji	1	Usambazaji Umeme Vijijini	1,500,000,000
		2	Kuijengea Uwezo Shirika la Umeme	
		3	Usambazaji Maji Vijijini	400,000,000
		4	Uimarisahji wa Sughuli za Maji Mijini	150,000,000
		5	Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji Awamu ya Pili	300,000,000
		6	Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira	350,000,000
		7	Utekelezaji wa Sera ya Nishati	200,000,000
		8	Utafiti wa Nishati Mbadala	300,000,000
		JUMLA		**3,200,000,000**

KIAMBATANISHO "G3"

MUHTASARI WA MAPATO 2015/2016

KIFUNGU	IDARA	KASMA	CHANZO CHA MAPATO
03	AFISI KUU PEMBA	1415003	Kodi ya nyumba za serikali
		1423005	Mauzo ya nyumba za serikali
		1422008	Utoaji wa viwanja na nyaraka
		1422023	Mauzo ya kokoto
		1422052	Malipo kwa huduma za kazi za useremala
			Jumla Ndogo
05	UJENZI	1415011	Ukodishaji wa mashine ya kokoto
		1422077	Malipo ya kazi za biashara
		1422078	Kodi ya makontena
			Jumla Ndogo
07	HIFADHI YA MJI MKONGWE	1422016	Vibali vya ujenzi
		1422077	Malipo ya kazi za biashara
			Jumla Ndogo
09	ARDHI NA USAJILI	1422044	Maombi ya fomu za viwanya
		1415002	Kodi ya ardhi kwa makampuni
			Jumla Ndogo
10	UPIMAJI NA RAMANI	1422008	Utoaji wa viwanja na nyaraka
			Jumla Ndogo
11	NYUMBA NA MAKAAZI	1415003	Kodi ya nyumba za serikali
			Jumla Ndogo
15	MRAJIS WA ARDHI	1422074	Utoaji wa kadi za usajili wa ardhi
			Jumla Ndogo
			JUMLA

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa hotuba yako. Waheshimiwa Wajumbe, nichukuwe fursa hii kuwashukuru kwa leo kwa wale ambao wamechangia michango yao mbali mbali kwa lengo la kuleta ufanisi katika shughuli za serikali.

Vile vile, nimpongeze Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote kwa kupitisha bajeti ya wizara yao. Mhe. Waziri, nikuombe tu kwamba kuna yale ambayo umeyaahidi na mwaka 2016 sio mbali. Kwa hivyo, kwa yale ambayo umeyaahidi Mhe. Waziri, tungekuomba sana uyatekeleze.

Baada ya kusema hayo machache Waheshimiwa Wajumbe, naahirisha kikao hiki mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:39 usiku Kikao kiliahirishwa mpaka tarehe 12/06/2015 saa 3:00 za asubuhi)